**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Tisa – Tarehe 7 Novemba, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 107

**Kuboresha Huduma Hospitali - Mtwara**

**MHE. MOHAMED S. SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni barabara ya lami kutoka Dar-es-Salaam – Mtwara - Mnazi Mmoja – Masasi – Mtambaswala imekamilika; na kwa kuwa, kukamilika huko kunaweza kusababisha ongezeko la magari na vilevile ajali za barabarani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma katika Hospitali kama vile Ikwiriri, Kilwa Kivinje, Hospitali ya Mkoa wa Lindi na Hospitali ya Masasi na kadhalika, ambako barabara hizo zinapita ili kuwahudumia watu watakaopata ajali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kuwaletea maendeleo wananchi wake ikiwa ni pamoja na kutengeneza barabara za lami. Kati ya barabara za lami zinazojengwa ni pamoja na ile ya Dar-es-Salaam – Mtwara – Mnazi Mmoja, Masasi – Mtambaswala, ambayo imeshakamilika. Haya ni maendeleo makubwa katika maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Spika, kwasababu barabara ni nzuri, ni dhahiri kuwa magari yanayopitia katika barabara hizo yataongezeka. Hata hivyo, naomba kumueleza Mheshimiwa Mbunge, kuwa, kwa vile barabara hiyo sasa ni nzuri isiwe ni kigezo cha ongezeko la ajali. Ajali ni kitu ambacho kinaweza kutokea wakati wowote. Rai yangu kwa madereva ni kwamba wawe waangalifu wakati wote na waendeshe kwa mwendo wa kawaida ili hata kama ajali itatokea inakuwa na athari kidogo. Aidha, kuna haja kwa Halmashauri zetu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi zikatoa elimu ya namna ya kutumia barabara ili kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma za Hospitali za Mikoa kwa kutoa fedha za kufanya ukarabati ili ziwe katika hali nzuri ya kuwahudumia wananchi kwa wakati wote. Katika mwaka 2008/2009, Serikali imeanza kutekeleza mpango mkubwa wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ambao lengo lake ni kujenga na kuboresha Vituo vya Ikwiriri, Kilwa Kivinje, ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja.

Madhumuni ya ujenzi na ukarabati huo sio kuhudumia ajali zinapotokea tu lakini ni ili kuvifanya vituo hivi viwahudumie wananchi wote wanapohitaji huduma za afya. Inapokuwa kwa bahati mbaya ajali imetokea, huduma kwa majeruhi zitakuwa nzuri zaidi na kwa wepesi wa kushughulikia dharura.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mikakati maalum ya ujenzi wa vituo vya afya katika kila kata:-

Je, Wizara au Serikali kwa ujumla, wanaweza wakashauriana na Wilaya husika ili waweke mikakati ya makusudi ili angalau kuweka vituo vya afya maeneo ya Mbwemkuru na Nangurukuru katika barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, kwamba kuna haja ya kuhakikisha kwamba vituo vyetu vya afya vinakuwa katika hali nzuri ili endapo panatokea matatizo kama haya anayozungumzia Mheshimiwa Mohamed Sinani, huduma zile ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, tunachoona hapa ni kwamba Serikali, imeshaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila kijiji kinakuwa na zahanati yake na wakati huohuo katika maeneo hayahaya ya barabarani kwa mfano juzi hapa nimetembelea Mkoa wa Ruvuma na Mheshimiwa Jenista Mhagama anafahamu, eneo la Madaba pale, tulikuwa tumeweka utaratibu na sasahivi tunaushughulikia, wa kuona kwamba huduma inayotolewa pale inakuwa ni nzuri ili ajali zinapotokea waweze kusaidiwa katika eneo hilo. Ni hivyo hivyo tunavyofanya katika eneo la Tumbi na katika maeneo anayozungumzia Mheshimiwa

Rished. Ni jambo ambalo linakubalika kabisa kwa maana ya kuimarisha huduma zinazotolewa katika zahanati na vituo vyetu vya afya.

Na. 108

**Elimu ya Uchafuzi na Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, hapa nchini kuna uharibifu mkubwa wa mazingira hususan katika vyanzo vya maji, maeneo ya maziwa na uchomaji moto misitu:-

(a)Je, Serikali hutenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira?

(b)Je, Serikali ina mpango gani kwa viongozi wanaotoa viwanja sehemu za vyanzo vya maji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silavanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna uharibifu mkubwa wa mazingira hususan katika vyanzo vya maji, maeneo ya maziwa na uharibifu wa ardhi na baionuai kutokana na uchomaji wa misitu. Serikali kupitia mkakati wake wa uhifadhi wa ardhi na vyanzo vya maji iliweza kubaini changamoto za kimazingira zilizopo katika uchafuzi wa ardhi, vyanzo vya maji, na uchomaji wa mapori na misitu na kuelekeza hatua mbalimbali za kushughulikia changamoto hizo. Ama kuhusu uchafuzi katika maeneo ya maziwa, tayari mkakati umekwishaandaliwa utakaoshughulikia uharibifu wa mazingira katika maeneo ya ukanda wa Pwani, bahari, maziwa, mabwawa na mito.

Mheshimiwa Spika, kimsingi suala la utoaji elimu kwa jamii ni suala muhimu sana, hivyo Ofisi Makamu wa Rais imetenga fedha kwa ajili ya shughuli hizi katika bajeti yake ya mwaka huu kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Idara ya Mazingira imetengewa shilingi 160,825,000/=;

(ii) Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira limetengewa shilingi 245,000,000/=; na

(iii) Mradi wa Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, *EMA,* zimetengewa shilingi 30,000,000/=.

Aidha Serikali hushirikiana na taasisi mbalimbali zisizo za Serikali kama vile *World Wide Fund for Nature, WWF* na *Wildlife Conservation Society for Tanzania, WCST,* pamoja na makampuni binafsi katika kutoa elimu ya mazingira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viongozi wanaotoa viwanja sehemu za vyanzo vya maji, kama anavyoeleza Mheshimiwa Mbunge, hawa wanavunja sheria kama wapo. Hivyo basi, kwa kuwa Serikali inazo sera, sheria na taratibu zinazosimamia masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira, sheria hizo zitaendelea kutumika kudhibiti na kuwaadhibu wanaovunja sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya itaendelea kuhimiza uandaaji wa uendelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kuhimiza uandaaji wa uendelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Vilevile tutaendelea kubaini ugawaji na uendelezaji wa ardhi unaofanywa kinyume cha sheria ikiwa ni pamoja na utoaji wa viwanja kwenye vyanzo vya maji ili kuwachukulia hatua wahusika hao kwa mujibu wa sheria zilizopo.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini Mheshimiwa Waziri, atakubaliana na mimi kwamba huu uchafuzi wa mazingira umekuwa sugu hasa kwenye maziwa.

Mheshimiwa Spika, ukikuta meli imefika pale bandarini wanafungua kinyesi kinaingia mpaka kwenye maji, samaki wanakula na sisi binadamu tunakula. Je, Serikali ina mikakati gani kudhibiti huo uchafu? Hilo swali la kwanza.

Swali la pili, uchomaji wa misitu umekuwa sugu, hsa Mkoa wa Kagera unaweza ukakuta vyanzo vyote vya maji watu wamegawa viwanja na watu wanajenga. Ikifika kipindi cha mafuriko watu wote wanakwenda na maji, je, Serikali ina mikakati gani na hizo pesa kweli zitafika kutoa elimu mpaka Kagera?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu uchafuzi katika maeneo ya maziwa na hasa katika Ziwa Viktoria, sisi Ofisi ya Makamu wa Rais, tayari tumendaa mkakati wa kuweza kushughulikia masuala ya usimamizi wa taka za aina mbalimbali ikiwemo taka za maji ambazo zinaingia katika maziwa na mito, lakini vile vile taka za viwandani, taka za kutoka katika mahospitali, taka za majumbani na taka zile za sumu. Kwa hivyo tayari tumeshawapa elimu Wakurugenzi wa Halmashauri zote na kuwaeleza jinsi ya kundaa utaratibu huo na tunawasaidia kuandaa utaratibu huo ili kuweza kudhibiti hali hiyo na tunashirikiana na Wizara ya Maji, katika kuhakikisha kwamba wanaweka utaratibu mzuri wa kuweza kuelekeza maji ambayo tayari yameweza kuchujwa kabla ya kuingizwa katika maziwa na katika mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ama kuhusu jinsi gani fedha zile zitakavyoweza kupelekwa katika Wilaya, sasahivi tuna mkakati mkubwa wa elimu endelevu kwa ajili ya mazingira. Mkakati huo unalenga kushirikisha taasisi na asasi na mashirika yasiyo ya kiserikali na waandishi ambao wanashughulika sana katika masuala ya mazingira mikoani, vijijini ili elimu hiyo iweze kufika kwa wingi zaidi kuweza kutoa hamasa na kuweza kuhakikisha kwamba suala la mazingira sasahivi linakuwa ni kipaumbele na kila mtu anakuwa ni askari na ni mlinzi wa mazingira, ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Mkoa wa Tabora, hususan Urambo Mashariki katika Kata ya Uyumbu, kumekuwa na vikundi vya ujasiriamali vya akina mama ambao wanahifadhi misitu na ambao wanahifadhi eneo kubwa kamavile Ngitili, ili kusiwe na uharibifu wa mazingira, wa wanyama, na kadhalika.

Je, Serikali, hususan mama, uko tayari kuwasaidia akinamama hawa ambao mpaka hivi sasa wanashinda porini kuhifadhi mazingira hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mhweshimiwa Mwanne Mchemba, dada yangu, kwanza kwa kumshukuru sana kwa uchapakazi wake na kuweza kutetea mambo mengi ya kimsingi katika Jimbo na kwa wanawake kwa ujumla. Lakini napenda kumhakikishia na kumuahidi dada yangu kwamba niko tayari kuja Urambo Mashariki na eneo zima la Tabora, kuweza kuwaona akina mama hao.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, kimsingi akina mama wameonekana ni chachu kubwa ya kulinda na kutunza na kuhifadhi mazingira. Nilikwenda Zanzibar, katika Jimbo la Kitope na niliona jinsi akina mama wa kijiji cha Uzuri, walivyoweza kufanya vizuri katika kulinda na kutunza mazingira yao na sisi Ofisi tuliwazawadia Sh.2,000,000/= kama changamoto na tunaahidi tutakuja Urambo, tutawaenzi na tutawahamasisha zaidi akina mama wote Tanzania waweze kutunza mazingira. *(Makofi).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa jibu zuri sana. Uhakikishe unatoa taarifa ili Spika awepo huko. *(Makofi/Kicheko).*

Tunaendelea Waheshimiwa, sasa ni zamu ya Wizara ya Miundombinu, swali linaulizwa na Mheshimiwa Pascal Costantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini.

Na. 109

**Kutengeneza Barabara ya Dalai – Goima – Mrijochini**

**MHE. PASCAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Dalai – Goima – Mrijochini, Wilayani Kondoa haijafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu, na kwa kuwa barabara hiyo hivi sasa ni mbaya na inapitika kwa shida sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara hiyo ili kuwarahisishia wananchi usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dalai – Goima – Mrijochini, yenye urefu wa kilometa 47.6 ni sehemu ya barabara ya Olbolot – Dalai – Kolo yenye urefu wa kilometa 118.84 ambayo ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara, *TANROADS*, Mkoa wa Dodoma. Serikali inatambua kwamba sehemu ya barabara hii kati ya Dalai na Mrijochini, *Olbolot*, yenye urefu wa kilometa 47.6 inapitika kwa shida hasa wakati wa masika. Hali hii imetokana na ufinyu wa bajeti kuifanyia matengenezo makubwa barabara hiyo.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitenga shilingi milioni 690 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu ya barabara kati ya Mrijochini – Dalai. Matengenezo yamefanyika katika sehemu ya barabara yenye urefu wa kilomita 33.6 ambayo yamehusisha ukarabati, matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi na matengezo ya muda maalum. Aidha, ujenzi wa madaraja mawili ya mfuto katika kijiji cha Chandama pamoja na makalavati 23 katika maeneo mbalimbali ya barabara hii yamejengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 204.594 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya kawaida na baada ya matengenezo hayo kufanyika barabara hii inatarajiwa kupitika kwa urahisi.

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, katika jibu lake amekiri kwamba katika kilometa 47.6 iliyofanyiwa matengenezo ni kilometa 33.6 na kilometa 14 bado hazijafanyiwa matengenezo; na kwa kuwa, eneo hilo ni kati ya kijiji cha Songoro na Dalai, ambako hasa wakati wa masika inakuwa ni sehemu kofi:-

Je, Waziri atanihakikishia ni namna gani atawahi kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha kuridhisha kabla ya mvua ama kabla ya masika? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, matengenezo ya aina tatu yamefanyika, kuna matengenezo ya kawaida, kuna matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum; na kwa kuwa sasa barabara inaonekana ina viwango tofauti tofauti, je, ni lini sasa barabara nzima itatengenezwa kwa kiwango cha matengezo maalum ili iweze kupitika kwa urahisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama niliovyoeleza katika jibu la msingi hapa kwamba mwaka huu wa fedha Serikali tena imetenga kiasi cha shilingi bilioni 204 ambazo zitaendelea kufanyia matengenezo barabara hii. Kwa hiyo, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Degera kwamba tutahimiza wenzetu wanaosimamia ujenzi wa barabara hii kwa kutumia fedha hizi ili matengenezo yaweze kufanyika haraka kabla masika hayajafika kama alivyosema.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nataka tu nimhakikishie, kama nilivyokuwa nimesema katika majibu ya msingi, kwamba kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana ndivyo tutakavyokuwa tunaitengeneza barabara hii kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa muda wote. Lakini kwa kweli, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara hii na barabara nyingine zote nchini zinatengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha lakini tatizo letu ni ufinyu wa Bajeti.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi lililoulizwa na Mheshimiwa Degera, matatizo yaliyopo kule Dalai, Goima na Mrijo ni sawasawa kabisa na yale yaliyopo katika barabara ya Shelui – Sekenke, ambayo inamilikiwa na *TANROADS* katika eneo la mto Kyenkang'ombe, maarufu kama mto Nzalala. Eneo hili ni korofi, *TANROADS* wamekuwa wakitengeneza wakifika hapo Zalala wanaruka na wanaendelea mbele, lakini hali inaendelea kuwa mbaya sana na inashindikana kupitika wakati wa masika:-

Je, Serikali inasemaje kuhusiana na eneo hilo ambalo imekuwa ikiliruka muda wote?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nataka tu nikubaliane naye kwamba matatizo haya ya ukorofi wa barabara katika baadhi ya maeneo, Serikali pia inaona kwamba ni kero. Kama nilivyokuwa nimesema na kama ambavyo tunaendelea kusema hapa kwamba nia yetu ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yanaleta kero katika barabara yanatengenezwa.

Kwa hiyo nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tunaona kwamba ni muhimu kutengeneza eneo hilo ambalo analisema lakini tushirikiane naye tu kwa

kutumia fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka huu katika mkoa huo wa Singida kama kutakuwa na fedha zimetengwa basi tuweze kusisitiza kwamba eneo hilo korofi litazamwe kwa ukaribu zaidi.

Na. 110

**Kampuni za Ukandarasi Kuomba Kazi Zaidi ya Moja**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa, sifa na uwezo ndio msingi wa Mkandarasi kupewa kazi; na kwa kuwa, Mkandarasi mmoja anaweza kupewa kazi zaidi ya moja katika sekta moja kama ya ujenzi wa barabara; na kwa kuwa, ipo tabia ya baadhi ya makandarasi kuwa na udhaifu katika kutekeleza miradi wanayopewa kwa wakati mmoja katika kiwango cha chini:-

(a)Je, ni kampuni zipi za makandarasi zilizoomba na kupewa kazi zaidi ya mradi mmoja katika sekta mbalimbali?
(b)Je, ni kampuni zipi zilizoonesha udhaifu katika ujenzi wa barabara na kupewa onyo au adhabu kwa kukiuka mikataba yao?

(c)Je, ni nini msimamo wa Serikali katika kukomesha tabia ya makandarasi kuomba kazi nyingi kwa kuonesha nyaraka zinazoonesha uwezo mkubwa wa kazi na badala yake uwezo mdogo kujitokeza wakati wa utekelezaji wa kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa uwezo ndio msingi unaotumika katika kumpa kazi Mkandarasi yeyote yule. Kwa hali hiyo, Mkandarasi anaweza kupewa kazi zaidi ya moja katika miradi ya ujenzi wa barabara endapo mkandarasi huyo atakuwa amekidhi matakwa ya zabuni husika na kuwa kupewa kazi hizo hakutaathiri utendaji kazi wa Mkandarasi huyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kampuni nyingi za makandarasi zimewahi kuomba na kupewa kazi zaidi ya moja katika miradi ya ujenzi wa barabara wa viwango mbalimbali

hapa nchini pamoja na kwenye sekta nyingine kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004.

(b) Mheshimiwa Spika, zipo kampuni kadhaa zilizoonesha udhaifu katika ujenzi wa barabara, zikiwemo kampuni za kizalendo, pamoja na kampuni za kigeni.

Mara nyingi kampuni hizi zimekuwa zikipewa onyo, adhabu au kusitishiwa mikataba pale zinapokiuka mikataba yao. Baadhi ya makandarasi waliopewa onyo au mikataba yao kusitishwa hivi karibuni kutokana na utendaji mbovu katika miradi mikubwa ya barabara ni kama ifuatavyo:-

(i) Kampuni ya *China State Construction Engineering Corporation Ltd*, ya China iliyokuwa ikijenga barabara ya Kagoma – Lusahunga, yenye urefu wa kilometa 154, iliondolewa katika eneo la mradi kuanzia mwezi Februari 2008 baada ya kushindwa kutekeleza ujenzi wa barabara kulingana na mpango wa kazi.

(ii) Kampuni ya *Prismo Universal Italiano S.P.A and Badri East Africa Enterprises Ltd. JV* iliyokuwa inajenga barabara ya Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika, yenye urefu wa kilometa 32, ilishindwa kutekeleza mradi huu kulingana na mkataba na mnamo tarehe 25 Machi 2008 Serikali kupitia Wakala wa Barabara, *TANROADS*,ilimuondoa mkandarasi huyo kutoka eneo la mradi.

(iii) Kampuni ya *Wesons Tanzania Ltd.* inayojenga barabara inayounganisha Babati na Wilaya za Simanjirona Kiteto imeshindwa kumaliza kazi katika muda wa mkataba. Kwa sasa Serikali kupitia Wakala wa Barabara, *TANROADS*, inakamilisha taratibu za kusitisha mkataba na kampuni hii.

(iv) Kampuni ya *Shabridin & Co. Ltd.* iliyokuwa inakarabati barabara ya Nanganga – Mandawa yenye urefu wa kilometa 45 kwa kiwango cha Changarawe ilishindwa kumaliza kazi kulingana na mkataba na Serikali kupitia Wakala wa Barabara, *TANROADS*, imesitisha mkataba na Mkandarasi huyu mnamo mwezi Septemba 2008. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (b) ya jibu la swali hili, makandarasi wanaokiuka mikataba huchukuliwa hatua mbalimbali kwa kuzingatia mikataba yao ikiwemo kuwaonya, kuwapa adhabu na kusitisha mikataba yao.

Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi nchini imeendelea kufuatilia utendaji wa makandarasi mbalimbali hapa nchini ili kubaini matatizo

yanayochangia utendaji wao wa kazi na wale wanaobainika kukiuka taratibu zilizoainishwa kwenye sheria ya usajili wa Makandarasi, hufutwa.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, kwamba je, atakuwa tayari kunipa taarifa zaidi kwa maandishi inayoonesha Kampuni ya *Wesons,* jinsi walivyopewa onyo, adhabu na kwamba Mheshimiwa Waziri, ataniarifu kwa kina na kwa maandishi mara baada ya Serikali kusitisha mkataba huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, sasa udhaifu umeonekana kwa makampuni yaliyotajwa:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba udhaifu huu hauhamishwi katika mikataba mingine ambayo wataomba? Serikali itachukua hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nataka nimuahidi ndugu yangu Omar Kwaangw', kwamba katika kushughulikia masuala haya ya umma, Serikali iko wazi kabisa. Kwahiyo, nimhakikishie tu kwamba taarifa hizi nilizompa hapa kwamba huyu mkandarasi atachukuliwa hatua tutampa kwa kina na adhabu atakayokuwa amepewa mkandarasi huyo. Kwa hiyo, nataka nimuahidi kwamba hiyo tutamfikishia kwa tarehe ambayo ataachishwa kazi huyo mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, la pili. Nataka tu niseme kwamba kwa hawa wakandarasi ambao watakuwa wamepewa maonyo, wengine wamesimamishwa kwenye kazi zao, Serikali inachofanya kwanza ina wa-*blacklist,* yaani kuwaweka katika orodha ya watu ambao wanatiliwa mashaka katika upatikanaji wa kazi na majina yao yanatangazwa nchi nzima ili wasiweze kupata kazi mahali pengine kama watakuwa wameshaonekana na hitilafu katika maeneo mengine.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, kwavile Wakandarasi wengi hukataa au kusita kufanya kazi katika maeneo fulanifulani kama vile Ludewa, kwa vile mazingira ni magumu na kusema kwamba gharama za ujenzi wa barabara katika maeneo hayo zinakuwa kubwa kuliko viwango vinavyowekwa na Serikali:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba gharama za utengenezaji barabara kwa kila kilometa zinaongezwa kwa kuzingatia ugumu wa maeneo ambayo barabara hizi zinatakiwa kutengenezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kabisa kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yapo katika mazingira ambayo baadhi ya Wakandarasi hukwepa kutokana na ukubwa wa gharama. Lakini nataka tu nimhakikishie kwamba katika mikataba hii ambayo inaandaliwa katika kupata Wakandarasi wa kutengeneza barabara mbalimbali nchini suala la mazingira ya maeneo hayo limezingatiwa. Kwa hiyo, nataka tu nimuhakikishie kwamba suala hili

litaendelea kutazamwa kila tutakapokuwa tunatoa kazi kwa wakandarasi kwa kuzingatia maeneo na mazingira ya sehemu ambako barabara hizo zipo.

Na. 111

**Kutengeneza Daraja la Mto Simiyu**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, daraja la Maligesu kupitia Kabila linatokana na Mto Simiyu liko chini sana na ni hatari kwa wananchi wanaopita kwenye minada:-

Je, Serikali haioni haja ya kubadilisha ramani ya daraja hilo ili lijengwe kwa kupita juu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, daraja la Mto Maligesu liko kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi – Maligesu – Kabila, yenye urefu wa kilometa 32. Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, ili kulifanya daraja hilo liwe la kudumu iko haja ya kubadili ramani ya daraja hilo ili lijengwe kwa kupita juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2008/2009, italifanyia daraja la mto Maligesu usanifu wa kina ili kulijenga kwa kiwango cha kudumu. Katika kutekeleza azma hiyo, jumla ya shilingi milioni 120 zimetengwa kwa ajili ya usanifu huo ambao utatoa makadirio ya gharama za ujenzi wa daraja hilo.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nashukuru kwamba hilo daraja wameshaanza kulifanyia kazi na usanifu unaendelea. Je, Serikali sasa inaweza ikanithibitishia kwamba usanifu huo utanyika haraka ili malori makubwa yanayopitisha pamba yasiwe yanapata adha katika daraja hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba maadam Serikali imeshaona tatizo liliko katika daraja hilo na kutenga fedha kama tulivyokuwa tumesema katika jibu la msingi hapa tutahimiza basi kazi hiyo ifanyike haraka ili hatima yake azma ile ya kulijenga daraja hili katika kiwango cha kudumu iweze ikatekelezwa na kuondokana adha hiyo ambayo anaisema Mheshimiwa Mbunge.

Na. 112

**Ugawaji wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wakala wa Bodi ya Pamba imelalamikiwa sana na wakulima kwa utaratibuwake mbaya wa ugawaji wa pembejeo za kilimo yaani mbegu na dawa, kwamba thamani ya mbegu na dawa huletwa pungufu ikilinganishwa na fedha zilizoko kwenye *pass book* na kwa kuwa anayegawa pembejeo hizo hawafahamu wakulima hivyo wakulima huibiana kwa kugushi saini, fedha inayobaki kwenye *passbook:*-

Je, Serikali inasema nini juu ya kero hiyo na malalamiko hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu suala la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatiwa kuwepo kwa soko huru nchini, mfumo uliokuwepo kwa kuwapatia wakulima wa pamba pembejeo zao za kilimo kwa njia ya mkopo na kuzilipia kwa njia ya makato kupitia kwenye mauzo ya pamba haukuweza kuendelezwa kwa kuwa mfumo huo hautekelezeki kwa urahisi katika soko la ushindani.

Aidha, uwezo wa wakulima kujiwekea akiba kwa ajili ya kujinunulia pembejeo hizo kwa fedha taslimu ulikuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto hii, wadau wa pamba kupitia Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba, walibuni utaratibu mbadala wa kumwezesha mkulima kujipatia baadhi tu ya pembejeo zake kwa ajili ya kilimo kupitia *pass book*. Chini ya utaratibu huu wakulima wakati wa kuuza pamba yao walishauriwa kutunza sehemu ya mapato yao kama akiba ya baadaye kwa ajili ya kununulia pembejeo zao hususan viuatiflifu na mbegu za kupanda. Utaratibu huu umetumia kwa kipindi cha takriban miaka minne hadi sasa. Hata hivyo, utaratibu huu ulikabiliwa na vikwazo mbalimbali kama ilivyoainishwa na Mheshimiwa Mpina.

Serikali baada ya kutambua hayo imeamua kutumia utaratibu mbadala ufuatao kwa kuanzia mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, wanunuzi wa pamba watachangia fedha kwa ajili ya ununuzi wa viuwadudu, na kwamba michango hiyo itakusanywa na Mfuko ili kupata unafuu wabei, kwa kufanya ununuzi wa pamoja kupitia Mfuko. Aidha, walitakiwa, kuhifadhi mbegu kwa ajili ya kupanda katika kiwango cha asilimia 8 ya pamba zilizozalisha msimu huu.

Wanunuzi wa pamba ndiyo watakaouza pembejeo kwa wakulima kwa fedha taslimu kwa kupitia Kamati zinazosimamia usambazaji wa pembejeo katika ngazi za kata na vijiji. Viongozi wa Wilaya na Tarafa, watajulishwa juu ya mgao wa pembejeo ili kuweza kusimamia vizuri usambazaji.

Mheshimiwa Spika, kwa wakulima watakaobainika kutokuwa na uwezo wa kujinunulia pembejeo, utaratibu wa kuwakopesha utatumika ambapo Halmashauri kupitia Serikali za Vijiji na Kata zitahitajika kuwadhamini kwa kuingia mkataba na msambazaji ili kuhakikisha wakulima hao wanalipa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba usambazaji wa pembejeo unasimamiwa kikamilifu, msambazaji atawajibika kuripoti kwenye uongozi wa Wilaya husika, ili kupata mgao wa pembejeo na utaratibu wa ugawaji na kuripoti kwenye Kamati za pembejeo katika ngazi ya kijiji na kata wakati wa kusambaza pembejeo hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwepo na udhaifu mkubwa katika usimamizi usambazaji wa pembejeo, Wilaya zitatakiwa kuhakikisha kwamba Kamati za pembejeo zinaundwa na zinatimiza wajibu wao.

Aidha, hatua zichukuliwe na kuwahamasisha wakulima kujiunga na *SACCOS* ili waweze kujiwekea akiba na kujinunulia pembejeo za kutosheleza mahitaji yao.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu huu wa wakulima kujilipia pembejeo kwa maana ya mbegu na dawa ni utaratibu mpya na kwa kuwa wakulima hawakufanyiwa maandalizi kwamba mwaka huu wangeweza kununua pembejeo kwa fedha tasilimu na kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wakulima watajinunulia pembejeo, wengine walio na uwezo watadhaminiwa na Halmashauri na kwa kuwa muda wa kupanda sasa umefika na utaratibu huu wa kufanya mchakato wa kuwapata wenye uwezo na ambao hawana uwezo ni mchakato mrefu:-

(a)Je, Serikali inaonaje kuwakopesha pembejeo hii wakulima kwa maana ya mbegu na dawa kwa mwaka huu wakati ikiandaa utaratibu mzuri wa pamoja wa miaka ijayo?

(b)Wakati unafutwa utaratibu wa *pass book* wakulima wengi walikuwa wamepunjwa fedha zao na mfumo huu, Serikali imefuta mfumo huo lakini wakulima bado wana madai makubwa ya fedha ambazo tayari wamechangia katika *pass book* na hazijarejeshwa mpaka sasa. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba haki za wakulima hawa hazipotei? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa pembejeo unatolewa kwa kadri tunavyoona mfumo fulani unafaa kama vile tulivyofanya mwaka huu kwenye mbolea tumewaandaa wakulima kwa semina mbalimbali hata katika wakulima wa pamba wamefanyiwa semina hiyo. Kwa

hiyo, hakuna mkulima katika maeneo wanayohitaji mbolea na dawa za pamba ambayo yanaweza yakapata mkopo kwa sasa hivi kutokana na utaratibu tulioandaa. Utaratibu uliopo ni ruzuku na ruzuku, ile dawa ya pamba inavyonunuliwa tayari ruzuku iko ndani yake. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tutaendelea na utaratibu huo wa kuota hizo dawa za ruzuku na kutokana na uwezo wa mkulima na itauzwa shilingi 2100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu mapunjo Serikali kupitia bodi pamoja na mfuko wa pamba imeshafanya tathimini na imeshagundua kwamba takriban shilingii milioni 65 zinahitajika kuwarudishia wakulima ambao walikuwa wamepunjwa. Hivi sasa zoezi hili linaendelea katika Wilaya hizo ambazo *pass book* ilikuwa inatumika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpina napenda kukuondoa wasiwasi kabisa zoezi hili linaendelea na tumeshahakiki kabisa wale watu ambao hawakughushi kwa kuongeza 0 ama kwa kuandika kwamba eka moja inatoa kilo 5000, hawa hawawezi kupewa chochote kwa sababu walifoji.

Na. 113

**Uanzishwaji wa Viwanda Vikubwa vya Zana za Kilimo**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, viwanda vingi tulivyokuwa navyo tumevifunga kwa sababu mbalimbali vikiwemo kiwanda cha UFI, kiwanda cha Nguo, Ngozi, Matunda na kadhalika; na kwa kuwa, asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania ni wakulima:-

Je, Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji ina mpango gani wa makusudi wa uhamasishaji wa viwanda vikubwa vya kutengeneza zana za kilimo na pembejeo ikiwa ni pamoja na kubadlisha matumizi ya kiwanda cha UFI kilichokuwa kinatengeneza majembe ya mkono na kukokotwa na ng’ombe?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa viwanda vya zana za kilimo na pembejeo na kama nilivyoeleza wakati wa kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, mwezi Agosti, 2008, Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vipya vya zana za kilimo na pembejeo ikiwa ni pamoja na kupanua uzalishaji wa mbolea ya *Phospahate* ya Kiwanda cha Minjingu na uanzishaji wa Kiwanda cha Mbolea Mtwara kwa kutumia gesi asilia. Aidha, kwa sasa mchakato wa kupata mwekezaji wa kuanzisha kiwanda cha mbolea kwa kutumia gesi asilia Mtwara unaendelea na umefikia hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *UFI* kwa sasa kinazalisha mabomba ya maji yenye kipenyo kikubwa. Serikali imefanya mazungumzo na mwekezaji ili azalishe majembe ya kukokotwa na ng’ombe (Plau).

Mwekezaji anatarajiwa kuanza uzalishaji wa majengo ya kukokotwa na ng'ombe mwaka 2009. Mchakato wa kuagiza malighafi zinazohitajika kutengeneza (plau) unaendelea.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza kwa sababu swali la msingi hapa ni kwamba nataka kiwanda cha kutengeneza majembe ya kukokotwa na ng'ombe na majembe ya mkono ni sababu zipi zilizopelekea kiwanda cha *UFI* kubadilishwa matumizi kutoka kwenye kiwanda cha kutengeneza majembe na kuwa kiwanda cha kuzalisha mabomba?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, sababu iliyopelekea kiwanda cha *UFI* kubadilisha aina ya uzalishaji ni gharama kubwa za uzalishaji na pili ilikuwa ni ushindani mkubwa wa vifaa vya kilimo kutoka China.

Lakini baada ya Serikali kuona umuhimu wa kuwa na kiwanda chetu hapa Tanzania ambacho kitatengeneza zana za kilimo ambazo zitaendana na hali halisi ya ardhi yetu.

Vilevile zana hizo zitaweza zikalimiwa na wakulima wetu. Ndiyo maana nikasema kwenye jibu langu la swali la msingi kwamba Serikali imeingia tena katika mazungumzo na mwekezaji mpya na ikumbukwe hapa kwamba Serikali ilishindwa kuendesha kile kiwanda tukapata hasara na huyu mwingine naye akapata hasara na kubadilisha aina ya utengenezaji ndio tumeona umuhimu wa kuingia naye katika mazungumzo tena ili pamoja na kuzalisha bomba aongeze na plau ili kwa pamoja hata kama plau itampa hasara lakini lile bomba limpe faida ya kwa ujumla aweze kupata faida kidogo aweze kunufaika na wananchi wa Tanzania waweze kunufaika.

Na. 114

**Kujenga Soko la Mazao Korogwe Magharibi**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Korogwe Vijijini limegawanyika katika pande mbili kuu za Mashariki na Magharibi na kwa kuwa Serikali chini ya Programu ya Uendeshaji na Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo imefadhili ujenzi wa soko la kisasa la mazao upande wa Magharibi katika kijiji cha Makuyuni:-

(a)Je, Serikali chini ya programu h iyo haioni haja ya kujenga soko kama hilo upande wa Mashariki kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara ukanda huo?

(b)Kwa kuwa programu hiyo hujumuisha pia matengenezo ya barabara katika eneo husika, je, Serikali itakuwa tayari kujumuisha barabara za Kerenge, Makumba, Magoma na Kizara-Kwetonge katika programu hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Programu ya Uendekezaji Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimio *(Agricultural Marketing Systems Development Programme (AMSDP)* iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutumia mfumo shirikishi ambapo mchakato mzima wa uamuzi wa mradi wa kipaumbele kwa eneo husika hufanyika kwa kuzingatia mapendekezo ya wadau kupitia vikao vya Halmashauri ya Wilaya husika. Utaratibu huu ndiyo uliowezesha ujenzi wa soko la kisasa katika Kijiji cha Makuyuni kupitia programu ya Uendelezaji Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo Wilayani Korogwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu huu kuwa mzuri na unaokubalika, utekelezaji wake unategemea upatikanaji wa fedha. Halmashauri husika zimekuwa zikitengewa kiwango cha fedha kutegemea ukomo wa Bajeti ya Serikali. Hivyo, miradi iliyoibuliwa na kutekelezwa Wilayani Korogwe iliendana na ukomo huo wa bajeti. Wito wa Serikali ni kuzitaka Halmashauri za Wilaya nchini kuendelea kuibua miradi ya uendelezaji wa miundombinu ya masoko ikiwa ni pamoja na soko upande wa Magharibi wa Jimbo la Korogwe na barabara za Kerenge, Makumba, Magama na Kizara –Kwetonge na kubainisha vyanzo vingine vya fedha na hatimaye kutenga fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano kwa Mheshimiwa Mhina na kwa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe pale itakavyotakiwa kufanya hivyo, hususan katika kutoa ushauri wa kitaalamu utakaowezesha soko hili kujengwa.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kama nilivyoeleza mwanzoni kwamba programu hii inahusisha matengenezo ya barabara na tunashukuru sana kwa upande wa Magharibi barabara ya Bagai-Zege inayojengwa hivi sasa inajengwa katika kiwango cha kuridhisha.

Lakini katika barabara ya Welei, Lutindi hadi Bluu imekwishakamilika lakini cha kushangaza barabara ile haina mifereji na tunaelewa wazi kwamba uimara wa barabara ni mifereji je, Wizara inasemaje kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hilo analosema Mheshimiwa Mhina kwamba ukijenga barabara halafu ukaacha kuweka mifereji ya kuchua maji yale hasa wakati wa mvua basi ile barabara pamoja na ubora wake haidumu sana.

Mimi napenda kumshauri Mheshimiwa Mhina na kwa kweli huu ni msimamo wa Serikali kwamba kama vile ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe iliomba fedha ikapata ikajenga hizo barabara, mimi nina uhakika kwamba bado iko nafasi kwa Halmashauri ya Korogwe kwa sasa kuomba fedha kwa ajili ya kutengeneza mifereji ili kuhakikisha kwamba barabara hiyo inakuwa imara na ya kudumu na haiharibiki mara kwa mara. *(Makofi)*

Na. 115

**Upungufu Mkubwa wa Mahakimu Nchini**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, inadhihirika wazi kuwa, nchi yetu ina upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama mbalimbali, hali inayosababisha watu wengi kutopata haki zao kwa wakati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa (Mfenesini) kama ifuatavyo:-

Serikali inakiri upungufu wa Mahakimu wa Mahakama mbalimbali unaosababisha Hakimu mmoja kuhudumia zaidi ya Mahakama moja na hivyo kuathiri utendaji wake wa kazi kusababisha baadhi ya watu kutopata haki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mahakama ina mkakati wa kutatua tatizo la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Mkakati huo ni kwanza kuajiri

Wahitimu wa Stashahada ya Sheria kutoka Chuo cha Lushoto hasa wale wanaojisomesha wenyewe na wanaomaliza katika vyuo vingine.

Pili, ni Serikali kuongeza udhamini wa wanafunzi ambao wakimaliza masomo wataajiriwa na Mahakama moja kwa moja tofauti na ilivyo sasa ambapo wahitimu wengi hawako chini ya udhamini wa Serikali na hivyo hawalazimishwi kuajiriwa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, tatu ni Serikali kupitia Mahakama kuwaajiri kwa mkataba Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo waliokwishastaafu na wenye sifa nzuri ambao bado wana nguvu za kuweza kuitumikia nchi. Serikali inaamini kupitia mikakati hii itapunguza tatizo kubwa la uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Aidha, Serikali itaendelea kuajiri Mahakimu Wakazi kulingana na mahitaji. Kwa kuwa Kada ya Mahakimu wa Wilaya haipo tena katika muundo wa utumishi (*dying cadre),* Serikali sasa inapeleka Mahakimu Wakazi katika ngazi ya Wilaya.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa kuwa Serikali imekiri kuwepo na upungufu huo na kwa kuwa Serikali hivi sasa ina mikakati ya kuondosha tatizo hilo, je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili mikakati hiyo itaanza lini na imepanga bajeti ya kiasi gani?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, hiyo mikakati ambayo nimeelezea hapa tumeshaanza kuitekeleza, sina takwimu ya gharama za bajeti ambazo zitatumika katika kutengeneza mkakati huo. Lakini baada ya hapa Mheshimiwa Mbunge anipe muda nitamtafutia takwimu hizo halafu nitampa.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, kwa kuwa liko tatizo la Mahakimu kwenye Mahakama zetu sambamba na tatizo hilo pia kuna matatizo makubwa ya Mawakili wa Serikali waliowengi kuacha kazi ama kuanzisha makampuni yao binafsi ama kufanya kazi zingine nje ya Serikali je, Serikali inaweza ikatueleza kwamba tatizo ni nini hasa la Mawakili wengi kuacha kazi Serikalini na kwenda kuanzisha kampuni zao binafsi au kufanya binafsi ukiacha Serikali wakati ukizingatia wamesomeshwa na Serikali kwa gharama kubwa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli hivi sasa tuna matatizo ya ku-*retain* Mawakili wa Serikali katika utumishi wa umma.

Hii inatokana na mazingira ya utendaji kazi, mishahara na marupurupu hayawatoshelezi, kwa hiyo wanafikiri kwamba wakienda nje ya Serikali wanaweza

kupata masiaha bora zaidi lakini hivi sasa Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba inabadilisha mazingira ya kazi ya Mawakili wa Serikali.

Kwa hiyo, tunaamini kwamba muda ujao ambao sio mrefu kuanzia sasa Mawakili hao hawataondoka tena katika utumishi wa Serikali kwenda nje kutafuta maslahi ni bora zaidi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na matatizo ambayo tumefahamishwa nilikuwa naomba niulize swali dogo, kwa kuwa mara ya mwisho tulivyotembelea katika maeneo ya Geita *Mine* mpya kuna watu ambao wanaishi kwenye mazingira magumu kutokana na kesi yao kuchukua muda mrefu, kesi ya fidia katika migodi na kwa kuwa sasa sehemu ile imegeuka kuwa ni kijiwe cha vyama mbalimbali kwenda kujinadi pale kutumia zile hisia za wale ambao wanadai pale:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za makusudi kumaliza kesi ile ili kuondoa kijiwe kile?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, nimepokea tatizo lililoko Geita tutalifanyia kazi.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii imekuwa kwa muda mrefu inafanya kazi yake chini ya kiwango kwa maana utatuzi wa kesi mbalimbali kutokana na upungufu huu unaozungumzwa katika swali la msingi upungufu wa Mahakimu na Mahakama na kwa kuwa wako Mahakimu wengi ambao wamestaafu lakini bado wana uwezo na nguvu ya kuweza kutumikia Taifa:-

Je, Wizara hii haioni haja ya kuwarejesha wale hata kwa mikataba ili kujaribu kuondoa upungufu wa Mahakimu ulioko sasa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea, huo ni mmojawapo wa mkakati wetu wa kuhakikisha kwamba tunaondoa uhaba wa Mahakimu ulioko kwa sasa hivi na kama nilivyokuwa natoa jibu langu ni kwamba mkakati huo umeshaanza kufanyiwa kazi hivi sasa.

Kwa hiyo tunaangalia tukipata Mahakimu ambao wana sifa kuweza kuajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo au kuendeleza utumishi wao baada ya kustaafu basi hao wataajiriwa tena na Mahakama ili waweze kuendelea kuhudumia wananchi.

Na. 116

**Matumizi ya Kiswahili Yaliyochanganyika na Kiingereza**

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, matumizi ya Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza (Kiswaingilishi) yanashamiri sana hapa nchini na kutumika hata katika maeneo rasmi:-

(a) Je, kuna athari zipi kitaifa kwa matumizi ya Kiswaingilishi?

(b) Je, Serikali ina mkakati wowote wa kutokomeza Kiswaingilishi ili kutoa fursa kubwa ya kuendeleza Kiswahili halisi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijbu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nasita hata kutamka au kulitumia neno Kiswaingilishi katika kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kwani kwa kufanya hiyo kutaashiria kulikubaliki neno hilo kama neno rasmi la Kiswahili.

Hata hivyo, napenda kusema kwamba zipo athari nyingi ambazo taifa letu linazipata kutokana na kuchanganya matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza au na lugha nyinginezo. Athari hizo ni pamoja na hizi chache zifuatazo:-

-Kutowafikia walengwa ujumbe sahihi unaotolewa ukizingatia ukweli kwamba, wananchi wengi hawaelewi lugha ya Kiingereza au lugha nyingine itakayochanganywa;

-Matumizi hayo yanamnyima mwananchi fursa ya kupata habari muhimu;

-Matumizi hayo yanapotosha maana na ufasaha wa lugha yenyewe, iwe ya Kiswahili au Kiingereza; na

-Wananchi hususan vijana na watoto wanapandikizwa maeneno ambayo sio lugha rasmi kulingana na jisni yanavyotumika.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua tatizo lililopo la matumizi ya Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza, ina mikakati mbalimbali yenye lengo sio tu kutokomeza matumizi ya lugha ya Kiswahili iliyochanganyika na Kiingereza au na lugha nyingine ili kutoa fursa kubwa ya kuendeleza Kiswahili halisi, bali pia kujua matumizi ya maneno ya lugha ya kiswahili na maana yake mkakati hiyo ni pamoja na:-

-Kurusha hewani vipindi vya Redio na Televisheni vinavyojadili matumizi ya maneno ya Kiswahili na maana sahihi ya maneno hayo;

-Kuchapa machapisho mbalimbali kama vile kamusi ya Kiswahili na vitabu vyenye kuonyesha maana sahihi ya maneno ya kiswahili na matumizi ya lugha yenyewe;

- Kufundisha shuleni na vyuoni lugha ya Kiswahili kama somo; na

-Kuandaa semina, kongamano na mikutano mbalimbali ili kujadili masuala mbalimbali kama vile matumizi ya maneneo ya lugha ya Kiswahili na ujenzi wa sentensi kwa kutumika maneno mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala la matumizi ya Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza au lugha nyingine limekuwa likizungumziwa mara nyingi baada ya kuonekana yanashamiri sana hapa nchini hususan kwenye muktadha mbalimbali kama vile mikutano ikiwemo hii inayofanyika hapa Bungeni na mikutano mbalimbali ya kitaifa humu nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kupitia Bunge lako Tukufu kwa wananchi na hasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuacha kuzungumza Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza au lugha nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba walichukulie suala hili kwa umuhimu wake kwani tatizo hili linajitokeza kwa kiasi kikubwa hasa hapa Bungeni wakati tunapojadili mambo nyeti na muhimu kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana pia nimpongeze kwa kutorasimisha neno Kiswaingilishi ambalo hata mimi mwenyewe sikulirasimisha na ndio maana katika kuliandika nililiwekea alama ya kufunga na kufungua ili kutolirasimisha. Hata hivyo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Miswada yetu ya Sheria inawasilishwa hapa Bungeni kwa Kiingereza na hivyo inakuwa vigumu wananchi kufuatilia mijadala inayoendelea hapa Bungeni, ni lini Serikali itawasilisha Miswada kwa Kiswahili ili wananchi waweze kufuatilia vizuri na kuzielewa vyema sheria zetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa hata maneno ya Kiswahili bado mengine hayatumiwi kwa usahihi, Serikali inatoa wito gani ili kuhakikisha hata maneno ya Kiswahili tunayatumia kwa ufasaha nikitolea neno moja tu ambalo tunalikosea sana, neno upungufu linatumiwa sana kama mapungufu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana na ahsante kwa kutupa elimu kidogo katika masuala ya lugha, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu yako yasiwe na mapungufu. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikubaliane na yeye kabisa kwamba Miswada mingi inaandikwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza na kama Mheshimiwa Mbunge atakumbuka ndani ya Bunge hili Wabunge wengi wameomba kwamba Miswada sasa iandikwe kwa Kiswahili. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subiri Serikali inajitahidi kuweke mikakati ya kuweza kufanikisha Miswada iandikwe kwa lugha ya Kiswahili, kwa sasa hivi bado tuko katika harakati za kujiandaa kuweza kufanikisha zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nakubaliana na yeye kabisa kwamba maneno mengi yanatumiwa visivyo si Kiswahili sahihi, lakini ni vizuri tukajua kwamba nchi yetu hii wananchi wetu wana lugha za aina tatu kuna lugha za kijamii tuna jamii zaidi ya 100, makabila zaidi ya 100 lakini pia tuna Lugha ya Taifa ambayo ni Kiswahili na lugha za kigeni kwa hiyo inatokea tu hata lafudhi kwa mfano kama ndugu yangu Mheshimiwa *Dr*. Mlingwa aliyeuliza swali, ni mtani wangu, yeye ni msukuma hata akiongea tu utajua kwamba anazungumza zungumza Kisukuma, yaani vitu kama hivyo vinatokea.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba ni sisi kubadilika na kuzungumza Kiswahili fasaha na pia tujifunze kuwa na utaratibu wa kusoma kamusi kwa sababu kamusi inaelezea wazi kabisa matamshi na lugha halisi ambayo inatakiwa izungumzwe.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matumizi ya Kiswahili kilichochanganyika na Kiingereza kinatumiwa zaidi na tabaka na watu ambao wamefikia elimu ya juu pamoja na wanafunzi katika maeneo ya elimu ya juu pamoja na wale watu ambao wamebahatika kuishi nje wakawa wamerejea nchini:-

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kama hii ni hulka ya hao watu na itakuwa ni ngumu sana kuibadilisha?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kabisa kwamba watu waliofika kiwango cha juu cha elimu na watu ambao wamekaa labda nje muda mrefu kutokana na mazingira walikotoka wanajikuta wanazungumza hata sauti zinabadilika kutokana na mazingira aliyokuwa nayo huko. Lakini mimi nataka nitoe wito kama nilivyosema tubadilike, tuzungumzeni Kiswahili kinachostahili hata kama umekaa nje miaka 100 basi kumbuka kwenu. (*Makofi*)

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, wakati tupo shule sisi kule Zanzibar tuliambiwa kwamba Kiswahili fasaha kinazungumzwa pale Zanzibar Mjini na katika masomo yote tulisomeshwa maneno kama *hospital*, *motorcycle, school* na kadhalika.

Je, Waziri anasema kuhusu hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, haya maneno ni sahihi, *school* na ...

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, alichozungumza ni sahihi, nataka nitoe tu hali halisi, nimezungumza hapa kwamba baadhi ya maneno ya Kiswahili tumeyatohoa kutoka lugha mbalimbali kwa

mfano unakuta Kiswahili kina Kiarabu, Kiswahili kuna Kireno, Kiswahili kuna Kiingereza, kuna Kifaransa tumetohoa kutoka katika lugha mbalimbali. Kwa hiyo, baadhi ya maneno yanayotamkwa yamo kama *school*, Zanzibar *school* ni Kiswahili sahihi kabisa, marikiti, ni neno sahihi kabisa kwa hiyo tumetohoa kutoka lugha mbalimbali. (*Makofi*)

Na. 117

**Ujenzi wa Utamaduni wa Taifa**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa utamaduni wowote wa asili ni nguzo ya uhai wa Taifa lolote:-

(a) Je, kwa nini kasi ya kurekodi nyimbo za asili kwa vyombo vya habari ni ndogo sana?

(b) Je, kwa nini Maafisa wa Utamaduni na Michezo ambao ni muhimu katika ujenzi wa utamaduni wanaonekana kama hawahitajiki katika Utumishi wa Umma kwa kutowatumia ipasavyo?

(c) Je, nini mipango ya baadaye ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuimarisha utamaduni katika shule, vyuo taasisi na hasa katika vyombo vyetu vya habari?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), ( b)  na (c) kama ifuatavyo:-

(a )Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kasi ya kurekodi nyimbo za asili kwa vyombo vya habari ni ndogo sana. Sababu ya msingi ya kuwepo kwa hali hiyo inatokana na vyombo hivyo kufanya kazi ya kibiashara zaidi badala ya kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia wajibu wa vyombo hivyo.

Hivi sasa vimeanzishwa vikundi vingi vya nyimbo za muziki wa dansi, taarabu na injili, jambo ambalo limezua ushindani mkubwa wa kibiashara wa kurekodi nyimbo hizo na kuziuza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile sanaa ya muziki wa dansi na nyimbo hivi sasa inatoa ajira na vyombo vinavyofanya kazi ya kurekodi kazi za wasanii navyo vinafanya biashara, nyimbo za asili zimeonekana hazina soko kubwa kiasi kwamba, kasi ya kurekodi nyimbo hizo kuwa ndogo.

(b)Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Maofisa Utamaduni na Michezo wamekuwa hawatumiki ipasavyo katika shughuli za fani zao ambazo ni muhimu katika ujenzi wa Taifa letu. Sababu ya msingi ni kwamba Halmashauri za Wilaya hazitengi fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali zinazohusu utamaduni na michezo na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu mbalimbali yanayohusiana na ujenzi wa utamaduni na michezo. Hata hivyo kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta hizo katika ujenzi wa Taifa letu, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda (Mb) tayari ameshaziagiza Halmashauri zote nchini kutenga fedha zitakazotumika kuendeleza shughuli za utamaduni na michezo. Ni matumaini yangu kwamba agizo hili litatekelezwa ili Maafisa hawa waweze kufanya kazi zao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge ambao pia ni Madiwani katika Halmashauri zao kuhakikisha kuwa, fedha zinatengwa kwa ajili ya shughuli za kuendeleza utamaduni na michezo.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuimarisha Utamaduni katika shule, vyuo, taasisi na hasa katika vyombo vyetu vya habari, Wizara yangu katika kutekeleza Sera ya Utamaduni, inahimiza kuendeleza stadi za kazi kwa vijana shuleni na vyuoni na kutambuliwa kwa mfumo wa jadi wa utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa Walimu na viongozi wengine wa sekta ya utamaduni na michezo ili waweze kufundisha shuleni na vyuoni na vikundi mbalimbali vilivyoundwa ili kuendeleza sekta hizo. Vile vile, Serikali itaendelea kuhamasisha vyombo vya habari ili viendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa michezo na utamaduni.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Waziri mwenyewe amesema nyimbo za asili hazina soko ndio maana kasi ya kurekodi ni ndogo:-

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kuwa tulipounda Mfuko wa Utamaduni kwa Taifa shabaha na madhumuni ilikuwa ni kuendeleza hayo aliyokuwa anasema Mheshimiwa Waziri na Sweden ikachangia bilioni 1 kwa kutambua umuhimu wa utamaduni?

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami ya kwamba kwa kuanzia, tumia mfuko huo kwa kusaidia Mkoa wa Rukwa na Mkoa jirani wa Tabora ili wafanikishe azma ya kujenga utamaduni katika Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa hali ya utandawazi imeanza kuwa utamaduni wetu na mila na desturi katika nchi hii na kusababisha ufisadi, uchoyo, ubinafsi na kukosa heshima miongoni mwa viongozi wetu:-

Je, Waziri atafanya mpango wa kukusanya viongozi mbalimbali wakiwemo wa siasa ili tabia ambayo imeanza kujengeka ya viongozi wetu kudharauliwa hata na watu wadogo iweze kutafutiwa dawa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, kwa lile la pili una kazi kubwa kweli kweli. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikubaliane naye kwamba kwa kuuenzi utamaduni na kuendeleza utamaduni katika nchi yetu Serikali yetu imeona ianzishe Mfuko wa Utamaduni. Mfuko wa utamaduni upo na unaendelea. Ni kweli alichosema kwamba Serikali ya Sweden inatusaidia na hapa katikati ndio imeacha, lakini Serikali yetu pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kuheshimu hiyo katika bajeti ya mwaka huu wametutengea milioni 200, ni chache lakini zipo na mfuko unaendelea na kama mtakumbuka wakati wa bajeti Wizara yangu ilileta hapa kitabu kuonyesha miradi yote ambayo imegharamiwa na Mfuko wa Utamaduni katika nzima.

Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane naye kabisa kwamba tutajitahidi kama Wizara kuona kwamba Mkoa wa Rukwa na Tabora basi na wao wanafaidika na Mfuko wa Utamaduni katika kuendeleza utamaduni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nataka nikubaliane naye katika hali ilivyo sasa hivi katika utandawazi kuna maandishi na kuna maneno mengi sana ambayo yanazungumzia kuhusu viongozi na kudhalilisha viongozi kuhusiana na neno ufisadi.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme wazi sisi kama Wizara ambao tunahusika na habari, tutaendelea kutoa elimu kwa kutumia vyombo vyetu vya habari kuona kwamba suala la ufisadi basi litumiwe vizuri, hatuwezi kukubali viongozi wetu wa nchi hii ambao tunawachagua wenyewe tena kwa asilimia kubwa wadharauliwe au kuzungumzwa ovyo katika vyombo vya habari au na wananchi kutumia maneno haya, tutajitahidi tutakapopata fedha kuona kwamba tunafanya kwa awamu kuhakikisha kwamba viongozi tunawapa elimu ili angalau waone kwamba viongozi wetu wanaheshimiwa na neno hilo halitumiki vibaya. (*Makofi*)

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wapiga densi wanakuwa na wanenguaji kwenye majukwaa na kwa kuwa wanenguaji hao ni wa jinsia mbili wanaume na wanawake na kwa kuwa wanaume wanavaa vizuri mavazi ambayo yanaficha miili yao na wanenguaji wanawake wanavaa mavazi ambayo yanaonyesha kuwa ni nusu uchi:-

Je, Wizara haioni kwamba wanawake hao wanawadhalilisha wanawake wa Kitanzania ambapo huu sio utamaduni wa Kitanzania? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, inaelekea Mheshimiwa Nuri Bafadhili naye ni shabiki anaangalia angalia mambo hayo. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, anachokizungumza ni kweli kwamba wanaonengua katika dansi kuna jinsia ya kike na ya kiume na akina mama au wanenguaji wadada nguo zao kidogo hazileti heshima, Wizara imeliona hilo, Baraza letu la Sanaa BASATA limeshatoa onyo na sisi Wizarani tumetoa onyo, tumeomba miziki ya dansi wavae nguo ambazo hazitii aibu wala haimdhalilishi mwanamke, tutaendelea kuweka mkazo huo ili na wakina mama nao wavae nguo zinazotoa heshima. (*Makofi*)

Na. 118

**Tatizo la Kukatika kwa Umeme**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mji wa Kahama kuna tatizo sugu la umeme kukatika mara kwa mara hasa wakati wa masika kutokana na uchakavu wa nguzo za umeme na kwa kuwa, hali hiyo husababisha usumbufu, hasara na vifo kwa wananchi:-

(a) Je, kwa nini Serikali hailishughulikii tatizo hilo la muda mrefu?

(b) Je, ni kwa nini chanzo cha tatizo hilo na pia ni hasara kiasi gani imepatikana kwa watumiaji wa umeme na Serikali kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1981 Mji wa Kahama unapata umeme wa gridi ya Taifa kutoka kwenye kituo cha Ibadakuli mjini Shinyanga kilichopo umbali wa kilometa 110 kutoka Mji wa Kahama. Mahitaji ya umeme ya Mji wa Kahama bila kuhusisha migodi mikubwa inayopata umeme wake kupitia njia za KV 220 ni MW 4.5.

Kwa kuzingatia umri wa njia hii ya umeme inayopeleka umeme katika Mji wa Kahama ambayo ilianza kujengwa mwaka 1980 ni wazi kuwa njia hii kwa sasa imechoka na inahitaji matengenezo makubwa.

Kwa kipindi cha takriban miaka miwili sasa tatizo la kukatika kwa umeme limekuwa likijitokeza mara kwa mara. Hali hii inasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi kwani mara umeme unapokatika, shughuli zao husimama na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa hali yao kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kukatikakatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ukiwemo Mji wa Kahama ni tatizo ambalo Serikali inalifahamu na imeshaanza kulitafutia ufumubuzi. Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* imeweka mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kupanua na kukarabati miundombinu ya umeme ikiwemo ya Mji wa Kahama alioutaja Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikisha kuwa wateja wote wanapata umeme ulio bora na wenye uhakika.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo yamefanyika katika kuhakikisha kuwa Mji wa Kahama unapata umeme wa uhakika ni ubadilishaji wa nguzo 50 za njia kubwa ya umeme na nguzo 28 za njia ndogo ya umeme. Vilevile transifoma nane (8) zilibadilishwa kutoka mfumo wa *KV 11* kwenda mfumo wa *KV 33* ili kuongeza nguvu ya umeme. Kazi hii ambayo ilifanyika mwaka jana 2007 iligharimu shilingi milioni 71 za Kitanzania. Katika kipindi cha mwaka huu, kazi ya kubadilisha nguzo zilizooza inaendelea. Jumla ya nguzo 68 za njia kubwa ya umeme na nguzo 22 za njia ndogo ya umeme zimekwishabadilishwa. Aidha, transifoma tatu (3) zimeongezwa nguvu kutoka KVA 50 za awali na kuwa *KVA 200.* Kazi hii hadi itakapokamilika itagharimu kiasi cha shilingi 35,377,344.40.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* Mkoa wa Shinyanga Mkoa wa Shinyanga imepanga kutenga kiasi cha shilingi 97,644,538.00 kwa ajili ya ujenzi wa njia mpya ya umeme kutoka kituo cha *KV 220* cha Buzwagi kwenda Kahama Mjini. Hali hiyo itafanya umeme wa Kahama mjini kuwa wa uhakika zaidi ukilinganisha na njia ya sasa inayotoka Shinyanga umbali wa kilometa 110.

(b) Mheshimiwa Spika, chanzo cha tatizo ni kutowekeza kwenye miundombinu ya umeme kwa kipindi kirefu na kusababisha miundombinu kuchakaa au kuzidiwa nguvu kutokana na mahitaji ya umeme kuendelea kukua mwaka hadi mwaka. Kukatikakatika kwa umeme kumekuwa kunasababisha hasara kwa wateja, hususan, wale ambao wanatumia umeme kwa ajili ya kuzalisha mali na shughuli za biashara. Aidha, *TANESCO* imekuwa inakosa mapato kutokana na kukatika kwa umeme na Serikali imekuwa inakosa mapato yatokanayo na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*).

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa hatua ambazo imeanza kuzichukua kuhakikisha tatizo hili la kukatika kwa umeme katika Mji wa Kahama mara kwa mara linakwisha, lakini pamoja na pongezi hizo nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Kahama unakuwa kwa kasi kubwa na mahitaji ya umeme kwa Wananchi wa Mji wa Kahama na maeneo ya jirani ni makubwa, lakini kila wananchi wanapoomba kupatiwa umeme na hususan wa maeneo ya Majengo, Sokola, Mongolo, Mbulu na kadhalika hawapati majibu sahihi na wala hawaunganishiwi umeme kwa urahisi:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu tatizo hili sugu ambalo limekuwa katika Mji wa Kahama kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tunapokea changamoto aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge lakini niseme tu kwamba kwa sasa hivi hali ilivyo ndani ya Shirika letu la *TANESCO* na hasa kuwahudumia umeme kwa kiwango ambacho ukilinganisha na kiwango kilichokuwa kinafanyika siku za awali au miaka ya nyuma hali inaenda vizuri. Tarehe 9 mwezi wa 10, mimi na baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Shinyanga tulikuwa pale Kakola tulikuwa tunazindua Mradi wa Umeme tuliwaeleza wananchi juhudi ambazo Shirika la *TANESCO* linafanya na kwa kuwa yapo maeneo ambayo na sisi tunapata taarifa wananchi kwa sasa hivi kweli kwa kiasi fulani wanaridhika kwa sababu kasi ya kuwahudumia wananchi hasa kwenye huduma hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, niseme hata baadhi ya Wabunge wako hapa ndani spidi imeongezeka kiasi tunapata taarifa mbalimbali, lakini tunapokea changamoto hiyo kwamba yako mambo ambayo kiutendaji yanahitaji kufanyiwa kazi, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza kwenye swali hili kutoka sehemu yenye dhahabu, Mheshimiwa Mabina, simuoni vizuri ni Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo Kahama yanafanana sana na matatizo yaliyo Geita, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri sasa *MC Challenge* tunaona jitihada zake zinaanza kuonekana, lakini katika bajeti iliyopita tuliona *REA* ingeanza kufanya kazi ili wananchi waendelee kuwa na matumaini katika maeneo ya wachimbaji, anasemaje? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mipango yote inaendelea, utekelezaji wa miradi mbalimbali kama tulivyoahidi, tumekuwa tukiahidi na kutoa taarifa kupitia Bunge lako Tukufu lakini pia kwa wananchi. Utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo imepangwa na Seriakali inaendelea vizuri. *REA* kwa maana ya wakala wa nishati vijijini naye anaendelea na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla, *REA* wako kazini wanaendelea vizuri na nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kama yako maeneo ambayo tulikuwa tuna ahadi nayo kupitia Wakala wa Nishati Vijijini na angependa kujua taarifa tulipofikia basi tuwasiliane naye ili tuendelee kumpa kiwango cha utekelezaji kimefikia hatua gani.

Na. 119

**Kugawa Upya Vitalu vya Madini Vinavyoachwa na Wachimbaji Wadogo**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kutokana na uwezo na teknolojia ndogo ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini wanakosa uwezo wa kuvuna madini hasa ya dhahabu na tanzanite yanayokuwepo kina kirefu ardhini na hivyo kuwepo uwezekano wa madini hayo kuachwa:-

Je, kuna uwezekano na taratibu gani wa kugawa upya maeneo au vitalu vinavyoachwa na wachimbaji wadogowadogo kwa wenye uwezo mkubwa ili kuvuna madini yanayoachwa ardhini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, naomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, leseni za uchimbaji mdogo (*PML*) hutolewa kwa kuzingatia Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Uhai wa *PML* ni miaka mitano (5) na huweza kuhuishwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) kwa matakwa ya mmiliki. Aidha mmiliki anayo haki ya kuiacha (*surrender*) leseni yake kabla ya muda wa leseni kuisha kutokana na sababu atakazozitoa kwa Kamishna wa Madini ambazo zinaweza kuwa za kuichimbaji, uchenjuaji, kiuchumi au hata kijamii.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi kina cha mashimo ya wachimbaji wadogo kikishakuwa kikubwa kufikia mita 50 kwenda chini, matatizo kama zebaki kushindwa kutenganisha dhahabu na madini mengine, mashimo kujaa maji na ukosefu wa hewa ya kutosha husababisha uchimbaji mdogo wa madini husitishwa.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na sababu kuwa uchimbaji wa madini ya dhahabu unaofanywa na wachimbaji wadogo huhusisha tabaka la juu la miamba ambayo imeoza (*weathered*) ambalo kina chake hakizidi mita 50 kutoka usawa wa ardhi. Katika tabaka hili madini kama dhahabu kwa kiasi kikubwa huwa yameachana na madini yanayoambatana nayo kama vile *sulphides* hivyo wachimbaji wadogo hutumia zebaki katika kutengenisha dhahabu na mchango na madini mengine.

Mheshimiwa Spika, kina kinapoongezeka miamba yenye dhahabu huwa haijaoza (*un weathered*) hivyo dhahabu mara nyingi huwa imeambatana na madini mengine kama *sulphides*. Hali hii hufanya zebaki isiweze kutumika katika kutenganisha dhahabu na madini mengine. Kwenye migodi mikubwa *cyanide* hutumika kutenganisha dhahabu na madini mengine.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kwa wachimbaji wadogo ni maji kujaa kwenye mashimo ya uchimbaji katika maeneo yenye maji mengi iwapo wachimbaji watakuwa hawana pampu zenye nguvu kubwa zenye uwezo wa kusukuma maji kuyatoa nje ya mgodi. Vilevile, jinsi kina kinavyoongezeka inawawia vigumu wachimbaji wadogo kuweza kupeleka chini hewa ya kutosha kwa ajili ya watu wanaofanya kazi mgodini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchimbaji mdogo atakayeshindwa kuendelea na shughuli za uchimbaji wa madini kwa sababu zozote zile ikiwemo uwezo mdogo wa kuchimba anayo haki ya kuliachia eneo hilo kwa kumwandikia Kamishna wa Madini kuelezea nia yake ya kusitisha kuchimba na kuliachia eneo la leseni yake. Vilevile, mchimbaji mdogo atakayeshindwa kuendeleza eneo lake kwa kushindwa kutimiza masharti ya leseni yake, leseni yake inaweza kufutwa na Kamishna wa Madini.

Mheshimiwa Spika, endapo leseni itaachiwa na mchimbaji mwenyewe au kufutwa na Kamishna wa Madini kwa maeneo ya wachimbaji wadogo yasiyotengwa kisheria kuwa ya wachimbaji wadogo kulingana na kifungu Na.14 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998, mwombaji mwingine yeyote awe mwekezaji mkubwa au mchimbaji mdogo anaweza kuomba leseni ya madini katika eneo hilo. Iwapo eneo lenye leseni liko katika eneo lililotengwa mahususi kwa ajili ya wachimbaji wadogo eneo litakuwa wazi na mchimbaji mdogo mwingine mwenye sifa anaweza kuomba na kupewa eneo hilo.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu marefu na ya kina. Lakini hata hivyo ninaomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, yalipotokea maafa kule Mererani hivi karibuni wachimbaji wakubwa waliwasaidia sana wachimbaji wale wadogo hasa kwa kutoa vifaa kuwasaidia kuokoa, kwa msingi huo huo wa ushirikiano uliooneshwa:-

Je, Mheshimiwa Waziri haoni ipo haja ya kuimarisha kujenga mahusiano hayo mazuri ili wachimbaji wakubwa waweze vilevile kuwakodishia wachimbaji wadogo vifaa vyao ili waweze kwenda chini zaidi na kupata dhahabu zaidi au madini zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Herbert Mntangi kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba ushirikiano ulioonyeshwa baada ya kutokea tukio la kusikitisha pale Mererani mwanzoni mwa mwaka huu unaendelea kuimarishwa, tumekuwa tukifanya hivyo na mwezi wa saba ninaamini Waheshimiwa Wabunge wengi walifuatilia na wananchi, mimi nilizindua pale *program* moja inayoendeshwa na Kampuni ya *Barrick* kule Nyamongo, *North* Mara kule Wilaya ya Tarime *program* ambayo inahusisha mwekezaji mkubwa lakini anashirikiana na wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, ninaamini Waheshimiwa Wabunge wameshafika maeneo hayo na wameona lakini pia Kampuni ya *Barrick* inaendelea na mashirikiano katika maeneo ya Kahama na wachimbaji wadogo, pale Mwadui Shinyanga mwendeshaji wa mgodi ule *De Beers* kuna mradi maalum ambao unaendelea kushirikiana na wananchi wa maeneo ambayo wanazunguka mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumesema kwenye Bajeti yetu kwamba katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanzisha mfuko maalum ambao utasaidia wachimbaji wadogo kwa maana ya *revolving fund* mfuko ambao tunaamini tunasaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo itakayowasaidia kuimarisha mitaji yao lakini pia kupata vifaa ambavyo vitavyowasaidia katika kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Swali fupi la nyongeza Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, kwa sababu imetajwa Mererani.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati ya Jaji Mark Bomani ilithibitisha kwamba uchimbaji endelelevu sharti lake muhimu na haswa kwa wachimbaji wa madini ya vito ni vizuri ukafanywa na wazalendo na hasa wachimbaji wadogo na kwa kuwa uwezo wa wachimbaji wadogo wakati mwingine unahitaji kupewa msaada ili waweze kuongezewa nguvu ya kuendelea na uchimbaji kwa njia nzuri zaidi:-

Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kutenga fedha za kuwaunga mkono wachimbaji wadogo ili uchimbaji huo endelevu uweze kuendelea kwa faida ya wachimbaji wadogo na kwa faida ya Taifa letu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia masuala ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie nafasi hii ili kuliaribu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Maendeleo katika Sekta ya Madini yanahitaji nguvu ya pamoja na haitakuwa rahisi kuendeleza Sekta ya Madini na Taifa kunufaika kwa kiwango kikubwa kwa kutegemea uegemeo wa upande mmoja tu kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo kama nilivyokwisha kusema kwamba Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi wa ndani na nje ya nchi na Serikali pia imetenga fedha kwenye mwaka huu wa fedha ili tuwe na mfuko ambao hatimaye tunaamini kwamba utawasaidia sana wachimbaji wadogo wakiwemo kwa kweli wachimbaji wadogo wa Mererani.

Lakini natoa wito pia kwa wafanyabiashara wetu tuendelee kushirikiana na wachimbaji wadogo kwa sababu wachimbaji wadogo wameajiriwa na wanashiriki katika shughuli hii kwa sababu wameajiriwa na wale ambao wana leseni katika maeneo husika. Ni rai yetu sisi kama Serikali kuwaomba waendelee kushirikiana na wachimbaji wadogo kuimarisha manufaa ya wachimbaji wadogo lakini kwa taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ukomo wa kipindi cha maswali umefika lakini nadhani ni utaratibu mzuri tu tuyamalize haya mawili ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufindi, kwa hiyo Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally kwa swali linalofuata.

Na. 120

**Shule za Sekondari za Kata**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na mvutano usio wa lazima kati ya Serikali Kuu na TAMISEMI juu ya Shule za Sekondari za Kata:-

(a) Je, shule hizo ziko Halmashauri au Serikali Kuu?
(b) Je, kwa nini Idara ya Ukaguzi isiwe Halmashauri ili kurahisisha kazi za Ukaguzi?

**SPIKA:** Majibu, hatimaye Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa wakati muafaka:-

(a)Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari za Kata hujengwa kwa nguvu za wananchi wakishirikiana na Serikali. Katika ujenzi wa shule hizo yapo majukumu ya msingi ya wananchi na yale ya Serikali Kuu. Mchakato unafanywa sasa kuhamishia umiliki wa shule zote za Sekondari za Serikali kwenye Halmashauri za Wilaya. Baada ya ujenzi kukamilika, umiliki wa shule hizo ulikuwa chini ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Jukumu la Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia mabadiliko ya sasa, ni kusimamia na kuendesha shule ambapo Serikali Kuu inasimamia sera, sheria, kanuni, utoaji wa miongozo ya usimamizi na uendeshaji wa shule. Aidha, Serikali Kuu inasimamia masuala ya mitaala na ubora wa elimu pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya elimu kwa ujumla.

(b)Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi wa Shule iliundwa kwa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kifungu 40 – 43 na rekebisho Na. 10 la mwaka 1995 Vifungu 31 – 32. Sheria inaelezea jukumu la idara hiyo ni kufuatilia uzingatiaji wa sheria, kanuni na viwango vya utoaji wa Elimu.

Idara hii inatenda kazi zake hadi katika ngazi ya Wilaya. Ili kurahisisha na kuleta ufanisi zaidi katika kazi ya ukaguzi wa shule Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeunda kanda mpya 3 za ukaguzi wa shule na hivyo kuwa na kanda 11 badala ya 8 zilizokuwepo. Hii itasaidia kupunguza ukubwa wa kanda na kuleta ufanisi wa kazi ya ukaguzi wa shule. Kanda hizo ni:-

1. Kaskazini Magharibi (Mikoa ya Arusha na Manyara);

2. Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga);

3. Kati (Mikoa ya Dodoma na Singida);

4. Ziwa Magharibi (Mikoa ya Kagera na Kigoma);

5. Ziwa Mashariki (Mikoa ya Mwanza na Mara);

6. Magharibi (Mikoa ya Tabora na Shinyanga);

7. Mashariki (Mkoa wa Dar es Salaam peke yake);

8. Nyanda za Juu (Mikoa ya Mbeya na Rukwa);

9. Nyanda za Juu Kusini (Mikoa ya Iringa na Ruvuma);

10. Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi); na

11. Pwani (Mikoa ya Morogoro na Pwani).

Mheshimiwa Spika, ripoti za ukaguzi wa shule hutumwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na nakala hutumwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Afisa Tawala wa Mkoa, Mwenyekiti wa Bodi ya Shule na Mkuu wa Shule.

Aidha, kwa shule za binafsi ripoti hutumwa pia kwa Meneja wa Shule na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule. Halmashauri na wadau wake hupewa ripoti hizo kwa lengo la kupata taarifa kamili za shule ili kuimarisha uendeshaji na usimamizi wa shule pamoja na utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na Wakaguzi wa Shule.

Mheshimiwa Spika, ahsante! (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na nia njema kabisa ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata elimu ya Sekondari kwa kiwango kikubwa kadri inavyowezekana lakini kwa kuwa nia hiyo bado inakabiliwa na matatizo makubwa hasa katika sekta hiyo ya Elimu ya Sekondari kwani shule hizo bado zinahudumiwa na shule mlezi katika kupata ruzuku kitu ambacho kimekuwa kero kubwa kubwa na fedha za kuhudumia fedha shule hizo zimekuwa zimekuwa zikichelewa sana na kufika wakati ambao sio muafaka. Lakini vilevile Walimu wanaohudumia shule hizo bado wanahudumiwa na Serikali Kuu kwa hiyo mafao yao yamekuwa yakichelewa, mishahara yao imekuwa ni kero kubwa.

Sasa mimi nimwulize Mheshimiwa Waziri, matatizo hayo ndiyo yatakayosababisha mchakato huo wa kuzipeleka shule hizo kwenye Halmashauri kuchelewa, je, haoni ni wakati muafaka sasa Serikali kufanya maamuzi ya dhati ya kumaliza kero hizo ili shule hizo ziweze kuwa na hadhi inayotakiwa katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Jenista J. Mhagama la nyongeza kama ifuatavyo:-

Awali ya yote, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ya kipekee wanavyoguswa na changamoto katika Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Pili, naomba kutamka rasmi kwamba suala la kuwa na shule mlezi tulishalifuta mwaka 2006 na kwamba hivi sasa shule zote hujitegemea zenyewe hata kama ndivyo zimeanza. Mchakato huu ulibadilishwa na kupeleka majukumu makubwa kwa Halmashauri zenyewe pamoja na Mikoa. Kwa hiyo, fedha inapopelekwa Hazina ndogo tayari inakuwa imeshaelekezwa iende shule gani na kwa kazi gani.

Hivyo, natoa wito kwa Walimu Wakuu au Wakuu wa Shule wote kufanya kazi kwa juhudi na kuwa wafuatiliaji ili pale panapokuwa na fursa mbalimbali walizopelekewa waweze kuzitumia kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Spika, la pili, tumetatua madaraka ya shule hizi na Wizara yangu pamoja na TAMISEMI tupo katika hatua za mwisho kabisa na ninaamini mara baada ya Bunge hili tunaweza tukafanya makabidhiano. Lengo ni kuhakikisha kwamba shule hizi sasa zinakuwa karibu zaidi na Watendaji Wakuu na Walimu waweze kupata huduma zao za msingi na hii tunaamini itatusaidia kupunguza kero za Walimu kwa kadri itakavyowezekana. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jawabu lake katika swali mama lililopita.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza, umma wa Watanzania pamoja Bunge lako Tukufu limeshuhudia jinsi wananchi wa Tanzania walivyotumia nguvu zao nyingi katika kujenga shule mbalimbali katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kujenga shule peke yake hakutoshi, tatizo linalofuata hivi sasa ni wanafunzi wetu kukaa chini kwa sababu hawana madawati:-

Je, Mheshimiwa Waziri amejipangaje pamoja na Serikali kuweza kuweka madawati katika shule ambazo zimejengwa hivi sasa ili kwenda sanjari na kazi na nguvu nyingi zilizotolewa na na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kupata elimu ili watoto wetu wasiote vibyongo kwa kukaa chini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda nirudie tena kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote kwa kushirikiana katika kuzijenga hizi shule, ni zetu na kwamba tunashirikiana katika utekelezaji na kuwekeza miundombinu mingi. Serikali kwa wakati wake kwa kadri inavyojaliwa kwa kushirikiana na Halmashauri hupeleka fedha kwa ajili ya upatikanaji wa madawati.

Naomba nitoe wito, kila Halmashauri kwa sababu na Mbunge ni sehemu ya Madiwani, naomba wanapokaa katika mipango yao ya bajeti watenge fedha kwa ajili ya madawati, inawezekana. Zipo Wilaya ambazo zimefanya hivyo na ipo Mikoa ambayo imefanikisha ni kweli inakera wanafunzi kuketi chini.

Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi imekuwa ikitoa fedha kwa shule za Sekondari na kwa kushirikiana na wadau ili kuweza kupata madawati. Naomba fedha zinazotengwa kwa ajili ya madawati zitumike kwa ajili ya madawati na niwasihi Waheshimiwa Wabunge ingieni kwenye vikao vya Halmashauri muweze kusukuma na kuhimiza maamuzi yatakayoleta tija kwenye sekta ya elimu. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Narudi kwenye swali la msingi, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana hapa kwamba mpango wa Serikali ni kuzipeleka Sekondari zote za Kata kwenye Halmashauri za Wilaya husika, jambo ambalo ni jema na kwa hiyo Shule za Msingi na Sekondari zote zitakuwa kwenye Halmashauri husika.

Lakini Idara hii ya Ukaguzi Wilaya yaani Ukaguzi wa Elimu yenyewe iko Serikali Kuu japo ipo Wilayani, ni kwa nini basi Serikali isikubaliane umuhimu wa Idara ya Ukaguzi nayo kuwa chini ya Halmashauri ili kuboresha Elimu ya Msingi na Sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikiri kwamba tumegawana madaraka, tumewamegea sehemu na hii ni kutaka kupata ile *check and balance*, nasikitika nimetumia lugha ya kigeni, kwamba tukibaki na nafasi zote peke yetu tutashindwa kujipima na tukiwapelekea wenzetu sehemu yote watashindwa kujipima.

Mheshimiwa Spika, naogopa tusije tukageuka kama yule mcheza dansi wa Kizaire anayeitwa Loketo. Sasa naomba tubakie na hili kwa sababu kwenye sera itabaki Wizara ya Elimu na Mafunzo na kwamba kwa sehemu kubwa itabakia kwenye Halmashauri ambapo Watendaji hawa wakaguzi ndipo walipo. Kwa pamoja tutashirikiana, naomba wote tuwe na dhamira njema tutashinda.

**SPIKA:** Maelezo ya ziada Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niongezee kidogo kwenye majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, Shule za Sekondari zinahamishiwa katika Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Manispaa na Majiji.

Katika sehemu hizo, Halmashauri zitakuwa na kazi ya kusimamia uendeshaji wa shule na Wizara itasimamia Sera, ubora wa elimu na upimaji wa elimu na katika upimaji na utekelezaji wa mitaala Idara ya Ukaguzi ni msingi sana katika kazi hizo, tutaendelea kuwapa ushirikiano wa karibu sana Halmashauri pamoja na Idara hizi za Ukaguzi ili kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa bora iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

Na. 121

**Idadi ya Wanafunzi Waliofaulu na Kwenda Sekondari**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa mstari wa mbeke kuzisifia Wilaya zilizofanikiwa kuwapeleka wanafunzi waliofaulu Mitihani ya Darasa la Saba kwenda Sekondari bila kujali asilimia ya waliofaulu na wasiofaulu; na kwa kuwa, hali hiyo husababisha Wilaya zilizofaulu kwa asilimia ndogo kuweza kuwapeleka wanafunzi wote na kuwaacha wengi walioshindwa:-

Je, Serikali haioni kuwa, utaratibu huo haufai kwa kuwa, utasababisha Wilaya zingine pia zihakikishe wanafunzi wengi wanashindwa ili nazo zipate sifa ya kupeleka wanafunzi wote Sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Watahiniwa wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba hufanya masomo matano nayo ni Kiingereza, Kiswahili, Sayansi, Maarifa ya Jamii na Hisabati. Kila somo lina jumla ya alama hamsini (50). Hivyo kiwango cha juu cha kufaulu katika Mtihani wa Darasa la Saba ni jumla ya alama 250. Aidha, kiwango cha chini cha ufaulu kwa watahiniwa wa Darasa la Saba nchini ni alama 100. Sera yetu ni kuwa wanafunzi waliofaulu na kufikia alama 100 au zaidi ndio wanaendelea na masomo ngazi ya sekondari. Idadi ya wanafunzi wanaofaulu na kuchaguliwa hutegemea nafasi zilizopo katika kila Wilaya husika. Wilaya zenye shule nyingi za sekondari hupeleka asilimia kubwa ya wanafunzi hao Kidato ha Kwanza na zile zenye shule chache hupeleka wanafunzi wachache. Serikali inazihimiza Wilaya kuwa kila Kata iwe na angalau shule

moja ya sekondari na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaofaulu wanapata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wa kutoa takwimu zinazoonesha hali ya ufaulu Kitaifa, Mkoa, Wilaya na kila Shule. Hivyo Wilaya zinazofanya vizuri vinastahili pongezi na zile zinazofanya vibaya pia hubainishwa ili ziweke mikakati ya kuboresha ufaulu. Idadi ya wale wanaoendelea huoneshwa ili Wilaya ziongeze kasi ya ujenzi wa shule za sekondari na kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wanaofaulu kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni mzuri kwani umekuwa chachu ya mashindano kati ya Wilaya na Wilaya na hata Mkoa kwa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, wananchi wa Geita wameitikia wito wa Serikali wa kujenga shule nyingi sana za Sekondari ikilinganishwa na wakati tunaingia madarakani mimi Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba na Mheshimiwa James Philipo Musalika Geita ilikuwa na Shule za Sekondari 9 tu lakini leo hii Geita ina shule 44.

Katika shule hizo mpaka sasa hivi kuna matatizo ya kutokuwa na Walimu pamoja na vitabu vya ziada na kiada na kupelekea wanafunzi kutokuwa na elimu sahihi au kwenda pale kama kucheza tu:-

Je, Serikali inaonaje kuiwekea mkakati Wilaya ya Geita kuweza kupeleka Walimu na vitabu katika shule hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita kama ifuatavyo:-

Awali nawapongeza kwa kujenga shule nyingi za sekondari na pili naomba nimueleze kwamba Serikali imeweka mkakati wa muda mfupi, wa kati na mrefu wa namna ya kupata Walimu na kila mwaka huwa tunasambaza Walimu. Tatizo lililopo ni kwamba Walimu wengi wanapokwenda kwenye maeneo husika ama wanakuta mazingira yasiyowaridhisha au wanakuta matatizo fulanifulani ambayo huwafanya warudi.

Lakini naomba niseme kwamba mwaka huu peke yake Mkoa wa Mwanza umepelekewa zaidi ya Walimu 300 na ninaomba wafuatilie kwa Afisa Elimu kuona namna ya kuwadhibiti Walimu hao.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Magale Shibuda, yeye alifika Wizarani akatafuta orodha ya Walimu waliopangiwa kwenda Shinyanga akafanya nao mkutano na wengine aliwapa nauli yeye mwenyewe ili waweze kwenda kwenye Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, pia suala la kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia Wizara yangu kila mwaka hutenga fedha kwa kadri bajeti ilivyoturuhusu kwa kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nikiri kwako kwamba gharama za vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni kubwa hivyo nitoe rai kwa wazazi baada ya kuwalipa wanafunzi wao au watoto wao ile ada ya shilingi 20,000/= wawe tayari pia kuwanunulia pia vitabu vya kiada ambavyo vinaweza kusaidia katika maendeleo yao. Sisi kama Serikali tutaendelea kutoa fedha kwa ajili ya vifaa vya kufundishia kwa kadri bajeti itakavyoturuhusu.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la mwisho.

Mheshimiwa Spika, shule hizi pamoja na kukosa Walimu, vitabu na kukosa vitabu vya kiada bado shule hizi hazina maabara na vifaa vya maabara:-

Je, ni lini Serikali itaweka mikakati maalum ya kujenga maabara na kuacha huu mpango wa kusema Bajeti haitoshi?

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji mkubwa wa maabara. Hivi sasa tunao mpango maalum wa upatikanaji wa maabara kwa kila shule ya Kata ambao tunautafutia fedha na utekelezaji wake utaonyeshwa kwenye mwaka wa fedha wa 2009/2010. Kwa hivi sasa, Mheshimiwa Mbunge aingie katika vikao vitakavyokuwa vinapanga ni shule zipi zitakazopatiwa Maabara. Kila Mkoa utapata Maabara 10 hivyo Mkoa unayo hiari kufuata mapendekezo wapi ziende na hivyo ndivyo bajeti yetu inavyoturuhusu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Waheshimiwa Mawaziri wote na Naibu Mawaziri kwa Majibu yenu na Waheshimiwa Wabunge kwa maswali yenu, hicho ndiyo kimekuwa kipindi cha maswali na majibu katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu.

Matangazo, wageni ni kama ifuatavyo, kwanza, wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, waliopo pale katika jukwaa la Spika ni Mama Bertha Kaitila ambaye ni Dada yake na Mheshimiwa Waziri Mkuu, amefuatana na Mumewe Bwana Sadiq Kaitila. Karibuni sana. Nimefahamishwa kwamba mmetoka moja kwa moja Mpanda ni mbali kidogo

natumaini mmekuwa na safari isiyokuwa na usumbufu, tunafurahi kuwaona hapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wengine ni 15 wa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mbunge wa Uzini, Waziri wetu wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), wao ni Viongozi wa CCM Jimbo la Uzini Zanzibar. Naomba wasimame tafadhali! Karibuni sana ndugu zetu kutoka Zanzibar kila mara tunafurahi kuwaona hapa Dodoma na tunawatakia mema katika shughuli zenu. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa James Daudi Lembeli wa Kahama ni Mheshimiwa Daudi Leo Mabala ambaye ni Diwani wa Kata ya Bulungwa kule Kahama. Ahsante sana Mheshimiwa Diwani na karibu sana. Pia na Bwana Deus Sane ambaye ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Bulungwa, karibuni sana. Tunawaomba muendelee kuhimiza kilimo cha pamba ili nchi yetu izidi kupaa katika uchumi. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Luhaga J.Mpina, ni Ndugu Sayu Mwigulu ambaye ni Katibu wa Siasa na Uenezi CCM Kata ya Lubiga, karibu sana.

Ndugu Nzunzu Ndaturu, Mwenyekiti wa Kijiji cha Longalaniga kutoka Jimbo hilohilo la Kisesa. Karibuni sana Waheshimiwa, nashukuru sana kuwaona. (*Makofi*)

Wapo pia wanafunzi 31 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma wanaendelea na ziara yao hapa Bungeni, ninaomba wasimame tuweze kuwatambua, karibuni sana wasomi wetu.Sisi Wabunge wenu tunawatakia mafanikio katika masomo na kwamba mzingatie masomo kwa sababu nchi yetu inawahitaji sana. (*Makofi*)

Matangazo ya Kazi, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii saa 5.00 asubuhi mara baada ya matangazo katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, ameniomba nitangaze kwamba saa 5.00 asubuhi leo kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Viwanda na Biashara katika Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ameniomba nitangaze kwamba saa 5.00 kutakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 227, kikao cha Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Nishati na Madini mkutane leo saa 7.00 mchana au mara baada ya kuahirishwa Bunge katika ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Anne S. Makinda, Naibu Spika na Mwenyekiti wa *TWPG,* Wabunge Wanawake wa Bunge la Jamhuri, ameomba Wabunge wote Wanawake mkutane leo tarehe 7 Novemba, Saa 7.00 mchana ama mara baada ya kuahirisha mkutano huu wa Bunge katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, ile semina ya Viongozi kuhusu Kanuni za Bunge ambayo inawahusu Wajumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge, Wenyeviti na Makamu Wenyeviti pamoja na Waheshimiwa Mawiziri ambao watakuwa na muda, ilikuwa ifanyike kesho hapa Dodoma, kwa sababu mbalimbali imeonekana ni vema ifanyike jumanne tarehe 11/11 katika Ofisi Ndogo ya Dar es Salaam saa 3.00 asubuhi. Semina hii itafanyika kama ilivyopangwa kwa ratiba ambayo mmegawiwa, imeonekana ni vema tufanye hivyo.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo, naomba sasa Katibu atuelekeze katika hatua inayofuata. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Kanuni ipi?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Kanuni ya 68

**SPIKA:** Endelea!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nimeona nisimame kuomba mwongozo wako kutokana na maandishi yaliyoandikwa na gazeti la Serikali la Habari Leo, Toleo Namba 686, la tarehe 5 Novemba, 2008 lililoandika habari zilizolenga kuleta mtafaruku na uchochezi kati ya Bunge lako Tukufu na Serikali ya Chama Tawala Serikali yetu ya CCM, iliyoandika habari zilizopewa kichwa cha habari kwamba:-

*“Kundi la Wabunge wa CCM lasuka zenge la EPA kuwasilisha hoja kupinga uamuzi wa Kikwete leo Dodoma yadaiwa wanachochewa na viongozi wa ndani na nje ya Bunge”.*

Mheshimiwa Spika, gazeti hili limeandika kwamba kuna njama za Wabunge wa Bunge lako Tukufu za kupinga Serikali ya Rais Kikwete na zaidi imeelekeza kwamba ni Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, kitendo ambacho kimeelezewa kwamba Wabunge wa Bunge hili wanatumiwa na watu walioko nje ya Bunge hili na hasa inaendelea kuonyesha kwamba haturidhiki na hatua anazochukua Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika suala zima la kupambana na suala la *EPA* na hasa hatua zinazochukuliwa hata baada ya kwamba Rais wetu amefanya kazi nzuri na kwamba sisi Wabunge wa CCM tunamuunga mkono kwa asilimia mia moja. Lakini gazeti letu hilihili la Serikali limeendelea kujenga hoja katika gezeti hilo la toleo hilo kwamba …

Mheshimiwa Spika, labda nilisome kwa ruhusa yako kama utaniruhusu ili muendelee kuwa na uzito wa …

**SPIKA:** Kwa kifupi tu maana kwa sasa unatafuta Mwongozo wa Spika usiwe na hotuba.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, mandhari gazeti hili limeelekea kujenga uchochezi kati ya Serikali na Bunge na kati ya Wabunge na Rais, ambaye sisi tunamheshimu na kutambua na kuthamini kazi yake, naomba mwongozo wako.

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali imechukua hatua za kulifungia gazeti moja kwa ajili ya habari hizo hizo zilizodaiwa ni za uchochezi; na kwa kuwa habari hizi ni nzito zaidi kuliko hizo zilizokuwa zimeandikwa kwenye Gazeti la Mwanahalisi; na kwa kuwa habari hizi zimetolewa na Gazeti la Serikali yetu; naomba Mwongozo wako juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa gazeti hili, ili kulinda heshima ya Bunge lako na kulinda heshima ya Serikali yetu na ya Chama Tawala. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hata mimi nilishtuka sana niliposoma taarifa hiyo katika gazeti husika na ni mchezo ambao ni wa hatari sana na ungetegemea mchezo kama huu uendelezwe labda na vijigazeti vya ovyo ovyo tu. Linapokuwa gazeti tena la Serikali, linajitahidi kuchonganisha Wabunge na Serikali yao na kwa idadi Wabunge wengi ni wa CCM, wanachonganishwa na Serikali ambayo ni ya CCM, hili ni jambo zito sana.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba, wahusika wote; Waheshimiwa Wabunge waliotajwa, waandike malalamiko rasmi. Serikali kwa sasa hivi imesikia, lakini waandike kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari na tutafuatilia sasa hatua gani zitakuwa zimechukuliwa baada ya malalamiko hayo kupokelewa rasmi Serikalini.

Nadhani Katibu tunaweza kufanya utaratibu ambao tutapeleka nakala ya gazeti hilo kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari, kama msimamizi wa eneo hilo. Lalamiko hilo litakuwa limechukuliwa rasmi kutokana na *Hansard* ambayo ni mazungumzo tuliyonayo hapa leo. Tunategemea kwa kweli Serikali ichukue hatua na sio kukaa kimya.

Mheshimiwa Waziri, naona ana ufafanuzi sasa hivi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuungana na mtoa hoja kwamba ni kweli Gazeti la Serikali la Habari Leo, juzi liliweka kichwa cha habari ambacho sisi wengi kilitushtusha. Wizara yangu imekwishachukua hatua, wanaohusika wametakiwa wajieleze ukweli au usahihi wa habari walizoandika, baada ya kupata majibu yao Serikali itachukua hatua kwa jinsi itakavyoona inafaa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Nadhani kwa usahihi zaidi na kwa kuwa hatuwezi kusubiri Mkutano wa Kumi na Nne, ambao utaanza nadhani utakuwa mwaka kesho Januari pengine; ni vizuri jambo hili liweze kufikishwa Ofisi ya Spika. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali mara itakapokuwa imefanya utafiti wake, inifikishie pale ofisini ili na mimi niweze kuishirikisha Kamati ya Maadili. Ahsante sana. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

## A Z I M I O

### Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana wakati Naibu Spika akiahirisha shughuli za jana, kulikuwa na wenzetu sita walioomba kuchangia. Sasa najaribu kufanya jitihada, tuweze kumaliza kikao chetu cha leo saa 7.00 mchana. Hoja zilizopo, nina wasiwasi watakuwa warudia rudia tu kwa sababu ni hoja mbili tu, kwamba ama tuongeze mipaka ya hiyo Mbuga ya Wanyama au tuahirishe hatua hiyo.

Kwa hiyo, nitawasihi sana hawa nitakaowataja Mheshimiwa Ndugai, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Kaika Telele. Kwanza, kama baadhi yao wanaweza kujitoa ili tusiendelee tu kupigia kelele jambo lililowazi kabisa, itakuwa vyema. Kama hawatajitoa, nitaangalia muda na hususan nikiona wanarudia rudia, chini ya Kanuni zetu za Bunge basi nitasitisha tu maana yake itakuwa hakuna faida kuendelea kusikiliza watu wanaungana mkono upande ule na ule. Kwa tahadhari hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Job Ndugai, ajiandae Mheshimiwa Prof. Mwalyosi.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, niwe mchangiaji wa kwanza asubuhi ya leo, kuhusiana na Azimio la Bunge la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa kuleta Azimio hili. Vile vile niwapongeze *TANAPA*, Shirika letu ambalo tumelikabidhi jukumu la kusimamia na kuendesha Hifadhi za Taifa, kazi ambayo wanaifanya vizuri sana chini ya Bodi yao na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hili Ndugu Bigurube.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, kwanza, nitoe salamu za rambirambi kwa askari wa *TANAPA*, ambaye pia alikuwa ni dereva, aliyeuawa wiki iliyopita kwa kukatwakatwa na mapanga kwenye Hifadhi ya Taifa ya Kitulo. Jambo hili linasikitisha, tungeliomba sana mambo kama haya yasiendelee kutokea na Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu huyu mahali pema peponi. *Amin.*

Nawapa pole Wahifadhi wote Tanzania, kwa kazi ngumu wanayoifanya kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Azimio lililo mbele yetu, linatutaka turidhie kwa kuunga mkono Upanuzi wa Hifadhi ya Ziwa Manyara. Ninaanza kwa kusema, naunga mkono hoja hii. Ninaunga mkono kwa sababu gani? Hifadhi ya Manyara ni hifadhi ambayo ina umuhimu wa kipekee na inatambulika duniani. Hifadhi hii ni ndogo sana kuliko hifadhi zote zilizoko hivi sasa katika himaya ya Hifadhi za Taifa za Shirika letu; hifadhi kama 15, hii ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi hii upande mmoja kuna Ziwa Manyara na kutoka Ziwa Manyara kuna gema la bonde la ufa. Kwa hiyo, wakati wa masika mvua ikinyesha na Ziwa lile kupanuka, sehemu ya malisho ya wanyama ni ndogo sana, kwa sababu huku ni Ziwa na huku ni gema la mlima mkali. Kwa kuwa sehemu yake ni ndogo sana, wanyama wengi sana wamepotea.

Tumeambiwa hapa faru hayupo tena, nsia hayupo tena, palikuwa na pofu pale hakuna tena, tulikuwa na duma pale hakuna duma hata mmoja. Mwaka juzi wamekufa *Flamingo* kwa maelfu pale. Kwa wale waliosoma masuala ya uhifadhi ya Ireland *bi-geography* ni hifadhi ambayo sio *sustainable*, huwezi ukawa na hifadhi ndogo kama *Manyara National Park* halafu ukategemea iwepo miaka 100 ijayo, haiwezekani. Lazima hifadhi ile kwa udogo wake na jinsi ilivyo na ilivyobanwa, itakufa ikiachwa vile ilivyo. Eneo hili ni muhimu sana, ndiyo maana hatuna namna ni lazima Hifadhi ya Manyara ipanuliwe na zoezi hili tuliambiwa miaka ya 1970, halikuanza juzi kama tulivyokuwa tunaambiwa hapa, limeanza zamani. Ndiyo maana katika mawasilisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri ameeleza yafuatayo:-

Kwamba, kinachoombwa kiongezeke hapa ni Msitu wa Marang wenye kilomita za mraba 230, Mashamba Namba 1, 2 na 3, majimoto yenye kilomita za mraba 38, sehemu ya Ziwa Manyara yenye kilomita za mraba 42 na ufukwe wa Ziwa Manyara wenye kilomita 7; ni maeneo manne tofauti.

Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, katika zoezi hili unagusa Wilaya ya Babati Vijijini, ambapo Mheshimiwa Nakei, unagusa Wilaya ya Mbulu ambayo Mheshimiwa Marmo ni Mbunge wake, unagusa Wilaya ya Karatu kule kwa Mheshimiwa Dr. Slaa na kwa sehemu ndogo unagusa Wilaya ya Monduli kwa Mheshimiwa Lowassa. Kwa hiyo, isijengeke picha kwamba, hapa kinachoongezeka katika upanuzi huu wa Ziwa Manyara ni kuwaonea watu wa kona fulani peke yao, hapana, upanuzi unagusa karibu Wilaya nne. Sasa upanuzi wenyewe unahusu nini, tuanze kwanza na Msitu wa Marang; nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ipo katika kitabu ambacho tumepewa na Mheshimiwa Waziri humu ndani.

Ukurasa wa tatu pale, Msitu wa Hifadhi ya Marang ulitangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Serikali Kuu, kupitia tangazo la Serikali Na. 89 la mwaka 1938. Tayari hivi sasa hiyo ni *Forest Reserve. Forest Reserve* ipo chini ya Idara ya Misitu ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ambayo Waziri wake ndio ametuomba kwa mamlaka ya Bunge,

tuhamishe *status* ya hifadhi ile ya Misitu sasa ihamie kuwa kwenye Hifadhi za Taifa chini ya TANAPA; jambo hili halina mgogoro.

Pili, Shamba Namba 1 Majimoto na imepitishwa karatasi moja ndogo, ambayo ina ramani nyuma yake inayoonyesha mashamba haya vizuri sana. Shamba Na. 1 Majimoto ndio lile la kwanza upande wa kulia; 1, 2, 3 ni mashamba ya *TANAPA*. Shamba hili lilikuwa linamilikiwa na Bwana Baker, ambaye baada ya kushindwa kuliendeleza alilirudisha Serikalini mwaka 1974. Serikali ilitoa miliki ya shamba hili kwa Shirika la Hifadhi la Taifa *(TANAPA)*, kupitia Ajenda Na. 2 ya tarehe 23 Julai, 1974 ya *DDC* ya Wilaya ya Hanang kwa wakati huo. Sisi kama Kamati ya Maliasili na Utalii, tumeona mihtasari yote hiyo na barua zote zilizotoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ya kukabidhi shamba hilo kwa *TANAPA* mwaka 1974.

Mashamba Namba 2 na 3, hayana mgogoro wowote ule kwa sababu yalikuwa yanamilikiwa na Bwana Vasta Sisodya na yalinunuliwa na *TANAPA* mwaka 1990 kwa hatimiliki namba 16299 na 354, tayari *TANAPA* wanazo. Hayo ndiyo maeneo makubwa manne ambayo yanaongezwa.

Kwa hiyo, ilipokuja rai hii katika Kamati, Wizara inahamisha maeneo ambayo yapo chini ya miliki yake katika upanuzi wa eneo hili la Ziwa Manyara. Kamati haikuona sababu ya kuzuia jambo hilo. Kwa jinsi hiyo, Kamati ilikwenda Arusha, lilikuwepo swali hapa kwa nini Kamati haikwenda kwenye vijiji jirani. Kamati ilikwenda Arusha, kwa sababu tulikuwa na Muswada Mpya wa Sheria Mpya ya Wanyamapori, ambao ulikuwa uingie katika Bunge la safari hii. Kama unavyojua, Muswada huo umesogezwa uingie Januari/Februari.

Kwa hiyo, tulikwenda Arusha, pamoja na mambo mengine kusikiliza wadau kuhusiana na Muswada wa Sheria hiyo ya Wanyamapori ya 2008. Tulifanya *Public Hearing* kwenye Ukumbi wa *AICC* pale Arusha, baada ya kumaliza shughuli iliyotupeleka kule Kamati ilitembelea Ngorongoro na *Lake Manyara National Park*. Hapakuwa na suala lolote kwa wakati huo, linalohusiana na ubishi wowote kuhusiana na zoezi hili. Kwa hiyo, ziara ya Kamati ilikuwa ni ya kawaida kutembelea maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, tulipokuja hapa Jumatatu wiki hii, ndipo tulipopata maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati, kuhusu upanuzi wa zoezi hili na tukawa tumewakaribisha Wabunge ambao ni majirani. Ndipo mambo haya yalipoanza ya kusema kwa nini hivi, kwa nini vile. Ushauri wetu kwanza kuhusu Shamba la Prince Bernard, mtaliona katika ramani lenyewe lipo nje kabisa, Prince Bernard ni nani? Prince Bernard alikuwa kiongozi nadhani wa Netherlands, Uholanzi, ni Mhifadhi wa Kimataifa aliyetoa maisha yake kwa muda mrefu kusaidia hifadhi na alikuwa ni Rais wa *World Wildlife Fund for Nature* Duniani *(WWF)*.

Aliipenda sana Tanzania, akatoa shamba hili ambalo alikuwa na miliki yake ili liwe sehemu ya hifadhi ya *TANAPA*, liko nje kabisa pembeni. Itakuwa ni jambo la ajabu

kama Serikali italirudisha shamba hilo kwa kulinunua kwa namna moja au nyingine, lakini ikawapa wanavijiji kulima mashamba itakuwa tunakwenda kinyume na ile *will*. Kumbukeni kwamba, hili shamba lipo katika ile hati sijui wanaiita nini, tamko la mwisho la mtu kabla hajafa anasema katika mali yangu jambo gani lifanyike vipi; wosia wake. Ahsante sana.

Katika wosia wa Prince Bernard, amesema kwamba, kipande kile kiende kwa *TANAPA* kwa ajili ya uhifadhi. Ninachoweza kuunga mkono ni kama shamba hilo litarudishwa, lakini litakuwa ni sehemu ya hifadhi ya wanavijiji katika sehemu ya mapito, ambapo kama zitawekwa hoteli au jambo Fulani, mapato na faida itakwenda kwa wanakijiji. Nia ya hifadhi ya Prince Bernard aliyetoa shamba lile kwa uhifadhi, ibakie pale pale.

Mheshimiwa Spika, mwisho, faida za Manyara *National Park* ni kubwa sana. Bajeti ya mwaka huu peke yake, wametoa zaidi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya vijiji jirani. Tunaujua wote Mji wa Mto wa Mbu pale unavyochemka kiutalii, fedha zilivyo nyingi kwa ajili ya *Lake Manyara National Park*. Mji wa Karatu unaokwenda haraka sana, kwa sababu ya utalii. Hili eneo la kusini linalopangiwa mpango ni kwamba, Bunge likiridhia Azimio hili la Kupanua, litawekwa geti kule Kusini mwa hifadhi, watalii watakaotoka Tarangire kupitia Babati au sehemu za Minjingu kule, watapita kule Kusini kutakuwa na geti jipya. Kwa hiyo, sehemu zile za Magala, Majimoto na Moyomayoka zitakuwa zimechangamka sana kiutalii. Hali ya wananchi kiuchumi itaboreka sana, jambo hili ni bora kwao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namalizia kwa kusema kwamba, naunga mkono jambo hili, lakini nakuomba kwa sababu ya kuweka mambo sawa na kuwaelimisha wananchi na viongozi; Kamati ya Maliasili na Utalii chini ya maelekezo yako, itakuwa tayari baada ya Azimio hili kupita ama Kamati nzima ama sehemu ya Kamati kwenda kule haraka iwezekanavyo, kama utakavyoagiza, kuongea na uongozi wa Mkoa, Wilaya na hata na Wanavijiji husika ili kuhakikisha kwamba, jambo hili linakaa sawasawa. Namalizia kwa kuwaomba tena Waheshimiwa Wabunge, tuunge mkono jambo hili kwa sababu ni jema kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndugai, kama kawaida yako umelieleza jambo kwa uwazi na ufasaha mzuri. Nashukuru kwamba, Mheshimiwa Lekule Laizer, amejitoa hachangii kwa maana hiyo nikitazama watu walio karibu na eneo hilo, labda Mheshimiwa Prof. Mwalyosi uniwie radhi nimwite sasa Mheshimiwa Kaika Telele tumsikie halafu tuendelee.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mawazo yangu juu ya Upanuzi wa Hifadhi ya Ziwa Manyara. Kusema kweli naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasisitiza mambo matatu yafuatayo: Jambo hili kwa kweli linahitaji elimu kwa wananchi, linahitaji ushirikishwaji na kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Ndugai, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, waende huko kuzungumza na wote hawa ambao wamewataja, itatusaidia sana kupunguza matatizo ya wananchi huko.

Mimi naunga mkono kwa sababu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na hasa *Crater* ya Ngorongoro ni eneo dogo sana, kilomita za mraba 250. Mapito ya wanyama yameshafungwa, kwa sababu zamani wanyama walikuwa wanatokea Masai Mara kule wanakuja Serengeti, wanakuja Ngorongoro halafu wanaingia Manyara wanakuja Tarangire wanazunguka hivyo. Kutokana sasa na idadi ya watu na watu kufungua mashamba na kujenga makazi kwenye mapito ya wanyama; wanyama hawako tena huru kupita kwenye maeneo ambayo Mwenyezi Mungu alikuwa amewawekea katika asili yao.

Kwa hiyo, kule Ngorongoro siku hizi nina wanyama wengi sana, ambao wamekuwa ni wakazi wa kudumu katika *Crater* ya Ngorongoro, ambalo ni eneo dogo la kilomita za mraba 250. Kwa hiyo, hii *corridor* ikifunguliwa ya kutokea *Ngorongoro Crater* na kupita *Ngorongoro Forest Reserve,* wakiingia pale wakateremkia Mto wa Mbu wakaingia Manyara, wale wanyama ambao ni wakubwa na ni wengi ndani ya *Crater* watapungua. Kwa sababu eneo lile malisho yake na maji ni kidogo sana na kwa hiyo, wanyama wakiwa wengi majani yatakwisha kwa haraka na wanyama wanaweza wakafa kwa kukosa malisho na maji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kamati ilikwenda hata Ngorongoro ikazungumza na Menejimenti ya Shirika, wakazungumza na wafanyakazi, lakini pia nilikuwa nimewaomba kwa sababu walikuwa wamekosa muda, warudi tena wazungumze na Baraza la Wafugaji la Ngorongoro kwa kuwa ni wadau muhimu sana katika eneo lile. Sasa kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati amesema wapo tayari kwenda, wataunganisha na safari yangu ya Ngorongoro na nilishawaomba ili tuweze kutatua matatizo haya ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia hili suala likaangaliwa kwa makini kwa sababu hata tukipitisha Azimio hili na kama kuna matatizo ya wananchi, basi na wanyama nao wanaweza wakapata hiyo tunaita *human wildlife conflict.* Tukiweza kutatua hii migogoro na wananchi, basi wanyama nao watakapoingia kwenye hii misitu wanaweza wakaishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nitolee tu mfano; sisi tulikupokuwa tunaingia *Ngorongoro Island* kutoka Serengeti ili kupisha *National Park* ya Serengeti, tulipewa *Ngorongoro Island*. Tulikuwa tunaishi mpaka chini ya *Crater* kule chini. Baada ya sisi kuondolewa na Jeshi mwaka 1975, wale faru zaidi ya 200 waliokuwa kule wakaisha wamebaki kama 25 tu sasa. Sasa hivi tena kwa mujibu wa *DMP* wanasema, kuna kitu kinaitwa *crater zone,* kwa hiyo watu wasogee kama kilomita 25 *on other side of the Ngorongoro Crater.* Sasa hii ya kusukumasukuma watu namna

hii ni vizuri masuala hata hii kamati ikienda huko tuyazungumzie haya ili katika msitu huu wa Marang wasiendelee kuwekewa vikwazo kama sisi huko. Kimsingi naunga mkono hoja na naomba niishie hapo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Telele, umeongea kwa kifupi na umetupa uzoefu wako wa eneo ambalo unalifahamu sana. Mheshimiwa Prof. Mwalyosi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nitazungumza kwa kifupi. Nianze kwa kusema, napenda kuunga mkono Azimio hili mia kwa mia na kwa nguvu zote. Nitazungumzia maeneo kama matatu manne. Nataka kuanza kwa kusema kwamba, umuhimu wa Hifadhi ya Ziwa Manyara Kitaifa na Kimataifa, hata kwa mazingira yanayozunguka eneo lile kama alivyoeleza Mheshimiwa Ndugai, hakuna anayepinga kwamba ni hifadhi ya pili kuundwa mwaka 1961 baada ya Serengeti na kati ya hifadhi maarufu hapa nchini.

Hii ni miongoni mwa hifadhi zinazozalisha fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya hifadhi nyingine, ikiwa ni pamoja na Ruaha, *Mount Livingstone National Park* ambayo tunategemea kuianzisha na hifadhi zote za kusini ambazo hazizalishi fedha zinategemea hifadhi nne tu za Kaskazini; *Manyara National Park* ikiwa mojawapo.

Vilevile hifadhi hii inasaidia sana, kama nilivyosema, wananchi wanaozunguka pale mamilioni ya fedha yanakwenda kupitia ujirani mwema kusaidia maendeleo. Ukiua Hifadhi ya Manyara, umeua Mto wa Mbu. Mto wa Mbu pale mazingira yale ndiyo kijiji au mji mkubwa katika Wilaya ya Monduli, ambao wanategemea kimapato na kiuchumi. Kinachosukuma pale ni Hifadhi ya Ziwa Manyara. Kwa hiyo, umuhimu wa hifadhi ile hakuna anayeupinga. Yaelekea vilevile kutokana na watu walivyozungumza hapa kwamba, hakuna mtu anayepinga umuhimu wa kupanua hifadhi ile. Sote tuliozungumza, pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Kwaangw’, hata Mbunge wa Babati Vijijini walivyozungumza ni kwamba, tunakubaliana kuna umuhimu wa kuipanua hifadhi hiyo.

Nataka nieleze vitu viwili tu kwa nini ni muhimu. Tunategemea njia hizo za mapito ya wanyama, kwa mfano, kwenda Ngorongoro kupitia Silarei lakini vilevile kupitia Marang kwenda Yaeda chini mpaka Ziwa Eyasi kupandisha Mang’ola kwenda kule juu, wanyama hawakwenda Tarangire kupitia Mashariki ya Ziwa Manyara, lakini vilevile ikiwezekana Kusini mwa hifadhi hiyo kwenda Tarangire na maeneo ambayo ni Mbuga za Simanjiro.

Sote tunaelewa kwamba, uwezekano wa kuyapata maeneo yote hayo ambayo yalikuwa ni mapito ya wanyama, ambayo sasa hivi sehemu kubwa ni mashamba na wananchi wanaishi ni mdogo. Kuna Sheria ya Wanyamapori ambayo inatakiwa kuja hapa pengine Januari, lakini tusije tukadanganyana kwamba, tunaweza tukaya-*secure* maeneo yale yote yaliyokuwa ni mapito ya wanyama, haitawezekana.

Kwa hiyo, umuhimu wa kupanua hifadhi ili wanyama hawa angalau waweze kupumua katika maeneo yanayowazunguka bila ya kutegemea sana kuhamia maeneo mengine ni muhimu sana kushughulikia. Ndiyo maana naona umuhimu wa kuipanua

angalau kidogo hii hifadhi, kama wanyama hao hawataweza kutoka nje ya hifadhi hiyo basi wapate maeneo ya kuweza kwenda kuzalia na kupata chakula wakati wa dhiki, hasa wakati ambapo wa Ziwa linajaa maji na hawana namna ya kuweza kutoka kwenda kupata malisho maeneo mengine nje ya hifadhi. Kwa hiyo, nadhani hakuna mtu anayepinga kupanua hifadhi ile.

Suala hili ni muhimu kama tunataka hifadhi ile iendelee kuwepo pengine milele na milele, la sivyo itakufa kesho kutwa, kama tulivyoambiwa wanyama wengi waliokuwepo wametoweka wote, hawatarudia tena, labda uwalete kutoka maeneo mengine uwapandikize upya pale, lakini hawatarudi pale. Utaratibu huu wa kupotea wanyama, unaendelea kwa vile eneo lile ni dogo sana.

Suala kwamba mashamba yale matatu ni mali ya Serikali, nadhani halina mjadala sana. Kuna vielelezo vinavyoonyesha kwamba, Hifadhi za Taifa wana hatimiliki. Sasa kama Serikali imetoa hatimiliki kwa mashamba yale, inakuwa ni *undisputable*, hatuwezi kushindana tena kwa sababu ni kweli. Vilevile hifadhi ya Marang kuwa mali ya Serikali hakuna anayebisha. Kwa hiyo, maeneo tunayosema tuyapanue tuyaongeze yaelekea wote tunakubaliana kwamba ni kweli ni ya Serikali yanaweza yakachukuliwa. Inaelekea tatizo hapa linalojitokeza ambalo na mimi nakubaliana nalo ni namna ya kushirikisha wananchi wanaozunguka mashamba hayo.

Mimi nakubali kwamba, kuwashirikisha watu wanaokuzunguka ni kitu muhimu sana. Nakumbuka kabisa, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, hilo analitilia mkazo, analikubali kwamba watafanya kila linalowezekana, kuhakikisha kwamba Azimio likipita, haya mambo kama hayakufanywa yatafanywa. Kamati tunakubali chini ya Mwenyekiti wetu, tupo tayari kurudi kule maana mimi nipo kwenye Kamati hiyo, turudi kule tukaongee na wadau wanaohusika tuweke mambo sawa. Kusiwe na kizuizi kwamba, Azimio hili lisipite mpaka tutakapofanya yale, sidhani kama ni sababu ya msingi sana. Hilo la kwenda kulifanya, linawezekana baada ya kupitisha Azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, hakuna anayepinga umuhimu wa kuhusisha wananchi; ni kweli lazima tukawahusishe kwa vile wanakaa mpakani, wanalima mpaka huku Kusini. Lazima tuzungumze wataishi vipi na wanyama watakaowasogelea mpaka kwenye milango yao. Kwa hiyo, hilo hatulipingi ni lazima tukazungumze nao. Kwa mantiki hiyo, mimi nawaomba sana ndugu zangu Wabunge wa kule, wanasiasa wa kule na wananchi, pamoja na Wabunge wenzetu, ambao pengine walikuwa na wasiwasi kuhusu suala hili tukubaliane tu. Tupitishe hili azimio lakini tuwape kazi Kamati, pamoja na Wizara na watu wa *TANAPA*, tuhakikishe kwamba, watarudi kuweka mambo sawa kule kwenye eneo tunalolizungumzia na tuhakikishe hilo linafanyika. Nadhani sisi ni watu wazima na kwenye Kamati yetu ni waumini kabisa wa mambo ya kushirikisha wananchi, tutahakikisha haki inatendeka na wananchi wetu wanatendewa haki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba tena Waheshimiwa Wabunge, sote tukubaliane tulipitishe hili ili tuendelee na hatua ya pili ya kwenda kuweka mambo sawa kule maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, kama kawaida unadhihirisha taaluma yako ya upande wa Uhifadhi wa Mazingira na Viumbe hai.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja iliyo mbele yetu na kwa kutorudia yaliyosemwa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja, kwa sababu zilezile zilizosemwa na wenzangu. Kwa nini naunga mkono hoja? Naomba nianze kwa utangulizi. Haya mambo tunayoyafanya ambayo ni ya maliasili, dira yetu kuu ya Tanzania kwenye Sekta Kuu ya Maliasili ni uhifadhi endelevu. Uhifadi endelevu ni sarafu moja yenye pande mbili, moja ya kuhakikisha uwepo wa maliasili tulizonazo na upande wa pili ni kupata na kuboresha faida zitokanazo na maliasili hii tuliyonayo, kwa faida ya taifa letu na wananchi wake wote. Kwa hiyo, dhumuni kubwa linalopendekezwa hapa ni kuhakikisha kuwa, tunafaidika na uwepo wa maliasili hii kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, hakuna anayebisha hili, isipokuwa nadhani pale ambapo pengine kuna tatizo ni kwa sababu labda tu hatujaangalia kwa kina katika suala zima. Kwa hiyo, nasema uendeshaji wa nchi yetu unaongozwa na miongozo ambayo tunaiweka sisi wenyewe. Miongozo miwili ambayo inahusika katika Muswada huu wa kwanza ni Sera ya Wanyamapori. Sera hii ndiyo inayotuongoza na katika dhima yake kwa Kiswahili nikitafsiri sehemu, kwa ruhusa yako ni kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza rasilimali za wanyamapori. Hii ndiyo Sera ya Tanzania na kwa hiyo, pendekezo la Serikali linapokuja kusema tupanue eneo ili hifadhi ya taifa iwe kubwa zaidi ni kwa mwongozo huu wa Sera na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa pili ambao ni muhimu pia ni Sheria. Maeneo yanayopendekezwa yaongezwe katika Hifadhi ya Taifa ya Manyara; Msitu wa Marang', Shamba Namba Moja, Mbili na Tatu upande wa Majimoto, maeneo haya yanasimamiwa na Sheria ya Ardhi. Maeneo nje ya hapo yale ya Maghala, yanasimamiwa na Sheria Namba Tano ya Vijiji. Sasa hapo Sheria Namba Nne Msimamizi Mkuu ni Serikali Kuu na hapa hakuna Sheria ya Ardhi inayoguswa. Kwa hiyo, Serikali kama isingekuwa inapenda kushirikisha, ingeamua kuleta azimio hapa kwamba imeshatangaza eneo hilo liwe Hifadhi, ingekuwa bado inafanya ndani ya Sheria Namba Nne, ambayo haigusi Sheria Namba Tano ya Ardhi ya Wanakijiji.

Mheshimiwa Spika, hizi ni Sheria zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu na sote tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa, miongozo hii muhimu inazingatiwa. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, sote tuunge mkono hoja hii, sioni tatizo kabisa kwa sababu mwongozo wetu kisheria na vielelezo tumeshagawiwa hapa, unaonyesha wazi msitu na mashamba hayo yanayotajwa yapo kwa mujibu wa Sheria Namba Nne. Serikali yetu ya CCM bado inaona umuhimu wa kuwashirikisha wananchi kwa namna moja au nyingine, pamoja na kwamba hii ardhi siyo ya kijiji kwa mujibu wa Sheria Namba Tano, bado kuna haja ya kuwaeleza kwamba, hifadhi hii inapanuliwa kwa kuongeza sehemu ya

ardhi ambayo ni ya Serikali Kuu, kwa mujibu wa Sheria Namba Nne, kwa sababu ninyi ni wadau muhimu mtafaidika nayo maana shabaha ni ustawi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, noamba pale ambapo panaonekana kuwa kuna mashaka mashaka hivi, miongozo yetu mikuu tuitumie. Jukumu letu sisi Waheshimiwa Wabunge ni kuhakikisha kuwa, miongozo ya uendeshaji wa nchi yetu tunailinda kila siku ili kuhakikisha kuwa shabaha tulizojiwekea za ustawi wa taifa na wananchi wetu zinazingatiwa. Kwa hiyo, kwa mantiki hiyo, Kamati yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti mwenye uwezo kabisa, iliona hakuna haja ya kuweka kipingamizi kwa pendekezo la Serikali na ndiyo maana kwa niaba ya Bunge lako hili Tukufu, ikaona iunge mkono hoja hii.

Mimi kama Mhifadhi ambaye leo sikupenda kuzungumzia sana upande huo, kwa sababu kuna hadithi ndefu. Ukizungumzia kuongeza hifadhi, lijumuishe Ziwa lote la Manyara. Nitasema tena tulichelewa katika maana ya uhifadi wa ndege hususan ndege anayeitwa heroe ambaye ustawi wake asilimia 98 duniani, unategemea kuwepo katika maana ya uhifadhi wa maziwa yaliyopo kwenye bonde la ufa.

Hii ni kwa sababu anapatikana Tanzania na anategemea Tanzania kwa asilimia 98 ya maisha yake. Ziwa Manyara ni muhimu sana katika uwepo wa ndege huyu, ambaye kiutalii anatuingizia pesa nyingi sana; kiutalii, kiutafiti, kielimu na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, bila kusita tuunge mkono hoja hii na nakushukuru sana. *(Makofi*)

**MHE. ANTONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa vile mambo mengi sana yamezungumzwa hasa na wazungumzaji wa leo asubuhi ni kama wameyaelezea na kwa kuzingatia Kanuni zetu sitayarudia. Ila nina wito mmoja tu kwenye maeneo mawili.

Kwanza, Tanzania tunaanza kuonyesha dalili ya kutumia ardhi yetu vibaya. Tunajiona kama tuna ardhi kubwa tu, ndiyo maana miji yetu inapanuka kwa kwenda tambarare, hatukumbuki kujenga maghorofa, hatukumbuki kwamba ardhi ni pamoja na anga, kwa hiyo, tunajikuta tunatumia ardhi yetu vibaya. Hawa wananchi nadhani wa hili eneo linalosemwa, wanataka kwa ajili ya kilimo lakini bado utaona leo tunatoa labda magunia matano au kumi kwa heka. Sasa ufanisi kwenye kilimo huenda usingehitaji tuchukue ardhi kubwa ya nchi hii, ambayo baadae tutakuja kuijutia. Nawapongeza sana watu wa Kusini, ambao wamejua matumizi ya mbolea na wanapata magunia mengi ya mahindi kwenye heka moja. Kwa hiyo, kuna umuhimu tuangalie mwelekeo wetu ukoje.

Mheshimiwa Spika, sasa uchumi wa dunia leo mahali ambapo unapata fedha kwa mtu anakuja kutazama na kupatia fedha, ningetarajia kwamba ndiyo tuangalie zaidi kwa sababu eneo la huduma linaingiza fedha bure. Ndiyo maana utakuta nchi zote zenye maeneo ya utalii, hata fukwe, wanayatunza sana. Sasa sisi tunataka kukimbila kwenye

uzalishaji; uzalishaji ndugu zangu hauna *future* ya kutupeleka pazuri, kwa sababu kwanza nguvu kazi watu hatupo kwenye hali ambayo ni nzuri. Hizi malighafi ambazo tunatakiwa tuwe nazo kwenye maeneo ya uzalishaji, siyo nyingi na tunatumia vibaya. Sasa hili suala lisingekuwa wala azimio, kwa sababu linatuongezea eneo la mtu anakua anatoa fedha zake anaangalia wanyama anaondoka hajaondoka na sungura, swala au tembo wako.

Nadhani inabidi tuangalie zaidi, kwa sababu hili eneo ambalo tunalizungumza, wanyama wa Tarangare wamezibwa, yaani hawawezi ku-move. Ndiyo maana kuna jitihada tulizifanya, ukipita sasa hivi Mheshimiwa Spika, ile Manyara Ranchi ilipewa *African Wildlife* sasa hivi kuna wanyama wameanza kurudi. Sasa kuna Wildlife *Management Area*, ambayo inaitwa Juhibu, ambayo wanyama wanapita kwa sababu wananchi wa sehemu hiyo wameelewa umuhimu wa kuwaruhusu wanyama wakae pamoja na binadamu na wanapata mapato mazuri. Tungetegemea sasa hilo eneo la Juhibu na hili eneo ambalo mwanzo lilikuwa Shamba Namba Mbili, ambalo halina mtu, wananchi wamevamia na hilo eneo ambalo litachukuliwa kutoka kwa huyu Ganji, ambalo alipewa kinyemela, mkilichua lile msiwapatie tena wananchi.

Mkiwapatia tena wananchi, bado kutakuwa na eneo ambalo wanyama hawawezi kupita kutoka Manyara kwenda mpaka Tarangire. Kwa hiyo, kama mtalichukua hilo eneo maana mwenye hilo eneo amekubali kama ulivyoeleza. Wakilichukua, liendelee kuwa wazi kwa ajili ya mapito ya wanyama. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, sioni ubishi hapa na naunga mkono hoja hii. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tena ahsanteni sana. *(Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwanza, kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa njia moja au nyingine. Kuna ambao wamechangia kwa kuongea na wale ambao wamechangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Job Ndugai, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa James Lembeli, ambaye alikuwa Msemaji wa Kamati, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ambaye alikuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Damas Nakai, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Telele na Mheshimiwa Antony Diallo.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Janet Massaburi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashuku wote waliochangia na ninapenda kusema kwamba, michango yao yote ilikuwa mizuri na imeboresha zaidi. Michango ambayo pia imetupa fursa sisi Serikali ya kuweza kutatua mambo mengine, ambayo labda kwa njia moja au nyingine, tulikuwa hatuyaoni. Ninapenda kusema nawashukuru wote, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa majibu ya jumla, halafu nitakuja na majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Jambo la jumla ambalo liliongelewa karibu na Wabunge wote na nimelipokea ni kuhusu ushirikishwaji. Ushirikishwaji ni jambo muhimu kwa dunia ya sasa hivi na pia haliepukiki. Dhana hii ya ushirikishwaji ni mpya, ambayo karibu nchi nyingi za Kiafrika tukiwemo Tanzania, ndiyo tunaanza kujifunza na kuitumia. Ushirikishwaji tulikuwa nao zamani, ulikuwa zaidi ni Serikali inaamua kufuatana na taratibu zilizowekwa na sana ilikuwa inashirikisha ngazi za Wilaya kwenye Halmashauri, ambapo ilikuwa ni kama vile Serikali Kuu inashirikiana na Serikali zake ndogo. Ilikuwa na imani kwamba, Serikali za Mitaa zinaposhirikishwa ni kwamba, wameshirikishwa wananchi kwa sababu pia huko kuna wawakilishi wao ambao ni Madiwani.

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikishwaji wa azimio hili la upanuzi wa hifadhi, napenda kusema kwamba, limefanywa lakini kwa njia ambayo tukichukulia dhana ya ushirikishaji wa hivi sasa ni kwamba haikutosheleza. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwamba, tangu hatua za awali, wananchi walishirikishwa kwa kutumia Halmashauri yao na ndiyo ridhaa ya mashamba yote yale matatu. Mashamba ya Majimoto Namba Moja, Mbili na Tatu yalipatikana kwa kushirikisha Halmashauri yao, ambapo huko na Waheshimiwa Madiwani wapo. Ninazo barua za vithibitisho za Halmashauri mpaka kwenye vijiji na majina yapo ya Mwenyekiti na watu wote na orodha nzima ambao walishirikishwa katika kuamua na kukubali kwamba hifadhi ipanuliwe. Katika kukubali kwao, waliridhia kabisa kwamb, mashamba haya matatu yawe hifadhi. Kwa hali hiyo hiyo ni njia ambayo walishirikishwa, lakini kwa bahati mbaya, huenda wananchi wengine wa kawaida hawakushirikishwa kwa sababu ya mfumo duni wa mawasiliano ulivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ushirikishwaji mwingine ulikuwa ni kati ya kijiji chenyewe cha Mayoka na Wawakilishi wa Wizara ya Maliasili ambao ni *TANAPA*, walikaa kuongelea suala hilo na ikafikiwa muafaka kwamba, wanakijiji cha Mayoka walisema wenyewe wanahitaji ardhi ya kuweza kufanyia mambo yao mengine. Sisi tulikubaliana kwamba, tutawapa ardhi ambayo ndiyo hiyo tunasema ni ya Prince Bernard. Ardhi hiyo, kama Waheshimiwa Wabunge, mnayo ile ramani ni ardhi ambayo baada ya Kijiji cha Mayoka ambayo ni ya pink sijui kama za kwenu zina rangi; kijiji kinachofuatiwa pale chini ndiyo kijiji chenyewe na kwa jina lingine kinaitwa Kijiji Namba Tatu cha Magara. Hicho ndiyo kijiji ambacho tumekubaliana nao.

Kulikuwa kuna mchakato kwa sababu kile Kijiji cha Prince Bernard, kama ilivyosemekana kwamba kuna mtu alikuwa anatumia lile shamba, alipewa yeye alikuwa analima na mpaka leo kuna baadhi ya mazao ambayo yanaendelea kulimwa. Sasa ilitakiwa Serikali ifuate taratibu za kumwondoa yule, lakini kwa bahati nzuri Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, alifanya utaratibu na lile shamba lilipokonywa. Tuli-*revoke* ile hati ya yule mtu aliyekuwa anahusika pale na kilichotakiwa ni kupewa fidia. Sasa tupo katika mchakato wa fidia, lakini nisingependa kuongea mengi. Baada ya hapo, mawasiliano kati ya sisi Serikali na kijiji cha Mayoka, yalikatika kwa kiasi kwa sababu nafikiri walipata ushauri mwingine wakaamua kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kesi ilisikilizwa kwa awamu ya kwanza Arusha na suala hilo likatupiliwa mbali.  Ikasikilizwa kesi ya pili, suala pia lilitupiliwa mbali kwa misingi kwamba, tangu mwaka 2002 mpaka 2007 hakutokea mwakilishi wao wa Kijiji cha Mayoka na kuweza kupeleka ushahidi ili kesi iongelewe.  Baada ya miaka hiyo, ikabidi Mheshimiwa Jaji Chocha aweze kuifutilia mbali kesi hiyo na akasema kwamba, anaifuta kwa sababu ya wanakijiji kukosa kuleta ushahidi, lakini pia akaruhusu kwamba ikiwa baadae wataweza kuwa na ushahidi, basi hiyo kesi wakaifungue tena katika Mahakama ya Ardhi, kwa sababu wakati huo ilikuwa mambo ya ardhi yote yaende huko.

Kwa kipindi chote hicho hadi mwaka huu, wanakijiji hawakupeleka shauri hilo tena Mahakama ya Ardhi na sisi tukajua kwamba, shauri hilo limekwisha kwa sababu ni shauri ambalo lilikuwa linaonekana wazi, mashamba yale ni mali ya Serikali na tukawa hatuna wasiwasi.

Hatuna tatizo sana na uhusianio wetu na Kijiji cha Mayoka.  Napenda kusema kwamba, Mbunge wa Babaiti Vijijini, jana alikiri kuhusu uhusiano mzuri wa Kijiji cha Mayoka na TANAPA.  Kwa kuwa walikaa kimya katika kesi hii, tukajua mambo hayo yamekwisha, hayana chochote na ndiyo tukaona turudi tena kuomba ridhaa ya Wabunge, kwa ajili ya kupanua mapito haya ya wanyama, kwa sababu hali itazidi kuwa mbaya tusipowahi kufanya jambo hilo.  Kwa hiyo, hiyo ni kwa kifupi kwamba ushirikishwaji ulikuwaje.  Napenda pia kukiri kwamba, kwa sasa hivi ushirikishwaji inabidi uende ndani zaidi, kuliko tulivyokuwa tunafahamu zamani.

Kwa hiyo, Wizara yangu mwezi Januari italeta Muswada mpya wa Sheria ya Wanyamapori na katika Sheria hiyo jambo mojawapo tulilolisisitiza ni ushirikishwaji. Chochote kile tutakachoamua, tutahakikisha kwamba, wananchi wameshirikishwa na si mwananchi kwa maana ya Halmashauri au nani, tutakwenda kule chini kabisa kwa wahusika. Kama ni Kijiji cha Mayoka, tutakwenda kuongea na Kijiji cha Mayoka, tuwashirikishe wenyewe mpaka waweze kufahamu katika ushirikiano huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, napenda niongelee jambo ambalo la ujumla kuwa Serikali tunapenda wanyama kuliko wananchi wetu. Hilo si kweli; ni kwamba, Serikali ina jukumu kubwa na jukumu lake namba moja ni wananchi wake na pia haki ya mwananchi inaanza kuliko hata haki nyingine yoyote. Kwa hali hiyo, napenda kusema kwamba, katika utekelezaji wa mambo mengine yanavyokwenda, inaweza ikatokea dhana nyingine potofu ikaonekana kwamba, hatuwapendi wananchi. Katika uhifadhi huu, ndiyo sababu kila wakati tunakuja kuomba ridhaa ili kuonyesha kwamba, tunawajali wananchi kwa kupitia Waheshimiwa Wabunge ili waruhusu jambo hilo lifanyike, kwa kuwa tunajua kwamba binadamu ni muhimu na jambo la kwanza ni kuwaangalia wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda sasa kwa haraka tu niweze kujibu hoja za Wabunge ambao walichangia kwa kuongea.  Ninapenda nianze na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, yeye alihoji kuhusu Kijiji cha Vilima Vitatu na jinsi ambavyo inaweza kusababisha mambo mbalimbali, ikiwemo kuathiri njia za mapito za wanyama. Napenda kujibu kwamba, Kijiji hiki ni moja kati ya vijiji tisa vinavyounda Jumuiya ya Hifadhi ya Burenge, ambayo Mheshimiwa Diallo alisema inaitwa JUHUBI.

Vijiji vimetenga eneo kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori ambao ni *WMA* na ambapo kulingana na Kanuni za *WMA*, Jumuiya inaruhusiwa kujiwekea yenyewe mipango yake na matumizi bora ya ardhi yake. Sasa katika kuweka matumizi bora ya ardhi yake, Jumuiya hii ya JUHUBI katika mambo mbalimbali, waliamua pia kuwekeza katika uhifadhi. Katika kuwekeza huko, waliweza kumpata mfadhili wa Hoteli hiyo ambayo inaitwa Chemchemi, wakawekeza huko na walikubaliana mambo mbalimbali kati ya *WMA* yenyewe, pamoja na mfadhili.

Mheshimiwa Spika, huyu mfadhili kuwekeza hapo, kukatokea kikundi cha wafugaji kwa sababu nao wanajiona wana haki kule ya kuendelea na kazi zao. Hawa wafugaji waliamua kujenga maboma yao. Sasa pale ndiyo mtafaruku ukaanza, kati ya wanakijiji ambao wanataka *WMA* na wana mkataba na mwekezaji na wafugaji; wameamua kwamba nao wanaweka maboma na wanaendelea na ufugaji wao. Sasa katika hali hiyo, ilibidi kijiji kwa kushirikiana na viongozi wake wa *WMA*, wajaribu kuwaomba wale wafugaji waondoke na hapo ndipo kulipokuwa na tatizo.

Mimi nasema kwamba, hii yote ni dhana ambayo tumeileta na ni dhana ambayo ni nzuri katika kuwashirikisha wanavijiji katika uhifadhi. Dhana ambayo inatakiwa itolewe elimu ili pande zote waweze kuelewa; wananchi wanaofuga waelewe na wananchi wasiofuga waelewe. Wote waweze kushirikishwa juu ya umuhimu wa *WMA* ili kila mmoja aweze kushiriki kwenye kazi hiyo. Naomba sisi na Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane katika kuelimisha. Tuhakikishe kwamba, wananchi wanafahamu *WMA* na pia waweze kushirikiana katika kuchuma na kufaidika katika matunda ya *WMA*.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nijibu hoja ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ambaye alikuwa na hoja mbili. Kwanza, alisema kwamba, wananchi hawakushirikishwa katika suala la mipaka ya misitu. Ninapenda kujibu kwamba, wananchi hawakushirikishwa kwa sababu walikufahamu kwamba Msitu huu wa Marang ni wa Serikali kama nilivyosema awali, kwamba ambao ulisajiliwa tangu mwaka 1938. Kwa sababu Mheshimiwa Dr. Slaa alisema kwamba, mwaka 1960 kulikuwa kuna mabadiliko ya ramani, lakini mabadiliko haya ya ramani hayakuweza kutumika hadi leo hii na ndiyo sababu bado tunatumia ya mwaka 1938.

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye suala la Mheshimiwa Dr. Slaa ni kwamba, katika kuweka mipaka ya hii hifadhi, kitu walichofanya wataalam walijaribu kuweka sehemu za *beacon* pembeni kabisa ili isiingiliane na vijiji. Hilo ni jambo la kwanza tulilifanya tukijua kwamba, wanavijiji tayari wameishi pale na asili yao ipo pale, hatuwezi kuwaondoa na hatuwezi kuwaingiza ndani ya mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Dr. Slaa, jambo hilo tulilizingatia lakini pia tukishapata ridhaa yenu tutarudi tena huko kwa ajili ya kwenda kufanya upimaji ili kuweka *beacon.* Tutakapofanya hivyo, tutashirikisha vijiji vyako vifuatavyo; Buga, Geramok na Endara ili kuhakikisha kwamba, tunapoweka hizi *beacon* zisipite katika vijiji vyao husika. Baada ya hapo, naomba nikusihi uunge mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aliongelea pia mwananchi ambaye aliuawa huko kwenye Misitu ya Marang. Kweli Serikali tuna habari hiyo na tunasikitika sana. Hiki kifo kilitokea katika purukushani ya kupambana kati ya askari wetu wa doria na wananchi ambao walikwenda kukata miti kwa ajili ya mbao. Sasa katika purukushani zile, ndiyo ikatokea hayo mauaji lakini ni kitengo ambacho sisi tunakifuatilia. Katika Sheria mpya ni mambo ambayo tutazidi kuyatolea elimu zaidi, wananchi waelewe na askari wetu wajue mipaka ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Slaa pia aliongelea kuwa Askari wa *TANAPA* wana tabia ya kuingia mpaka kwenye nyumba za watu ndani, wakikuta stuli wanaichukua wanasema hii ni ya mbao yetu. Siwezi kukataa, haya ni matatizo ya kiutendaji yanayotokea; ni matatizo ambayo kila binadamu ana akili yake.

Ninapenda kusema kwamba, jambo hili nalikemea kwa nguvu zangu zote kwamba, watu wasinyanyaswe mpaka vyumbani mwao. Kuna taratibu nzuri tu, kama mwananchi ataonekana kakiuka au kachukua mali bila uhalali, kuna taratibu nzuri za kufuata ili kuhakikisha kwamba, hata kama ni kwenda kufuata stuli kuna taratibu zake na sio kuingia na kuleta bugudha. Hilo nalikemea na halitatokea tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mgana Msindai, aliunga mkono hoja moja kwa moja, lakini alitushauri kwamba, tatizo la Vilima Vitatu ambalo Mheshimiwa Magdalena Sakaya aliliongelea pia, tulitazame vizuri kuwe na uhusiano mzuri.

Mheshimiwa Spika, tumekubali ushauri huo na sisi pia tutakwenda kusaidia katika kuweka uhusiano mzuri kati ya wafugaji walioko Vilima Vitatu na wananchi ambao wameanzisha *WMA* ili kuhakikisha uhusiano unakuwa mzuri na ndio mojawapo ya elimu tukazokwenda kufanya katika maeneo yote hayo ya huko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Damas Nakei, alisema kwamba, Shamba Namba Moja na Namba Nne yaliyotolewa Kijiji cha Mayoka ni mali ya Kijiji cha Mayoka. Mimi nasema ni kweli Shamba Namba Moja na Namba Nne yalitolewa kwenye Kijiji cha Mayoka, lakini Mheshimiwa hapa hakuweza kutofautisha. Shamba Namba Moja ambalo Kijiji cha Mayoka kimepewa siyo katika msitu ule; samahani, kama mna zile ramani, kuna msitu ule una rangi ya njano. Msitu wa rangi ya njano ni Majimoto Namba Moja. Hawakupewa Namba Moja ya Majimoto, walipewa Namba Moja ya Magara.

Kwenye *pink* ile ni Kijiji cha Mayoka mle kuna namba moja. Hiyo ndiyo Namba Moja ambayo walipewa na nina barua za uthibitisho kuhusu jambo hilo kwamba kweli wamepewa Namba Moja na Nne. Namba Moja ni ya Magara, Namba Nne ndiyo ikuwa ya maji moto. Kwa hiyo, ni kweli ila kulikuwapo na *confusion*, hawakujua wamepewa kipi. Barua za Halmashauri na kila kitu ninazo hapa, kwa uthibitisho.

Mheshimiwa Spika, alihoji pia kuhusu kesi iliyofunguliwa, lakini nimeiongelea kesi kwa mapana kwamba, kweli ilifunguliwa na ilishafungwa na taratibu zote nimeziongelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda nimjibu Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, yeye aliongelea kuhusu wawekezaji watakaokaribishwa kwenye eneo la Shamba Namba Tatu Magara, wahakikishe wanawashirikisha wananchi angalau kwa asilimia 40 ya uwekezaji wote. Hilo sisi tumelipokea na tunasema kwamba, tukiwapa Shamba Namba Tatu la Magara, shamba lile ni la uhifadhi na sisi tutawakabidhi Mayoka waingie kwenye *WMA* na wao waweze kunufaika. Kwa hiyo, kunufaika siyo asilimia 40, kama watalichukua asilimia 100 ni la kwao, watakuwa wananufaika watu wa Mayoka.

Mheshimiwa Spika, aliongelea kuhusu Jamii ya Wahadzabe wanaotegemea kitoweo wanapotaka kibali cha kulinda kitoweo wanapata wapi; na nani anawapa? Hilo jambo tumelitambua na mtazamo huo wa Mheshimiwa Mbunge sisi tumeuona na sasa hivi katika Sheria Mpya ya Wanyamapori, jambo hilo tumeliweka bayana na tunarekebisha kwamba kutakuwa na utaratibu wa kutengwa sehemu maalum ya jamii kama hiyo, waweze kupata kitoweo na shughuli zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole Sendeka naye aliongelea kuhusu ushirikishwaji, ambao nimeuongelea na tunapokea ushauri wake. Tumeahidi kwamba, ushirikishwaji utaongezwa mara dufu. Pia aliongelea kuhusu mpaka wa Mkungunero. Naomba kukiri kwamba, Pori la Akiba la Mkungunero limekuwa na migogoro mingi, baina yake na wananchi. Katika kulitatua hilo, sasa hivi Wizara tumeamua kuingilia kati na tupo katika hatua mbalimbali za vikao na kuleta suluhisho katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Ole Sendeka aliongelea kwamba, Serikali iandae *Building Code* ambayo itawezesha kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kule kuwe na taratibu ambazo tumeweka za aina ya nyumba ambazo zitajengwa. Wamasai wasiendelee tu kukaa kwenye matembe yao na manyasi ili na wao waweze kuruhusiwa au kuwe na kibali maalum kwamba, wajenge wanavyotaka, lakini kuwe na msimamo; *standard* gani ambayo haitaathiri mambo mbalimbali kule ya kihifadhi nao waweze kujenga nyumba za namna hiyo. Tumepokea huo ushauri na wala hauna tatizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole Sendeka pia alinikumbusha kuhusu masuala ya Ngorongoro, ambayo aliyaongelea siku ambapo tulikuwa tunajadiliana Azimio hili. Yale masuala nimeyapokea na nimeanza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', naomba nianze kwa kusema, alishaniambia kabisa yeye haungi mkono. Sasa mimi naomba nianze kwa kukuomba kwanza, nikupigie goti, naomba uunge mkono kwa sababu mambo mengi nimeshayaongea na umenielewa. Jambo lililokuwa limebakia ni kuhusu hawa wananchi kwamba, tuwape nao sehemu. Napenda kutamka rasmi kwamba, Shamba Namba Tatu la Magara ambalo lilikuwa la Prince Bernard, sisi tutalikabidhisha kwao baada ya kumaliza taratibu za kumwondoa aliyeuziwa.

Tumesha-*revoke* baada ya sisi kulipa fidia na hiyo fidia Serikali tuna uwezo nayo, tunatakiwa tuharakishe. Mimi napenda nimhakikishie kwamba, tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wa Wizara yangu, kuharakisha hiyo fidia ili hilo shamba tuwape wananchi. Naomba niombe kwamba, najua wapiga kura wako wanakusikia, wapiga kura wa Mheshimiwa Nakei wanasikia, kwa sababu Kijiji cha Mayoka kilikuwa mpaka leo hii hakijajiunga na *WMA*, hii inayoitwa JUHUBI. Sababu za kutokujiunga zilikuwa mbili; sababu ya kwanza walisema hawajiungi kwa sababu ardhi yao waliyonayo haitoshi ni kwa ajili ya matumizi yao, hawawezi tena kuitoa kwa ajili ya *WMA*. Kwa sababu kila kijiji ili kijiunge, kinatakiwa kikate sehemu ya ardhi yake itoe kwamba hii iwe ya hifadhi. Sasa hawa walikataa, wakasema hawataki. Sababu nyingine, tulikuwa na kesi nao Mahakamani, wakaona hawa *TANAPA* wanarudi kwa mlango wa nyuma kuleta mambo ya *WMA* ili watupokonye na hapa tulipo. Kwa hiyo na hiyo wakasema sisi hatujiungi.

Sasa nawaomba Mheshimiwa Kwaangw' na Mheshimiwa Nakei mtusaidie, sasa hivi nina hakika wananchi wanasikiliza kwa sababu tangu jana najua wanawapigieni simu kutaka kujua hatima ya hili jambo ni nini. Tutatoa hiyo ardhi, lakini tunawaomba basi hiyo ardhi iheshimiwe, tuitumie katika mambo ambayo wananchi watanufaika. Wakati huo huo pia isaidie na uhifadhi, kwa sababu sehemu hizo pia hazikwepeki, wanyama watapita na wanyama wote wanaopita wanapita kwenye hifadhi yenu. Itakuwa hifadhi ya wananchi, watapita humo na ndio manufaa mtakayokuwa nayo. Kwa hiyo, nawaomba wananchi wasiogope tena, wakubali hilo eneo walichukue na pia wajiunge na *WMA* ile ya JUHUBI kwa sababu wamebakia peke yao ambao hawajajiunga. Hilo namba nihakiishe kwamba litatendeka, siyo ahadi hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo pia, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Omar Kwaangw' na Mheshimiwa Nakei, kuhusu sisi kwenda kuwashirikisha wananchi kwenye maongezi na elimu kuhusu mambo mbalimbali ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa ruhusa yako, kukuomba kwamba, Kamati ya Bunge pamoja na Wafanyakazi wa Maliasili, tutapenda kushiriki kwa ruhusa yako na Wizara yangu itakuwa tayari kugharimia hiyo safari ili tuzunguke, tukaongee na wananchi, tuwape elimu inayostahili, lakini pia tuwashirikishe katika jambo hili kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Raynald Mrope, alitoa ushauri wa kiujumla kuwasihi Waheshimiwa Wabunge tukubali, kwa sababu hili jambo ni la faida na tija kwa nchi. Napenda nimshukuru, ahsante sana.

Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, pamoja na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, walizidi kutoa msisitizo kuhusu ushirikishwaji wa masuala ya uhifadhi. Napenda kusema kwamba, tumeupokea ushauri na tutafanya hivyo na wala hatuna tatizo na jambo hilo. Napenda kuwashukuru kwa ushauri wenu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, kuna Wabunge ambao wamechangia leo, akiwemo Mheshimiwa Job Ndugai. Napenda nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa sababu na mimi pia ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Kwa hiyo, napenda nimshukuru

kwa jinsi ambavyo ameweza kupambanua jambo hili, ili liweze kueleweka na pia kufuatana na taaluma yake na yeye ni mhifadhi kwake ni jambo ambalo aliweza kulielewa kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi naye pia alikuwa anazidi kutuelimisha na kusisitiza jambo hili. Napenda nimshukuru.

Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, pia napenda nimshukuru, ametueleza mfano mzuri kwa sababu yeye amebobea katika masuala ya utafiti wa ndege na alitoa mfano ule wa ndege.

Mheshimiwa Ole Telele, nakushukuru na ushauri uliousema tumeupokea kabisa na tutaendelea kufanya hivyo. Umeomba tutakapokwenda Moyamayoka tupitie na Ngorongoro. Tutafanya hivyo, kuja kuongea na wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru pia Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa sababu ni mzoefu wa hiki Kiti cha Uwaziri nilichopo mimi. Anafanya masuala mtambuka vizuri sana na napenda kusema kwamba, kipindi kifupi nilichokaa kwenye Wizara hii katika sehemu ambazo nimeshiriki; shughuli za uhifadhi na utalii mpaka nje ya nchi, nimeona kiasi gani sehemu nyingine, nchi ndogo sana au mji mdogo sana unavyonufaika kwa ajili ya utalii tu. Watu wanakuja kuona, pesa inaingia nyingi sana na wananchi maisha yanaboreka. Kwa hiyo, kwa kitu hicho na mimi naomba tujitahidi na elimu tutazidi kuitoa kwa wananchi ili zaidi ya kilimo, pia waangalie na upande wa utalii; watafanya nini ili kuhakikisha kwamba wanaweza kuingiza pesa nyingine kwa watu kuona tu. Napenda kuwashukuru hao wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi; Mhehimiwa Mohamed Abdulaziz, naye ametoa ushauri wa ushirikiano, tumeupokea. Ametoa ushauri kwamba, kesi ile na wanakijiji tuhakikishe inaisha kwa usalama, pia tumeupokea.

Mheshimiwa Said Arfi, aliniambia kwamba, nisipoeleza sawa sawa haniungi mkono. Sasa Mheshimiwa, napiga goti tena, naomba na wewe uniunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Arfi alisema kwamba, anaona tunapenda mno hawa wanyama kuliko binadamu. Napenda kusema kwamba, sisi tunawapenda binadamu kuliko wanyama, ila wale hawana wa kuwasemea inabidi tuwasaidie. Aliongelea pia kwamba, hizi kero za kila wakati tunazidi kuongeza ardhi, tunazidi kuongeza ardhi, itafikia hatua binadamu nao wanazaana, watataka pa kukaa itafikia hatua itakuwa ngumu, itakuwaje? Sasa ndio hivyo basi, wao kule wana Mbuga kubwa ya Katavi, hawa wanyama wengine kama Nyumbu tuwahamishie huko, lile pori halina wanyama.

Ameomba na wengine tuwahamishie huko; Mheshimiwa ni kwamba, hayo mawazo nimeyapokea, lakini nitashirikiana na wataalam tusikie nao wanasema nini. Napenda tu nikuhakikishie kwamba, mawazo uliyoyaongea kuhusu upanuzi wa ardhi, ukweli ni kwamba, Serikali haina nia ya kusema itaendelea kupanua ardhi kwa ajili ya wanyama na wananchi wakose sehemu yao, kwa sababu katika upanuzi unatokea tu pale

ambapo hali ikizidi kwamba hapa sasa tunataka kupanua. Kama nilivyosema, sheria mpya hatutafanya kazi ya namna hiyo tena bila kuwashirikisha wanakijiji wa sehemu hiyo. Tukishakubaliana nao, ndio tutapanda ngazi kwenda sehemu nyingine na hatimaye tukisharidhika na wale wakiridhia, tutarudi Bungeni kuwaombeni ruhusa. Hatutafanya kienyeji wala kwa mabavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kueleza hapa mbele. Naomba tena nirudie kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, naomba tuunge mkono hoja hii ya Azimio la Kupanua Hifadhi ya Manyara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kwa jinsi alivyowasilisha hoja hii. Mchango wenu Waheshimiwa Wabunge, umetusaida sana baadhi kuelewa vizuri hali halisi ya jambo hili, ambalo pengine lilionekana jepesi lakini pia ni gumu. Sasa sijapata taarifa yoyote ya hoja ya kufanya mabadiliko Kanuni ya 57. Kwa hiyo, halina mabadiliko hili Azimio na kwa hiyo sasa nitawahoji, tulichonacho hapa ni Azimio la Bunge ili Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hata Mheshimiwa Kwaangw' ameafiki! Kwa hiyo, nafurahi kuwatangazia kwamba Azimio la Bunge la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara sasa limepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

**KATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu wa Bunge zimekamilika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sina hakika kama muda uliosalia unatosha kumwezesha Waziri Mkuu, kuwasilisha hoja ya kuliahirisha Bunge, bila kuathiri kanuni inayohusu muda wa kukaa humu Bungeni pale saa saba kamili. Kwa hiyo, nitamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, awasilishe Mbele yetu, hoja ya kuomba Bunge liendelee baada ya saa saba kamili hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapomaliza kusoma hoja yake.

## HOJA YA KUONGEZA MUDA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa vile pengine muda uliobaki, hautatosha kwa Mheshimiwa Waziri, kumaliza hotuba yake ya kuahirisha Mkutano huu wa Bunge, hivyo

naomba Bunge lako kwa kutumia Kanuni ya 28, limwezeshe Mheshimiwa Waziri Mkuu kumaliza hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwasilisha hoja yake, napenda mtambue uwepo wa Mama Tunu Pinda, pale kwenye *Speaker's Gallery*. Karibu sana Mama Pinda. Tunashukuru mara kwa mara unapokuja hapa Bungeni, kuweza kufuatilia yale yanayotokea. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hoja ya Kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa hoja ya kuliahirisha Bunge lako Tukufu, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kufikia salama siku ya leo. Namshukuru kwa kutuwezesha wote kukamilisha shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii ya mwanzo kabisa, kuvipongeza Vyama vyote vilivyoshiriki katika Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Tarime uliofanyika tarehe 12 Oktoba, 2008, kufuatia Kifo cha Mpendwa wetu, Mheshimiwa Chacha Wangwe. Kwa njia ya pekee, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, kwa kushinda Uchaguzi huo kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Nawapongeza Wananchi wa Tarime, ambao pamoja na changamoto nyingi wakati wa Kampeni, hatimaye walikamilisha Uchaguzi kwa kupiga kura kwa amani, utulivu na mshikamano. Nawapongeza wote kwa maamuzi yao ya Kidemokrasia, waliyotumia kuchagua mtu wanayempenda awawakilishe kwenye Bunge hili. Napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha Watanzania wote kuwa, wajibu wa Kidemokrasia ni kulumbana kwa hoja na siyo mapigano, vitisho wala vurugu. Katika chaguzi zetu, tuepuke mambo yote yanayoweza kuvuruga amani na utulivu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe kwenye Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili.

Vilevile, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shelukindo, Mbunge wa Kilindi, Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, kwa kuchaguliwa kuwa Wajumbe kwenye Bodi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kwa wote waliochaguliwa, tunawapongeza sana. Mategemeo yetu sote ni kuwa wataliwakilisha Bunge hili na Watanzania wote kwa ujumla vizuri katika Bodi za Taasisi hizo. Ninaamini kwamba, uwezo wanao na ndio maana wamechaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu, Waheshimiwa Wabunge, walipata nafasi ya kuiuliza Serikali jumla ya Maswali 121 ya Msingi na mengine mengi ya Nyongeza. Nitumie fursa hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, walioweza kuuliza Maswali ambayo kwa ujumla wake yalilenga katika kujua na kuhimiza shughuli za Maendeleo katika Majimbo, Sekta zinazohusika na maendeleo ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Sekta zilizohusika, kwa kutoa majibu ya maswali hayo kwa ufasaha na kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia Mheshimiwa Waziri Mkuu naye aliulizwa maswali 19. Naomba vilevile niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliouliza, kwani wameniwezesha na mimi kupata nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo katika kuyajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliweza kujadili na kupitisha Miswada ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi wa Mwaka 2008 *(The Contractors Registration (Amendment) Bill, 2008);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Miliki za Sehemu za Majengo wa Mwaka 2008 *(The Unit Title Bill, 2008);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008 *(The Mortgage Financing (Special Provisions) Bill, 2008);*

(iv) Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi wa Mwaka 2008 *(The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008);*

(v) Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama wa Mwaka 2008 *(The Animal Welfare Bill, 2008);*

(vi) Muswada wa Sheria ya Kutoa Fidia kwa Wafanyakazi wa Mwaka 2008 *(The Workers Compensation Bill, 2008);* na

(vii) Muswada wa Sheria ya Afya ya Akili wa Mwaka 2008 *(The Mental Health Bill, 2008).*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia lilijadili na kuridhia:-

(i) Azimio la Bunge kuhusu Kumpongeza Rais Mteule wa Marekani, Mheshimiwa Barrack Obama, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 44 wa Marekani; na

(ii) Azimio la Bunge kuhusu Upanuzi wa Hifadhi ya Ziwa Manyara.

Mheshimiwas Spika, vilevile Bunge lako Tukufu lilipokea Taarifa za Kamati mbalimbali zifuatazo:-

(i) Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini;

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge Kuhusu Utendaji Usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Containers Terminal Services (TICTS)*; na

(iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge Juu ya Utendaji Usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania *(Tanzania Railways Limited (TRL))* Uliofanywa na Kampuni ya Rites ya India.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli za Serikali na Hoja za Waheshimiwa Wabunge, ambazo ziliwasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, walioshiriki kupokea, kujadili na kutoa ushauri kuhusu Miswada, Maazimio na Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa hapa Bungeni wakati wa Mkutano huu. Michango yao itazingatiwa na itasaidia kuboresha juhudi za Serikali katika kuwaletea Wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepata nafasi ya kujadili Taarifa ya Kamati ya Rais ya Sekta ya Madini, iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Mark Bomani. Bila shaka, Waheshimiwa Wabunge, watakubaliana nami kwamba, Kamati ilifanya kazi nzuri na kwa umakini mkubwa. Mapendekezo yaliyotolewa yataisaidia Serikali, kuboresha Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Nchi yetu. Baadhi ya mapendekezo na ushauri uliotolewa, yatatekelezwa kwa kipindi cha muda mfupi na mengine yatahitaji muda mrefu kidogo kutekelezwa.

Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imeanza utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo na tutakuwa tunaliarifu Bunge lako, hatua tutakazokuwa tunachukua kila wakati. Mapendekezo mengine kama ya kurekebisha Sera na Sheria ya Madini, yanaendelea kufanyiwa kazi, kwani mchakato wa kurekebisha Sheria na Sera ulishaanza hata kabla ya kuundwa kwa Kamati ya Jaji Bomani.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane kwamba, ili Sekta ya Madini itoe mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya uchumi wetu na kuongeza ajira nyingi, tunahitaji kuyaongezea thamani madini yetu hapa Nchini.

Nilipotembelea Namibia hivi karibuni, nilijionea Kiwanda cha Kukata na Kusafisha Almasi, ambacho kinafanya kazi nzuri ya kuongeza thamani Madini ya Almasi kwa kutumia Almasi ghafi, inayozalishwa Namibia jambo ambalo limeipatia Namibia fedha nyingi pamoja na ajira. Hata hivyo, ili kuongeza thamani ya Madini, kunahitajika uwekezaji mkubwa na uhakika wa malighafi za kutosha.

Hizi ni baadhi tu ya changamoto ambazo hatuna budi kukabiliana nazo. Katika kufanya mabadiliko makubwa kwenye Sekta ya Madini, tunaweza kuanza na sisi kushirikiana na Sekta Binafsi, kuongeza thamani Madini hapa Nchini badala ya kuyauza ghafi. Tunalifuatilia suala hili kwa ukaribu mkubwa na nina imani tutafanikiwa. Nichukue fursa hii kuishukuru kwa dhati, Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa kuichambua vyema Taarifa ya Jaji Bomani na kutoa mapendekezo yake mazuri kwa Serikali. Vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia kikamilifu katika mjadala wa Taarifa hii na niwahakikishie kwamba, michango yenu itafanyiwa kazi inayostahili. Nawasihi wote tuvute subira ili Wataalam wapate nafasi ya kuyashughulikia mapendekezo yenu ambayo nina imani yatasaidia sana katika jitihada zinazoendelea za kuboresha Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 – 18 Oktoba, 2008, nilishiriki katika Mkutano wa Kuhamasisha Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo, uliofanyika Mkoani Morogoro ambao ulihusisha Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Morogoro na Kigoma. Lengo kuu lilikuwa ni kuweka Mikakati ya namna ya Kuongeza Uzalishaji wa Mazao hapa Nchini, hususan kupitia utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)*. Tuliona ni vyema kuanza na Mikoa hii sita katika mchakato huu kwa sababu mbalimbali, lakini kubwa ni kwamba, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Ruvuma, Rukwa, Iringa na Mbeya, ndiyo ambayo kihistoria imekuwa na mchango mkubwa katika uzalishaji wa mazao ya chakula na hivyo kuifanya ijulikane kama *"The Big Four"*. Mkoa wa Morogoro ulijumuishwa na Mikoa hii ya Nyanda za Juu Kusini, kutokana na changamoto uliopewa na Mheshimiwa Rais kuwa Ghala la Taifa la Chakula. Vilevile Mkoa wa Kigoma nao ulijumuishwa kutokana na fursa ilizonazo katika Kilimo zinazofanana sana na Mikoa hiyo mingine mitano.

Mheshimiwa Spika, takwimu za uzalishaji za mwaka 2007/2008, zinaonyesha kuwa Mikoa hii sita inachangia Tani milioni 3.9, sawa na asilimia 36 ya mahitaji ya chakula Nchini. Kitaifa uzalizalishaji ulifikia Tani milioni 10.78 za chakula kwa mwaka huo. Matarajio ni kwamba, kufanikiwa kwa Mikoa hii sita katika Kilimo, itakuwa chachu kwa Mikoa mingine kutumia mbinu na Mikakati iliyofikiwa kwenye Mkutano huo ili kuongeza uzalishaji kwa Nchi nzima. Dhamira yetu ni kufanya Mikutano mingine kama huu kwa Mikoa mingine kwa kuzingatia hali ya Mikoa inayofanana Kijiografia na Hali ya Hewa.

Mheshimiwa Spika, Uongozi wa Nchi yetu katika ngazi zote; Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa, lazima utuwezeshe kutekeleza yale tuliyojifunza kwa vitendo zaidi. Mambo hayo ambayo hatuna budi kuyafuatilia kwa karibu ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, imejidhihirisha kuwa Kilimo cha Tanzania bado kina tija ndogo sana na hivyo mavuno hayalingani kabisa na kiasi cha eneo linalolimwa. Kwa mfano, wakati Wakulima wengi sasa hivi wanazalisha mahindi wastani wa Tani 1.2 kwa hekta, lakini kama Kanuni za Kilimo Bora zitatekelezwa, wanaweza wakaongeza uzalishaji. Takwimu za mwaka 2007/2008 zinaonyesha kuwa, tulilima mahindi hekta milioni 2.88 na tukavuna Tani Milioni tatu. Lakini kama tungetekeleza Kanuni za Kilimo

Bora, ilitakiwa kuzalisha Tani tano kwa Hekta na kuvuna Tani milioni 14.4 katika eneo hilo hilo. Hivyo, uzalishaji huu wa mahindi unathibitisha kuwa tija ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu Viongozi na Wataalam, kumsaidia Mkulima kuongeza Tija ili aweze kupunguza umaskini na kuongeza akiba ya Hifadhi ya Chakula cha Taifa. Lengo ni kuongeza uzalishaji ili eneo dogo linalotumika, litoe mazao mengi kwa kutimiza Kanuni za Kilimo Bora. Mfano, Mkulima anaweza kuongeza uzalishaji kutoka magunia 12 ya sasa kwa Hekta na kufikia takriban magunia 30. Hivyo mkulima sasa anaweza kuweka akiba ya magunia 15 na kuuza 15. Hivyo atakuwa ameongeza kipato chake na kuongeza akiba ya chakula cha Taifa. Huu ni ukombozi mkubwa kwa mkulima na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo, bei kubwa, usambazaji na matumizi yasiyo sahihi bado ni tatizo. Upatikanaji wa Mbolea, Mbegu Bora, pamoja na Madawa ya Viatilifu hayakidhi mahitaji. Kwa mfano, mahitaji ya aina mbalimbali ya Mbolea yanakadiriwa kuwa ni Tani 400,000 kwa mwaka. Mwaka 2007/2008, zilipatikana Tani 211,000, sawa na asilimia 53 ya mahitaji. Kwa Msimu wa Kilimo wa Mwaka 2008/2009 hadi mwishoni mwa Oktoba, 2008, kiasi cha Mbolea kilikuwa Tani 188,600 tu. Kiwango cha mbolea tani 150,000 kitauzwa kwa bei ya Ruzuku. Hiki ni kiasi kidogo kwa kuzingatia kwamba Msimu wa Kilimo ndiyo umekaribia. Hata hivyo, Serikali imeongeza kiasi cha fedha kwa ajili ya Pembejeo kutokana na fedha za *EPA*, kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi katika Hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni. Ni matumaini yangu, nyongeza hii italeta mabadiliko katika suala zima la upatikanaji wa Pembejeo Nchini na hivyo kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu wa upatikanaji wa Mbolea Nchini, Serikali imetoa udhamini kwa Kampuni ya Mbolea Tanzania *(Tanzania Fertilizer Company)*, ili waweze kuagiza Mbolea zaidi ambayo tayari imekwishaagizwa na tutaipata hivi karibuni na kusambazwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tutaanza kutumia mfumo wa *VOCHA*. Lengo ni kuhakikisha kwa kiasi kikubwa, mbolea ya ruzuku inawafikia na kuwanufaisha Wakulima moja kwa moja. Ninaelewa ugumu wa utaratibu kukubalika hivi sasa, kutokana na uwezo wetu mdogo wa kuwafikia Wakulima wengi. Mwanzo wa jambo lolote huwa mgumu. Wito wangu kwa Viongozi na Wananchi wote ni kuwa, tuukubali utaratibu huu uanze ili tupate uzoefu. Uzoefu tutakaoupata utatusaidia sana katika kufanya maboresho ili kuweza kukidhi mahitaji ya Mbolea kwa Wakulima hapa Nchini. Mfumo wa *VOCHA* ni bora kuliko tulioutumia mwaka jana, kwa sababu mbolea ya ruzuku inawafikia Wakulima moja kwa moja na hivyo kumfanya kila Mkulima atumie mbolea.

Mheshimiwa Spika, natoa Wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote, washiriki katika kuwaelimisha Wakulima umuhimu wa matumizi ya mfumo wa *VOCHA*, tukishirikiana kwa pamoja Mfumo huu wa *VOCHA* utafanikiwa na hivyo kuwanufaisha Wakulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhaba wa Maafisa Ugani, ni lazima wale waliopo watekeleze wajibu wao wa kuwawezesha Wakulima kupata Elimu itakayowawezesha kutekeleza Kanuni za Kilimo Bora. Pamoja na upungufu wa Maafisa Ugani katika Mikoa, Maafisa Ugani waliopo wanaweza kuleta mabadiliko makubwa ya Kilimo chetu, kama watasimamiwa vizuri na kupewa vitendea kazi. Kwa mfano, Mkoa wa Mbeya una Maafisa Ugani 488; Morogoro 355; Iringa 428; Ruvuma 20; Rukwa 202 na Kigoma 204. Pamoja na upungufu uliopo, Wataalam hawa waliopo wakitumiwa vizuri, wakawezeshwa kwa kupewa vitendea kazi kama vile Pikipiki na zaidi ya yote wao wenyewe wakawa na Mpango wa Kazi na wakijituma na kutimiza wajibu wao, Mapinduzi ya Kilimo Tanzania yanawezekana kabisa.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunazo Taasisi za Umma kama Magereza, Kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Vyuo vya Kilimo na Mifugo, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo ni lazima viwe vitovu vya Mapinduzi ya Kilimo Nchini. Ni muhimu katika vita hii tukatumia kila nguvukazi iliyopo. Ni jukumu la kila Halmashauri kuhakikisha inatoa mafunzo ya msingi ya Kanuni za Kilimo Bora kwa Vijana wasiopungua 20 katika kila Kijiji, watakaosaidia katika utoaji elimu hiyo kwa Wakulima chini ya usimamizi wa Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia tena; ni jukumu la kila Halmashauri kuhakikisha inatoa mafunzo ya msingi ya kanuni za kilimo bora kwa vijana wasiopungua 20 katika kila kijiji, watakaosaidia katika utoaji wa elimu hiyo kwa wakulima chini ya usimamizi wa Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, aidha, upo umuhimu wa kuanzisha Mabaraza ya Kilimo ya Kata, ambayo yatatoa msukumo mkubwa katika Kilimo. Vilevile Sekta Binafsi ishirikishwe katika kutoa huduma za Ugani kwa Wakulima na Wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao. Nitamwomba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, atoe maelekezo mahususi namna Mabaraza ya Kilimo ya Kata yatakavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kila Mkurugenzi wa Halmashauri Nchini, ahakikishe kuwa Maafisa Ugani wanaacha kukaa Ofisini na badala yake wawafuate Wakulima popote walipo ili kujionea shughuli zao za Kilimo na kutoa ushauri stahiki, wawe na Ratiba ya Kazi na Daftari la Wakulima wanaowahudumia. Kama vile Madaktari wanavyokuwa na Daftari la Wagonjwa na kila siku wanajua watawaona Wagonjwa wangapi na saa ngapi, ni muhimu na Maafisa Ugani wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, kama vile Walimu walivyo na Daftari la kuandaa vipindi vya kila siku, Maafisa Ugani nao wawe na Daftari linaloonyesha Mpango wa Kazi wa kila siku. Wakurugenzi wa Halmashauri waweke vigezo vya tathmini kwa Maafisa Ugani wote na wahakikishe usimamizi mzuri na ufuatiliaji unakuwepo wakati wote. Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Wilaya, wafuatilie taarifa za Madaftari ya Maafisa Ugani wajue wanafanya nini. Vilevile Halmashauri zihakikishe zinawapatia

Maafisa Ugani makazi karibu na maeneo ya Wakulima ili wawe karibu katika kutoa ushauri kwa Wakulima.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta kweli Mapinduzi ya Kilimo Nchini, hatuna budi kuchukua hatua za makusudi za kuongeza ushirikiano wa karibu kati ya Watafiti, Wagani na Wakulima. Lazima Wataalam mbalimbali wahakikishe kuwa, matokeo ya tafiti zao yanawafikia Wakulima na kwa wakati. Aidha, lazima kuweka taratibu zitakazowezesha Teknolojia sahihi kutangazwa na kuenezwa kwa Wakulima ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa Mbegu Bora, nimeielekeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ihusishe na kushirikisha Taasisi za Serikali kama Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa ili mashamba yao yatumike kikamilifu kuongeza uzalishaji wa Mbegu Bora, ambazo asilimia 75 sasa hivi tunaagiza kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, Kilimo cha Umwagiliaji Maji bado kipo chini sana, kulingana na maeneo ambayo yanaweza kutumika katika Kilimo cha Umwagiliaji. Kwa mfano, Mkoa wa Morogoro una jumla ya Mito 143 inayotiririsha maji mwaka mzima. Kati ya hekta 123,500 zinazofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji ni hekta 8,800 tu ndizo zinazotumika, sawa na asilimia 7.0 ya eneo lote linalofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji. Tatizo hili lipo karibu Mikoa yote Nchini.

Mheshimiwa Spika, Kitaifa tunazo hekta milioni 29.4 ambazo tunaweza kuendesha Kilimo cha Umwagiliaji, lakini hivi sasa tunatumia jumla ya hekta 290,000, sawa na asilimia noja tu hapa Nchini. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa, bado Kilimo cha Umwagiliaji hatujakipa umuhimu mkubwa. Lazima tukubali kwamba, hapa bado kuna udhaifu. Hivi sasa tumeomba fedha kwa ajili ya Kilimo cha Umwagiliaji, lazima tuzitumie vizuri na kwa ufanisi. Hivyo, naagiza Kilimo cha Umwagiliaji kipewe kipaumbele hasa katika miradi inayoibuliwa na Wananchi Wilayani kupitia *DADPs*. Wataalamu wa Kilimo wawasaidie Wananchi kuibua miradi katika maeneo yao. Serikali kwa upande wake, itaangalia Wataalam wa Kanda watakavyoelekezwa kusaidia Wakulima.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ina nafasi nzuri katika kuleta Mapinduzi ya Kijani. Pamoja na kuwa *ASDP* inatoa msukumo mkubwa katika Kilimo, bado Wananchi hawajaelimishwa na kuhamasishwa kuibua miradi mizuri na yenye kuweza kuleta mabadiliko ya haraka katika Kilimo. Kwa mfano, hivi sasa Wananchi wengi wameanza kupata ufahamu wa Matrekta Madogo, lakini hawakuwa wamepata elimu na fursa ya kuibua miradi ya aina hiyo. Jukumu la Viongozi na Wataalam ni kuipeleka Programu hii karibu zaidi na Wananchi na kuwaelimisha ili waweze kuibua miradi mizuri itakayoongeza tija.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya biashara, lazima tuwasaidie pia Wakulima katika kuongeza tija kwa mazao kama vile Korosho, Kahawa, Tumbaku na Pamba. Hatuna tena muda wa kusubiri, bali Mikoa husika ichukue hatua za kuhakikisha uzalishaji wa mazao haya unaongezeka, kupata bei nzuri na kujumuisha mazao haya kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ili kupata ruzuku ya Serikali.

Uzalishaji wa Kahawa, kwa mfano, hivi sasa Nchini ni sawa na kilo 200 kwa hekta, ikilinganishwa na lengo la kilo 500 kwa hekta, zilizopo katika Mkakati wa Kuendeleza Zao la Kahawa.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija ya zao kama Kahawa ni lazima kupanda kwa wingi miche bora ambayo imefanyiwa utafiti na Kituo cha Utafiti cha *TACRI* na kuonyesha ongezeko la tija kwa mwaka. Lazima sasa kila Mkoa unaolima Zao la Kahawa, kuanzisha bustani za miche bora za mazao ya biashara katika maeneo ya Wakulima ili miche hiyo iwafikie Wakulima haraka. Aidha, ni lazima kuwahimiza kutumia Pembejeo, hasa mbolea za Viwandani na samadi ambayo inapatikana katika maeneo ya Wafugaji yaliyo karibu na mazao haya ya biashara. Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Wakurugenzi wa Wilaya, wajipange vizuri ili waweze kufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, tumejifunza mengi kwa kutumia mfano wa Mikoa sita ya awali tuliyoanza nayo. Kutokana na hali ya Kilimo ilivyo, Uongozi wa Mikoa kwa kushirikiana na Viongozi wa Wilaya, waweke utaratibu wa kujipima. Kuwepo na Mikutano ya kutathmini maendeleo ya Mipango yao ili kujua wamefika wapi na kama kuna matatizo wapange jinsi ya kuyatatua. Sekretarieti za Mikoa zijipange vizuri ili kuweza kuzisimamia Halmashauri katika majukumu yake hasa suala la uzalishaji. Halmashauri ziwe na mikakati mizuri ya uzalishaji badala ya kuwa watumiaji wa fedha tu na Vijiji vibadilike kutoka kuwa Vijiji vya Utawala na kuwa Vijiji vya Uzalishaji na Maendeleo. Lazima tubadilike kimtazamo na kiutendaji kama tunataka kubadili Kilimo chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitapenda kujua kila nikifika kwenye ziara Mikoani ni kwa kiasi gani mabadiliko katika Kilimo yametokea na uzalishaji umeongezeka vipi. Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya asiyeweza kuongoza mabadiliko hayo, hawezi kutusaidia katika kazi hii. Tutawapima kwa vigezo vya mabadiliko katika Sekta za Maendeleo ya Wananchi. Tuanze kwa kuanzisha Mashindano ya Kilimo na kutoa tuzo kwa Mwananchi mmoja mmoja, Vijiji, Wilaya na hata Mikoa itakayoonyesha kwa vitendo mabadiliko ya tija kwenye Kilimo. Tuzo hizi zitatolewa wakati wa Sikukuu ya Nane Nane Kitaifa. Mashindano hayo lazima yaanze mwaka 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeongelea sana Kilimo, lakini kwa Sekta ya Mifugo, Serikali imefanya jitihada za kuiboresha Sekta hiyo. Pamoja na mambo mengine, Serikali imeendelea kutoa Chanjo, kujenga Majosho, Malambo na ununuzi wa dawa mbalimbali za Mifugo. Kwa mfano, Serikali imejenga na kukarabati jumla ya Malambo 158 kupitia Miradi ya *PADEP* na *DADEPs*. Aidha, Serikali imeendelea na jitihada zake za kuboresha Ranchi za Taifa kwa ajili ya uzalishaji bora. Hata hivyo, Serikali inakabiliwa na changamoto nyingi katika Sekta ikiwemo ukosefu wa ardhi ya malisho ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeleta migogoro mikubwa kati ya Wakulima na Wafugaji, ambayo imesababisha uvunjaji wa amani, utulivu, mshikamano na umwagaji wa damu. Ili kuondokana na tatizo hili, tunahitaji kutenga maeneo kwa ajili ya Kilimo na Ufugaji na kuyamilikisha. Ardhi ipimwe na ijulikane imetengwa kwa shughuli gani. Hii

itatusaidia katika kupunguza migogoro inayoendelea kutokea kati ya Wakulima na Wafugaji. Mgogoro unaoendelea hivi sasa katika Wilaya ya Kilosa ni kutokana na kutokuwepo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Kuanzia sasa, naziagiza Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, waanze na kukamilisha zoezi hili la kuweka mipango katika vijiji vyetu ili tupunguze migogoro ya Wakulima na Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawasihi Wananchi ambao ni Wakulima na Wafugaji, kuvumiliana, kuishi kwa amani na kila upande kutumia eneo lake, hivyo kuepusha migogoro, uvunjaji wa amani, umwagaji wa damu na vifo visivyokuwa vya lazima.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inahitaji kuisimamia vizuri rasilimali ya Uvuvi ili kuhakikisha kuwa, Sekta ya Uvuvi inatoa mchango wake katika Kupunguza umaskini kwa Wananchi wetu. Usimamizi mzuri wa Sheria za Uvunaji wa Maliasili za Bahari na Maziwa, utasaidia kuongeza Pato la Taifa kutoka Sekta hii. Hivyo, Serikali inasisitiza kwamba, leseni za shughuli za uvuvi ambazo nyingi hutolewa na Halmashauri za Wilaya, zinapaswa kuwa na masharti yanayoonyesha zana, vifaa vya kila aina vya uvuvi na mahali zana hizo zinapotumika kwa urahisi wa ufuatiliaji. Ningependa kuwakumbusha Wavuvi wote Nchini kuwa wazitumie Ofisi zetu zinazohusika na shughuli za Uvuvi, hasa Maafisa Uvuvi kuhakikisha kuwa wanapata ushauri na ufafanuzi kuhusu masuala yanayohusu Leseni za Uvuvi ili kupunguza matatizo yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, nawasihi Wavuvi na Wadau wote wa Uvuvi Nchini, kusoma kwa makini na kutekeleza yaliyomo kwenye Kauli ya Serikali kuhusu Waraka wa Uvuvi Kuzuia Zana za Uvuvi Haramu Nchini kama ulivyowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge la Bajeti na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, wakati tunakaribia kufikia mwisho wa mwaka 2008, tunatarajia kwamba, Vijana wetu waliofanya Mtihani wa Darasa la Saba watapata majibu yao wakati wowote. Jumla ya Wanafunzi 1,017,865 walifanya mtihani huo, ambapo tunatarajia Wanafunzi 631,076, sawa na asilimia 62 watafaulu. Aidha, tunatarajia Wanafunzi takriban 504,860, sawa na asilimia 80 ya waliofaulu watachaguliwa kuingia Sekondari.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taarifa za awali zinaonyesha kuwa, idadi ya madarasa yanayohitajika ni takriban 12,622 kwa wastani wa Wanafunzi 40 kwa darasa. Wakati tunasubiri matokeo ni lazima tujiweke tayari kupokea Wanafunzi wote watakaofaulu ili waweze kujiunga na Sekondari. Tunao uzoefu wa miaka takriban mitatu iliyotangulia katika kuhimizana kujenga madarasa na Shule za Sekondari za kutosha kuwapokea wote watakaofaulu. Tumefanya vizuri katika kipindi hicho tufanye vizuri katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kuwakumbusha Wakuu wa Mikoa na Watendaji wote kuwa, zoezi hili la kupanua elimu yetu na kuongeza idadi ya

Wanafunzi wanaojiunga na Sekondari ni endelevu, halihitaji kusukumwa na Viongozi wa Kitaifa. Ni wajibu wa Viongozi wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha kuwa wanazo Shule na Madarasa zaidi yatakayotosheleza kupokea Wanafunzi wote watakaofaulu. Itakuwa aibu kwa Mkoa wowote ule utakaoshindwa kupeleka Wanafunzi wake wote watakaofaulu eti kwa vile hakuna madarasa na ni aibu kubwa zaidi kama wote hawa watakaofaulu kwenda madarasani watasoma wakiwa wamekaa chini.

Mheshimiwa Spika, nawaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote, kuhakikisha kuwa Wanafunzi wote watakaofaulu wanapata nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwakani. Tusisubiri kutoa visingizio na sababu za kushindwa. Jambo hili linawezekana, kila Kiongozi atimize wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya kipimo cha kupima ubora wa elimu yetu ni ufaulu wa Wanafunzi katika mitihani ya Kitaifa. Walimu, Wazazi na Wataalam wengine wa elimu, wanapata faraja wanapoona matokeo ya elimu ya Wanafunzi ni mazuri. Kwa mfano, tunayo rekodi nzuri ya ufaulu wa Wanafunzi waliofanya Mtihani wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2007, ambapo kati ya Watahiniwa 192,127 waliofanya Mtihani, waliofaulu Madaraja I – IV walikuwa 162,509, sawa na asilimia 86.2, ikilinganishwa na 116,647 sawa na asilimia 82.3 waliofaulu mwaka 2006 katika Madaraja hayo. Mategemeo yetu ni kwamba, matokeo yatakuwa mazuri zaidi kwa mwaka huu wa 2008. Hiyo ndiyo fahari yetu sote, kwani hutuwezesha kujipima kama Watoto wetu wanaweza kushindana katika soko la ajira au lile la elimu ya juu ndani na nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujivunia matokeo hayo mazuri, lakini sote tumesikia tukio la kuvuja kwa Mtihani wa Hisabati wa Kidato cha Nne mapema mwezi Oktoba, 2008. Hatutarajii kwamba, kufanya kwetu vizuri katika mitihani hii ni matokeo yanayotokana na ujanja wa kupata majibu ya mitihani kabla.

Mheshimiwa Spika, taarifa za kuvuja kwa mitihani ni jambo la aibu na ilipokelewa kwa mshituko mkubwa; sio tu kwa Watahiniwa, bali pia kwa Wazazi na Wananchi wote kwa ujumla. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, kama Taifa tukijenga dhana ya uvujaji wa mitihani ni dhahiri inaathiri aina ya Wataalam watakaopatikana katika Nchi yetu kwa miaka ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukijenga utamaduni huu wa uvujaji wa mitihani katika ngazi hii, Wataalamu wetu hawataweza kushindana katika soko la ajira na katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Vilevile tunawajengea watoto wetu misingi mibovu ya maisha yao. Napenda kuwaasa Wazazi na Wananchi kwa ujumla kwamba, tusishabikie wala kuruhusu utamaduni huu wa Wizi wa Mitihani. Ni aibu kubwa kwa Mzazi kushiriki kwa kumpa fedha mtoto wake ili akanunue mitihani mitaani. Tusikubali kuwapotosha Watoto wetu, kwani kwa kufanya hivyo, tunawatumbukiza katika shimo la kujiharibia maisha.

Vilevile Vyombo vya Habari vitusaidie kupiga vita upungufu huu. Visiwe mashabiki bali viwaongoze Vijana wetu kuwajengea tabia ya kutokimbilia mitihani inayonunuliwa mitaani. Tuwajengee Watoto mazingira na tabia ya kujifunza kwa bidii

kuwa ndio mlango wa kufaulu na hivyo kupata Wanafunzi Bora ambao ndio watakuwa Wataalam bora wa Nchi hii kwa siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchunguza tukio hilo, Serikali itatumia matokeo ya Uchunguzi huo kuimarisha Baraza la Mitihani la Taifa ili tabia hii tuweze kuikomesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, Serikali iliahidi kwamba, ingelipa madeni mbalimbali ya Walimu. Hadi mwezi Septemba, 2008, Serikali iliweza kulipa Malimbikizo ya Mishahara ya Walimu yenye jumla ya shilingi bilioni 7.4. Aidha, hadi tarehe 29 Oktoba, 2008, malimbikizo ya shilingi bilioni 2.3 yalikuwa yamefikishwa Hazina tayari kwa kulipwa. Pamoja na Serikali kulipa madai hayo na kuendelea na zoezi la uhakiki, bado Walimu kupitia Chama chao waliona madai yanachelewa kulipwa na hivyo kuamua kugoma. Wakati akilihutubia Taifa, tarehe 31 Oktoba 2008, Mheshimiwa Rais alieleza kwa kirefu chanzo cha mgomo huo. Mheshimiwa Rais, aliahidi na kuagiza madai ya Walimu yote yahakikiwe na Walimu wenye stahili waanze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madai hayo, Serikali ilifanya uhakiki wa kina na hadi kufikia tarehe 4 Novemba, 2008, uhakiki wa madai ya Walimu ulikuwa umekamilika katika Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji 129 kati ya Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji 133 zilizopo. Halmashauri za Wilaya na Miji ambazo zilikuwa bado ni Ilala, Temeke, Kinondoni na Manispaa ya Dodoma. Uhakiki wa madai ya Walimu katika Halmashauri na Manispaa hizo nao utakamilika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kuzielekeza Halmashauri zote kukamilisha zoezi hili na kutekeleza Maagizo ya Mheshimiwa Rais akiwa ziarani Mkoa wa Tabora kwa umakini. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, wahakikishe usimamizi wa karibu ili matatizo ya madai na madeni ya Walimu hayatokei tena. Vilevile natoa Wito kwa Walimu wachache ambao walionekana kudanganya, kujenga utamaduni wa kuwasilisha madai ya kweli ya stahili zao. Kwa kufanya hivyo, itarahisisha uhakiki wa madeni haya na kupunguza kero ya kucheleweshwa kwa malipo kwa wenzao ambao wamekuwa wakidai malipo halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la utoaji wa mikopo limekuwa likijitokeza Nchini katika miaka ya karibuni, tangu utaratibu huu uanze. Utoaji wa mikopo unaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo Na. 9 ya Mwaka 2004, pamoja na Kanuni na Miongozo iliyowekwa na Serikali. Sheria ya Mikopo pia inaweka bayana masharti ya kutoa mikopo. Hivyo, utaratibu wa kuwabaini wasio na uwezo na wale wenye uwezo unatokana na Sheria. Utaratibu wa kung'amua uwezo wa kiuchumi ndiyo njia pekee iliyopo kwa sasa ya kuwatambua Wanafunzi wenye uwezo kulingana na hali zao kiuchumi. Sera ya uchangiaji pia inalenga kutumia rasilimali kidogo za Serikali ili kuwawezesha Wanafunzi wengi zaidi kupata Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa kawaida, gharama za Elimu zinatakiwa kuchangiwa kati ya Wazazi na Serikali. Kwa mfano, Nchini Kenya wastani wa

Wanafunzi 120,000 wameandikishwa (kudahiliwa) kwenye Vyuo Vikuu Nchini humo, lakini wanaopata mkopo ni 10,000 tu. Kwa upande wa Uganda, kati ya wastani wa Wanafunzi 30,000 wanaodahiliwa kwa mwaka ni 4,000 tu ndio wanaopata mkopo kutoka Serikalini. Kwa upande wa Tanzania, Wanafunzi 60,000 wanapata mikopo kati ya Wanafunzi 80,000 waliodahiliwa katika Vyuo mbalimbali vinavyotoa Elimu ya Juu katika mwaka wa fedha wa 2008/2009. Kazi hii iliyofanyika ukilinganisha na wenzetu wa Kenya na Uganda ni kubwa na inastahili pongezi kwa Serikali. Lazima tujipongeze kwa kazi nzuri ambayo imefanyika kusomesha Watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Uchangiaji inalenga kutumia rasilimali na fedha kidogo za Serikali ili kuwawezesha Wanafunzi wengi zaidi kupata Elimu ya Juu. Kwa hiyo, sio busara Serikali kuwalipia asilimia 100 hata wale Wanafunzi wanaotoka kwenye familia zenye uwezo. Kwa kufanya hivyo, kwa Bajeti ya mwaka 2008/2009 ya shilingi bilioni 119 ni Wanafunzi 42,000 tu ndio wangeweza kukopeshwa badala ya 60,000 wanaopata sasa hivi.

Kwa maneno mengine, kuwapatia Wanafunzi wote 60,000 mkopo wa asilimia 100, kiasi cha shilingi bilioni 163.7 zingehitajika. Kwa upande mwingine, utaratibu huu umewasaidia sana Wazazi wasio na uwezo. Mimi najiuliza ni kwa nini Mtoto wa Waziri Mkuu, Spika, Mbunge au wa Mfanyabiashara Maarufu, ambao wana uwezo wa kusomesha Watoto wao katika Vyuo Vikuu wafaidike na utaratibu huu ambao tuna uwezo nao badala ya kusaidia wasio na uwezo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuelewe kwamba, Sera ya Uchangiaji Gharama za Elimu ya Juu si jambo geni kwa Nchi nyingi Duniani. Hapa kwetu, utaratibu huu haupo katika Elimu ya Juu pekee, bali upo katika Elimu ya Sekondari, Vyuo na pia katika huduma nyingine za jamii kama vile Afya, Maji na Nishati. Mchango wa Serikali katika Elimu ya Juu ni mkubwa ukilinganisha na mkopo wa Mwanafunzi kwa ajili ya Elimu ya Juu. Kwa ujumla gharama wanazolipa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ni za chini sana ukilinganisha na gharama halisi.

Mheshimiwa Spika, gharama halisi ya Kozi ya Udaktari wa Binadamu kwa mfano kwa Chuo Kikuu cha Muhimbili ni shilingi milioni 4.3, lakini Mwanafunzi hulipa shilingi milioni 1.0 tu kwa mwaka kupitia kwenye mkopo anaopewa (kwa wasio na uwezo).

Ada halisi kwa Kozi ya Udaktari wa Wanyama, Chuo Kikuu cha Sokoine ni shilingi milioni 3.2 kwa mwaka, lakini Mwanafunzi hulipa shilingi milioni 1.2 tu. Kwa upande wa Shahada ya Biashara, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, gharama halisi ni shilingi milioni 3, lakini Mwanafunzi hulipa shilingi milioni 1.25 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutolipa ada halisi, mikopo wanayolipa Wanafunzi kwa kipindi cha miaka 10 huwa haina riba. Hii ina maana kuwa, thamani ya fedha wanazolipa Wanafunzi ni kidogo sana ukilinganisha na thamani ya fedha wakati walipokopa. Kwa hali ya kawaida, hii mikopo ilitakiwa ilipiwe riba na Wanafunzi, lakini kwa sasa Serikali inabeba mzigo huo.

Mheshimiwa Spika, hatuna uchaguzi mwingine bali kuendelea kuchangia gharama za elimu ili Wanafunzi wengi zaidi wapate Elimu ya Juu. Napenda nirudie kusema kwamba, Serikali wakati wote itakuwa mstari wa mbele kuhakikisha Wanafunzi wanapata kile wanachostahili kujiendeleza kielimu. Naomba nitamke kuwa, Wanafunzi wale wanaotaka kupewa mikopo asilimia 100 haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Serikali kuwalipia Watoto wa Waziri Mkuu, Spika, Wabunge na Wafanyabiashara wakubwa. Tutaendelea na utaratibu uliopo kwa kuwa unawasaidia wazazi ambao uwezo wao ni mdogo na hivyo kutuwezesha kupata wanafunzi wengi zaidi katika vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni, Nchi yetu pia imeshuhudia matukio kadhaa ya Migomo na Maandamano, yanayofanywa na Vikundi mbalimbali kwa kile kinachoelezwa kuwa ni njia mojawapo ya Vikundi hivyo kudai haki zao. Matukio ya aina hiyo ni pamoja na Migomo na Maandamano ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu, Migomo ya Wafanyakazi wa Kampuni ya Reli Tanzania, Migomo ya Madaktari na Wauguzi katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili, Migomo ya Wafanyakazi wa NMB, Maandamano na tishio la Mgomo wa Walimu, Maandamano ya waliokuwa Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Migomo midogo midogo katika maeneo mbalimbali ya Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Serikali haipingi kufanyika kwa Migomo na Maandamano ambayo yanafuata Kanuni na Taratibu zilizowekwa Kisheria. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004, inatoa Uhuru wa Wafanyakazi kugoma ila tu wafuate Taratibu na Kanuni. Hata kwa upande wa Maandamano, yanaruhusiwa ila tu yanapaswa kupata Kibali cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa baadhi ya matukio ya hivi karibuni ambayo tumeyashuhudia, zipo dalili zinazoashiria kuwa, baadhi ya Vikundi vinavyohusika na kuandaa Maandamano na Migomo, vimefanya hivyo bila ya kufuata Sheria. Aidha, baadhi ya Maandamano na Migomo hiyo imetishia Usalama, Amani, Utulivu na Mshikamano wa Nchi yetu na hivyo kulazimisha Vyombo vya Dola kuingilia kati.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, Maandamano na Migomo yote ya Wafanyakazi inayotokea sehemu za kazi hasa zile zinazohusika na utoaji wa huduma muhimu kwa jamii, inaleta athari kubwa kwa Taasisi husika na Uchumi wa Nchi kwa ujumla. Kwa mfano, mgomo uliofanywa na Wafanyakazi wa Kampuni ya Reli Tanzania, ulisababisha Wananchi wengi kupata usumbufu na kuchelewa kufika wanakokwenda na wengine kukatiza safari zao. Vilevile shehena za mizigo zilikwama na hivyo kuwasababishia Wafanyabiashara hasara kubwa na zaidi ya yote, kudumaza shughuli za kiuchumi zinazotegemea Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi Nchini.

Vilevile Mgomo wa Madaktari Wanafunzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ulisababisha Wagonjwa wengi wasio na hatia, kukosa huduma muhimu za tiba. Maandamano yaliyofanywa na Wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao tarehe 28 Oktoba, 2008 walifunga Barabara za Ali Hassan Mwinyi na ile ya Umoja wa

Mataifa, Jijini Dar es Salaam, ni dhahiri yalisababisha kero kubwa kwa Wananchi wengi ambao kwa njia moja au nyingine, hawahusiki na wala sio Wadau kwa madai ya Wastaafu hao.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kujiuliza kama ni busara Makundi ya Wafanyakazi wa Taasisi mbalimbali Nchini, kutumia migomo katika kutetea maslahi yao, bila wahusika kutoa muda wa kutosha wa majadiliano wala kujali maslahi ya Umma na Wananchi wanaowahudumia. Ukweli ni kwamba, hasara na athari kubwa za migomo, pamoja na usumbufu, kero na mateso wanayopata Wananchi na Taifa kwa ujumla na kuzorota kwa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo kutokana na Migomo hiyo, haziwezi kulinganishwa na madai ya makundi ya Wafanyakazi wachache wanaoongoza migomo hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba, Wafanyakazi, Wanafunzi na Wananchi wengine wowote wanaoitisha na kufanya migomo ni vyema watambue kuwa pamoja na Serikali kuruhusu migomo katika mazingira fulani kisheria, ni lazima maslahi ya Umma yazingatiwe na kulindwa kwanza. Serikali inatoa wito kwa Makundi yote Nchini, kuacha kutumia migomo kama njia pekee ya kupata haki, kwani Migomo ina athari nyingi kama nilivyokwishaeleza. Kwa misingi hiyo, Serikali haitawavumilia wahusika wanaochochea migomo isiyo ya lazima na isiyofuata sheria, taratibu na kanuni, kwani ina athari kubwa kiuchumi na inahatarisha amani, utulivu na usalama wa nchi yetu. Vyama vya Wafanyakazi vilivyopewa dhamana ya kisheria kutetea haki za wafanyakazi, pamoja na kudumisha mahusiano mazuri kazini, vina wajibu mkubwa wa kuepusha migomo isiyo ya lazima. Ni vyema vyama hivyo vifanye kazi zake kwa kufuata Taratibu zinazokubalika Kisheria. *(Makofi)*

Vivyo hivyo, Serikali haitavumilia Watendaji wake wote wanaosababisha au kushindwa kutatua kero za wananchi hadi wananchi wafikie hatua ya kufikiria migomo, wakati uwezo wa kutatua kero zao wanao. Jukumu la Serikali iliyoko madarakani ni kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali za Wananchi, kulingana na uwezo uliopo. *(Makofi)*

Naomba nitumie fursa hii, kusisitiza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwa kuwaomba Wananchi wote kujenga dhana na utamaduni wa uvumilivu. Tujenge utamaduni uliokomaa Kidemokrasia. Mimi ninaamini kwamba, migogoro yote ina njia inayofaa katika kuitatua. Tuzungumze, tukubaliane; kwa njia hiyo tunaweza kuepusha athari ambazo zingeweza kuepukika. Hebu tukae kwa pamoja tufikirie tena jinsi ya kupunguza matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nizungumzie kidogo kuhusu matatizo ya Walemavu Nchini. Inakadiriwa kwamba, nchi yetu ina Watu wenye Ulemavu wapatao milioni 3.5. Hawa wanajumuisha Walemavu wa viungo, wasioona, viziwi, ulemavu wa akili, ulemavu mchanganyiko na ulemavu mwingine. Serikali inatambua umuhimu wa watu wenye ulemavu katika maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, ipo dhana iliyojengeka miongoni mwetu kwamba, watu wenye ulemavu hawawezi kazi wala shughuli yoyote. Dhana hii si sahihi hata kidogo na ni dhana potofu. Dhana hii potofu inapingana na mambo makubwa ambayo Walemavu wanaweza kufanya kuchangia maendeleo ya Taifa. Kwa mfano, sote

tuliona jinsi watu wenye ulemavu walivyoleta msisimko kwenye michezo ya Olimpiki iliyomalizika kule Nchini China hivi karibuni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kila mwananchi ana haki sawa kisheria ya kushiriki kikamilifu katika mambo muhimu yanayomhusu yeye mwenyewe na jamii nzima kwa ujumla. Watu wenye Ulemavu wana haki ya kupata mahitaji ya msingi, sambamba na Wananchi wengine wasio na ulemavu. Kimsingi, hawa ni wenzetu katika jamii, ambao kwa maumbile yao wanahitaji maangalizi ya pekee katika jamii. Kwa maana hiyo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha mahitaji yao yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kwamba, hadi sasa Serikali ina Vituo vya Watu wenye Ulemavu wa aina mbalimbali, vinavyotoa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo:-

Shule za Msingi Maalum kwa Wasioona tatu; Ulemavu wa Akili tano; Ukiziwi kumi; na Ulemavu wa Viungo tano.

Shule za Sekondari kwa Wasioona kumi na tano; Ulemavu wa Akili mbili ; Ulemavu wa Viungo tatu; na Ukiziwi nane.

Mwisho, Vyuo vya Ufundi kwa Wasioona tunacho kimoja na Ulemavu mchanganyiko sita.

Serikali inavihudumia Vituo hivi takriban 58 kwa kuandaa Walimu wa Elimu Maalum; Kutoa vifaa vya kufundishia; Kutoa nyenzo za kujimudu; Kuboresha miundombinu katika mazingira ya shule; na kutoa chakula, malazi na huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuihakikishia jamii ya Watu wenye Ulemavu na Wananchi wote kwa ujumla kwamba, Serikali inawajali na inatambua matatizo yao. Vilevile Serikali imeandaa mikakati ya kukabili matatizo ya Watu wenye Ulemavu nchini. Kubwa katika hili ni Kuandaa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria Na. 2 ya Mwaka 1982 ili kutoa nafasi ya kuboresha zaidi huduma kwa watu wenye ulemavu katika nyanja za ajira, miundombinu, elimu na upatikanaji wa vifaa kwa urahisi.

Kupitia Bunge hili, naomba kuziagiza Wizara zinazohusika na huduma za Walemavu, ikiwemo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; na Wizara ya Fedha na Uchumi, kushirikiana kukamilisha Miongozo yote inayohusu Watu wenye Ulemavu Nchini. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, iratibu zoezi hili na nipate Taarifa ya Utekelezaji kabla ya Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utunzaji wa Mazingira Uhai na Ustawi wa Nchi yetu, unategemea kwa kiasi kikubwa Hifadhi na Utunzaji wa Mazingira. Ukizunguka sehemu mbalimbali za Tanzania, utakuta sehemu mbalimbali zimechomwa moto na unaweza kudhani yapo mashindano maalum ya uchomaji moto nchini. Kumekuwa na utamaduni miongoni mwa Watanzania; wakulima na wafugaji wa kuchoma moto maeneo

mbalimbali Vijijini. Wakulima huchoma moto nyasi kwa ajili ya kurahisisha utayarishaji wa mashamba, wakati wafugaji huchoma moto ili kuwezesha majani mabichi kuchipua kwa ajili ya mifugo yao. Vilevile kuna sehemu za nchi ambapo wana imani kuwa anayechoma moto na kuwaka kwa muda mrefu, ana mkono mzuri. *(Makofi/Kicheko)*

Yapo baadhi ya maeneo hapa Tanzania vilevile huchoma mioto kwa ajili ya kurahisisha uwindaji wa wanyama na wengine kwa ajili ya kutafuta wanyama wadogo sana kama panya kwa ajili ya kitoweo. Utamuduni huu umepitwa na wakati. Kuchoma moto ovyo, kunaharibu mimea ambayo mingine huwa ni mazao ya chakula na hivyo kuleta ukame na njaa. Matokeo ya ukame na njaa ni kuongezeka kwa umaskini. Uchomaji wa moto ovyo huua viumbe hai wanaoishi kwenye majani na ardhini. Wataalam wanatueleza kuwa, viumbe hivyo ni muhimu kwa kurutubisha ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuna uharibifu wa Mazingira unaoendelea kufanywa kwenye vyanzo vya maji. Miti inakatwa ovyo na vyanzo hivyo vimekuwa malisho maarufu ya idadi kubwa ya mifugo. Matokeo ya kufanywa hivyo ni kukauka kwa vyanzo hivyo vya maji. Tujiulize; itakuwaje binadamu, wanyama na mimea vitakapokosa maji? Ni wazi kuwa maji ni uhai na bila maji hakuna uhai.

Tumeharibu sana mazingira, hali hii imesababisha maeneo mengi kukosa mvua na kuwa na upungufu wa uzalishaji wa mazao. Ni muhimu Wananchi wakazidi kufahamishwa madhara yatokanayo na kuchoma moto ovyo na kuharibu vyanzo vya maji. Halmashauri ziwe na Sheria zinazodhibiti uchomaji moto ovyo, uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla wake. Sheria hizo zisimamiwe na kutekelezwa kwa kushirikisha Viongozi wa Vijiji, Kata na Wilaya. Pia ni wakati sasa wa kuelekeza rasilimali za kutosha katika kulinda uhai wa viumbe hai vyote, ikiwa ni pamoja na sisi wanadamu. Tupande miti mara kwa mara kwenye vyanzo vya maji, mashamba yetu, nyumba zetu, kando kando ya barabara na kadhalika. Pamoja na Siku ya Kupanda Miti Kitaifa ni vizuri kila Mkoa ukawa na siku maalum ya kupanda miti inayoendana na hali yake ya Hewa. Badala ya kuwa na mashindano ya kuharibu mazingira, tuwe na mashindano ya kulinda mazingira katika ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. Natumaini kila mmoja wetu, atajisikia vizuri kuzungukwa na uoto wa asili na ikiwa upatikanaji wa maji halitakuwa tatizo kwenye jamii. Hilo liwe ndilo lengo letu kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunatekeleza malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), tuelekeze nguvu zetu kutumia fursa zilizopo kutekeleza Mkakati huu. Twendeni tukawahimize Wananchi kushiriki katika Maendeleo yao. Mambo ya Msingi ambayo napenda kuyasisitiza ni haya yafuatayo: -

Kwanza, tunayo nafasi nzuri ya kutumia rasilimali zilizopo hususan madini kuinua uchumi wetu. Tutumie nafasi iliyopo kwa kuyaongezea thamani madini yetu badala ya kuyauza ghafi. Tuanze kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Kwa kufanya hivyo tutafanikiwa. *(Makofi)*

Pili, tunatoka Bungeni wakati Msimu wa Kilimo umekaribia. Twendeni tukasukume Mapinduzi ya Kilimo. Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wakurugenzi wa Wilaya na Madiwani, tusukume hili ili iwe dhambi kutozingatia Kanuni Bora za Kilimo. Tuanze kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa pembejeo muhimu kwa Kilimo ikiwemo Mbolea, Mbegu Bora na Dawa za Kuuwa Wadudu waharibifu, ili kuongeza tija.

Tatu, tujenge dhana ya uvumilivu. Tuepuke kujenga tabia ya kuona kwamba, Maandamano na Migomo ndiyo njia ya kutatua migogoro. Bado Serikali yetu ni nzuri, inajitahidi kukamilisha mahitaji yote ya walimu, wastaafu mbalimbali na matatizo ya wanafunzi. Kubwa tuwe na subira na tushirikiane. *(Makofi)*

Nne, tushirikiane kuwasaidia watu wenye ulemavu, kwani ni sehemu ya jamii yetu. Tuwape moyo, tuwasaidie pale inapobidi ili waweze kushiriki katika kujiletea maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunahitimisha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Tumebakiza Mikutano takriban saba tu kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010. Sisi sote, kila mmoja wetu ndani ya Bunge hili, bila kujali itikadi ya Chama chake ni lazima ujiulize; kuwepo kwetu ndani ya Bunge hili tumewasaidiaje Wananchi wetu tunaowawakilisha. Ni vyema kila mmoja wetu kuanza kujifanyia tathmini mwenyewe ya kitu gani alichokifanya cha kuwaondolea wananchi wake Umaskini. *(Makofi)*

Je, umeshiriki vipi katika kuwaondolea Wananchi kero ambazo zinawakabili? Kila mmoja ajipime mwenyewe kujua kama kuwepo kwake ndani ya Bunge hili, ametumia muda wake katika kupunguza kero za wananchi au ndio amewazidishia ukali wa maisha. Twendeni nyumbani tukatumie muda wetu kutafakari yote yale ambayo yanatuhusu, tuyafanye kwa manufaa ya wananchi wetu. *(Makof/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru wote waliosaidia katika kufanikisha Mkutano huu. Nakushukuru kwa namna ya pekee wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kutuongoza vizuri. Nawashukuru Wenyeviti wa Bunge, kwa msaada mkubwa walioutoa kuliongoza Bunge hili. Nawashukuru sana Wenyeviti wa Kamati mbalimbali na Wabunge wote kwa michango yenu mbalimbali, wakati wa kujadili Miswada tuliyoipitisha katika Mkutano huu. *(Makofi)*

Namshukuru Kaimu Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Wasaidizi wake, pamoja na Wataalam wa Serikali, kwa kazi nzuri ya kutoa misaada ya Kitaalam na huduma mbalimbali katika kufanikisha Mkutano huu. Navipongeza Vyombo vya Habari, kwa kuwafikishia wananchi habari ya yale yaliyojitokeza hapa Bungeni kwa wakati na usahihi. Mwisho, nawapongeza madereva kwa kazi kubwa kubwa ya kuwaendesha Waheshimiwa Wabunge kwa usalama. Pia nawapongeza askari wote waliotusaidia ulinzi wote, kwa namna ya pekee kwa kazi yao nzuri ya ulinzi. Wote ahsanteni sana kwa kazi yenu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ni tarehe 7 Novemba, 2008, katika kipindi cha takriban mwezi mmoja na nusu, tutakuwa tumefikia mwisho wa mwaka 2008. Ni matumaini yangu kwamba, *Inshallah* Muumba wetu atatujalia sote kama tulivyo, kuumaliza mwaka

huu na kuuanza mwaka mwingine salama. Napenda nitumie nafasi hii, kuwatakieni wote Heri, Baraka na Fanaka tele ya Sikukuu ya Krismas na Mwaka Mpya wa 2009. *(Makofi)*

Nawatakia wote safari njema ya kurejea kwenye Majimbo yenu na nyumbani kwenu. Wale tutakaopata nafasi ya kwenda hadi majumbani, basi kila heri mwende salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 27 Januari, 2009, Siku ya Jumanne Saa Tatu Asubuhi, litakapokutana tena kwa ajili ya Mkutano wa Kumi na Nne kwenye Ukumbi huu hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge, mtaungana nami kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ambayo imelenga sawa sawa katika majukumu ambayo yanatukabili mbele yetu. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Kabla sijawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina matangazo machache; kwanza, ile semina ya Benki Kuu inayohusu mtikisiko wa soko la mitaji na fedha ulimwenguni imeahirishwa na sababu ya kuahirishwa ni kwamba, Magavana wa Benki katika Kanda yetu ya Afrika Mashariki, toka jana wanakutana Arusha na Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* na Benki ya Dunia. Kwa hiyo, hata ule waraka waliokuwa wanauandaa kwa ajili ya semina, itabidi ubadilike kwa kuzingatia kwamba, tatizo hili sasa limebainika kuwa ni kubwa na lina athari za muda mrefu zaidi katika dunia.

Kwa hiyo, isingewezekana hata kidogo, kwanza sisi ndiyo wenyeji maana yake ni Arusha, Gavana asingeweza kuja hapa huku jambo hilo linaendelea. Kwa hiyo, ni vyema tu tutapanga katika mkutano ujao ili semina hiyo muhimu sana iweze kufanyika. Nimearifiwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, pengine itahitaji siku mbili kutokana na uzito wa jambo hilo, hiyo ndiyo sababu.

La pili, naomba nikumbushe kwamba ile semina ya viongozi, yaani Wenyeviti wa Kamati za Bunge, Makamu Wenyeviti na Waheshimiwa Mawaziri watakaoweza, inayohusu Kanuni za Bunge itafanyika Ofisi Ndogo Dar es Salaam Jumanne ijayo tarehe 11 Novemba, 2008 ilipangwa kesho lakini tumesogeza mbele.

Mwisho, naungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuyashukuru makundi yote aliyoyataja bila kurudia rudia ambayo ni kinyume cha kanuni. Kwa hiyo, labda niseme tu nawashukuru Wabunge wote kwa mkutano mzuri huu wa kumi na tatu tunaomaliza leo. Sasa tutahitimisha kwa kuwahoji na nikishawahoji tutabakia kwa wimbo wa Taifa na ukishapigwa Wimbo wa Taifa ndiyo tatamka kuahirisha rasmi Bunge letu.

Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, Bunge liahirishwe hadi tarehe hiyo aliyoitaja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Naomba sasa tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiwa mmesimama sasa naliahirisha Bunge hili hadi siku ya Jumanne, tarehe 27 Januari, 2009, Saa Tatu Asubuhi katika Ukumbi huu huu.

*(Saa 7.15 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 27 Januari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*